ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR
MHE. PANDU AMEIR KIFICHO - SPIKA

1.Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	MBM/Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa na Rais
2.Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Dimani.
3.Mhe. Omar Yussuf Mzee	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo/ Kuteuliwa na Rais
4.Mhe. Haji Omar Kheri	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora/Jimbo la Tumbatu
5.Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais/Kuteuliwa
6.Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa
7.Mhe. Abubakar Khamis Bakary	MBM/Waziri wa Katiba na Sheria/Jimbo la Mgogoni.
8.Mhe. Rashid Seif Suleiman	MBM/Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Ziwani.
9.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Donge
10.Mhe. Juma Duni Haji	MBM/Waziri wa Afya/Kuteuliwa

11.Mhe. Zainab Omar Mohammed	MBM/Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto/Kuteuliwa
12.Mhe. Said Ali Mbarouk	MBM/Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo/Jimbo la Gando
13.Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban	MBM/Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Kuteuliwa.
14.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	MBM/Waziri wa Kilimo na Maliasili/Jimbo la Jang'ombe
15.Mhe. Nassor Ahmed Mazrui	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Mtoni
16.Mhe. Abdillah Jihad Hassan	MBM/Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Magogoni
17.Mhe. Haroun Ali Suleiman	MBM/Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika/Jimbo la Makunduchi
18. Mhe. Shawana Bukheti Hassan	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/ Jimbo la Dole
19. Mhe. Haji Faki Shaali	MBM/ Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Mkanyageni
20.Mhe. Machano Othman Said	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Chumbuni.
21.Mhe. Othman Masoud Othman	Mwanasheria Mkuu

22.Mhe. Issa Haji Ussi	Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Chwaka
23.Mhe. Zahra Ali Hamad	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake
24.Mhe. Dr. Sira Ubwa Mamboya	Naibu Waziri wa Afya/Kuteuliwa na Rais
25.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	Naibu Waziri wa Habari,Utamaduni,Utalii na Michezo/ Nafasi za Wanawake
26.Mhe. Haji Mwadini Makame	Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Jimbo la Nungwi
27.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi	Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Fuoni
28.Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak	Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili/Nafasi za Wanawake
29. Mhe. Mohammed Said Mohammed	Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi/ Jimbo la Mpendae
30.Mhe. Abdalla Juma Abdalla	Jimbo la Chonga
31.Mhe. Abdalla Moh'd Ali	Jimbo la Mkoani
32. Mhe. Ali Mzee Ali	Kuteuliwa
33.Mhe. Abdi Mosi Kombo	Jimbo la Matemwe
34.Mhe. Ali Abdalla Ali	Jimbo la Mfenesini
35. Mhe. Ali Salum Haji	Jimbo la Kwahani
36.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Nafasi za Wanawake

37. Mhe. Asaa Othman Hamad	Jimbo la Wete
38.Mhe. Asha Abdu Haji	Nafasi za Wanawake
39.Mhe. Asha Bakari Makame	Nafasi za Wanawake
40.Mhe. Ashura Sharif Ali	Nafasi za Wanawake
41.Mhe. Bikame Yussuf Hamad	Nafasi za Wanawake
42.Mhe. Farida Amour Mohammed	Nafasi za Wanawake
43.Mhe. Fatma Mbarouk Said	Jimbo la Amani
44.Mhe. Hamad Masoud Hamad	Jimbo la Ole
45.Mhe. Hamza Hassan Juma	Jimbo la Kwamtipura
46.Mhe. Hassan Hamad Omar	Jimbo la Kojani
47.Mhe. Hija Hassan Hija	Jimbo la Kiwani
48.Mhe. Hussein Ibrahim Makungu	Jimbo la Bububu
49.Mhe. Ismail Jussa Ladhu	Jimbo la Mji Mkongwe
50.Mhe. Jaku Hashim Ayoub	Jimbo la Muyuni
51.Mhe. Kazija Khamis Kona	Nafasi za Wanawake
52.Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa	Jimbo la Kikwajuni
53.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk	Jimbo la Kitope
54.Mhe. Mansoor Yussuf Himid	Jimbo la Kiembesamaki
55.Mhe. Marina Joel Thomas	Kateuliwa na Rais
56.Mhe. Mbarouk Wadi Mussa	Jimbo la Mkwajuni
57.Mhe. Mgeni Hassan Juma	Nafasi za Wanawake
58.Mhe. Mlinde Mbarouk Juma	Jimbo la Bumbwini

59.Mhe. Mohammed Haji Khalid Jimbo la Mtambile

60.Mhe. Mohammed Mbwana Hamad Jimbo la Chambani

61.Mhe. Mussa Ali Hassan Jimbo la Koani

62.Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali Jimbo la Uzini

63.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa Nafasi za Wanawake

64.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi Nafasi za Wanawake

65.Mhe. Nassor Salim Ali Jimbo la Rahaleo

66.Mhe. Omar Ali Shehe Jimbo la Chake-Chake

67.Mhe. Panya Ali Abdalla Nafasi za Wanawake

68.Mhe. Raya Suleiman Hamad Nafasi za Wanawake

69.Mhe. Rufai Said Rufai Jimbo la Tumbe

70.Mhe. Saleh Nassor Juma Jimbo la Wawi

71.Mhe. Salim Abdalla Hamad Jimbo la Mtambwe

72.Mhe. Salma Mohammed Ali Nafasi za Wanawake

73.Mhe. Salma Mussa Bilali Nafasi za Wanawake

74.Mhe. Salmin Awadh Salmin Jimbo la Magomeni

75.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman Nafasi za Wanawake

76.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha Jimbo la Mwanakwerekwe
77.Mhe. Subeit Khamis Faki Jimbo la Micheweni
78.Mhe. Suleiman Hemed Khamis Jimbo la Konde
79.Mhe. Ussi Jecha Simai Jimbo la Chaani
80.Mhe. Viwe Khamis Abdalla Nafasi za Wanawake
81.Mhe. Wanu Hafidh Ameir Nafasi za Wanawake

Ndugu Yahya Khamis Hamad Katibu wa Baraza la Wawakilishi

Kikao cha Kumi na Sita - Tarehe 5 Julai, 2013

(Kikao kilianza saa 3.00 Asubuhi)

DUA

Mhe. Mwenyekiti (Mgeni Hassan Juma) alisoma dua

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, kabla ya kuanza kikao chetu naomba nitoe matangazo mawili. Tangazo la kwanza linahusu vitambulisho, ambayo ni taarifa kwa Waheshimiwa na Watendaji ambao hawajachukua vitambulisho vyao vya taifa, wanaombwa kufika chumba cha kusomea juu kuanzia hivi sasa kwa ajili ya kupatiwa vitambulisho vyao. Pia wale ambao hawajapiga picha au kusajiliwa na wao wanaombwa kufika hivi sasa kwa ajili ya kufanya shughuli hiyo.

Tangazo la pili Waheshimiwa Wajumbe, kama ilivyo kawaida yetu tukipata wageni tunawatambulisha. Kwa hiyo naomba kuwatambulisha wanafunzi kutoka Skuli ya Mwanakwerekwe F, wanafunzi hawa ni walemavu wenye mahitaji maalum, na wanafunzi hawa ni kati ya wale wanafunzi ambao waliokuja juzi, wageni wetu karibuni sana (Makofi).

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 146

Kukosekana Kanuni za Sheria ya Watu Wenye Ulemavu Zanzibar

(*Mhe. Mjumbe aliyetaka kuuliza swali hilo ameliondoa)*

Nam. 118

Matengenezo ya Barabara ya Kijini – Matemwe

Mhe. Kazija Khamis Kona – Aliuliza:

Kwa kuwa wananchi wa Kijini – Matemwe wametaabika kwa muda mrefu sana na miundo mbinu mibovu ya barabara, na kwa kuwa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwa nia njema kabisa imeanza kuwajengea barabara hiyo wananchi wa Kijini kwa kiwango cha kifusi, na kwa kuwa barabara hiyo hivi sasa imechimbika sana kutokana na mvua kubwa zilizonyesha.

(a) Je, Serikali imejipanga vipi katika kuweka kifusi kipande cha barabara hiyo chenye urefu wa kilomita 3 tu ili wananchi hao waweze kufaidika na matunda ya Mapinduzi kama wenzao.

(b) Ni lini hasa barabara hii itajengwa na kukamilika kwa kiwango cha lami ili kuwaondolea usumbufu wananchi hao.

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano – Alijibu:

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi suali lake Nam. 118 (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, napenda kuchukua fursa hii kumpongeza Mhe. Mjumbe kwa kutambua juhudi zinazochukuliwa na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar ya awamu ya sita kwa kuleta maendeleo mbalimbali nchini yakiwemo ya ujenzi na matengenezo ya miundombinu ya barabara.

Barabara ya Kijini-Matemwe (7.5km) na Kijini-Mnemba (3.5km) ni miongoni mwa barabara sita za vijijini (*Rural roads*) zilizopangwa kwanza kufanyiwa upembuzi yakinifu (*feasibility study*) na wa kina (*detail engineering design*) na Kampuni ya *ICT* ya India mnamo mwezi Juni 2013. Kazi hiyo itachukua muda wa mwaka mmoja kwa mkopo nafuu kutoka Benki ya Maendeleo ya Afrika (*AFDB*). Aidha katika mwaka wa Fedha 2011/2012, Wizara yangu kupitia Idara ya Ujenzi na Utunzaji Barabara (*UUB*) iliifanyia matengenezo makubwa kwa kuijenga kwa kiwango cha kifusi barabara ya Kiashange – Kijini *School* (6.5km) kwa kutumia fedha za Mfuko wa Barabara ili iweze kupitika kwa urahisi na wakati wote,

Mhe. Spika, barabara hiyo imesaidia wananchi kwa kiasi kikubwa kusafirisha bidhaa zao kutoka sehemu mbalimbali ilipoishia barabara hiyo (Kijini *School*). Wizara inatambua umuhimu wa barabara ya Kijini – Matemwe (7.5km) na nyenginezo zilizomo jimboni kwa Mhe. Mjumbe. Kutokana na umuhimu huo, Wizara ililiona hilo na ndiyo maana ikachukua hatua ya kutafuta wafadhili wa kuzifanyia upembuzi yakinifu na kina barabara ya Kijini – Matemwe na Kijini – Mnemba zenye jumla ya urefu wa km 11 ili baadae ziweze kujengwa kwa kiwango cha lami. Aidha namshauri Mhe. Mjumbe atumie fedha zake kwa jimbo kuifanyia matengenezo madogo madogo barabara aliyoitaja hapo awali kwa kiwango cha lami.

Mhe. Kazija Khamis Kona: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwanza nampongeza Mhe. Naibu Waziri na naomba kumuuliza suali la nyongeza. Mhe. Naibu Waziri, kwa kuwa wananchi wa Kijini wanasumbuka sana na

ubovu wa njia hivi sasa ilivyokuwa. Sasa je Mhe. Naibu Waziri, utaupanga utaratibu gani kuona gari za abiria nazo zinaenda kule maeneo ya Kijini ili abiria wale wasipate usumbufu.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, kwa idhini yako na kwa niaba ya Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano naomba kumjibu Mhe. Kazija Khamis Kona, suali lake la nyongeza kama ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, msingi mkubwa wa Wizara yetu ni kuimarisha huduma za miundombinu. Aidha tunatambua miundombinu ikiimarika huduma za usafiri nazo zitaimarika, malengo yetu hatuna vikwazo, tutaendelea kuwashawishi na tutaendelea kutoa wito kwa wananchi na wafanyabiashara waweze kutumia fursa hiyo ya uimarishaji na miundombinu ya barabara na wao waweze kupeleka huduma hizi za usafiri wa magari kwa wananchi wetu. Tunatambua barabara zikiwa mbovu huduma za usafiri hazitoimarika, lakini malengo yetu kama barabara zikiimarika tuna hakika kwamba huduma hizi za usafiri nazo zitaimarika zaidi na kutoa huduma bora kwa wananchi wetu, kwa msingi huo nimwambie tu Mhe. Mwakilishi kwamba tutaendelea kuwashajihisha wafanyabiashara waweze kupeleka magari ya biashara ili kuweza kutoa huduma za usafiri kwa wananchi hao wa kijiji cha Matemwe Kijini.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, katika suali kama hili limefanana na watu wa Kijiji cha Mfumbwi, Jambiani, Bwejuu na baada ya kutegemea zao la karafuu Mwenyezi Mungu ajaalie iendelee kuzaa tukikosa hilo tunategemea watalii na kule kuna hoteli karibu sita mpaka nane, tokea dunia ilipoanza wananchi wale hawana barabara wana jangwa. Ni lini kama wewe ni Naibu Waziri dhamana hivi sasa wananchi wa Jimbo la Muyuni hasa Jambiani Mfumbwi wanataka kusikia, ni lini japo kifusi utawatilia.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, kwa idhini yako na kwa niaba ya Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano, naomba kumjibu Mhe. Jaku Hashim Ayoub, Mwakilishi wa wananchi Jimbo la Muyuni suali lake la nyongeza kama ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, katika majibu mama tumeeleza kwamba Wizara ya Miundombinu jukumu lake la msingi ni kujenga barabara, na barabara hizi ziko kwa viwango. Kiwango cha barabara anayoisema Mhe. Mwakilishi hakiangukii moja kwa moja katika majukumu ya msingi ya Wizara yetu. Ninachoendelea kumuahidi Mhe. Mwakilishi, sisi kama Wizara, tutaendelea kutoa aina ya ushirikiano ikiwa kama vifaa, ufundi pamoja na watendaji kazi kwa maana ya kwamba watendaji wetu au mafundi wetu.

Tunamuomba Mheshimiwa Mwakilishi, kwa mapenzi yale yale aliyokuwa nayo kwa wananchi wake nasi atupe ushirikiano kutusaidia gharama za mafuta, tuko tayari kwenda kuwasaidia wananchi hawa wa Jambiani, Mfumbwi, Kibigija, Kichakanyuki, Kichaachoni na kwengineko kote. Hatuna upendeleo kupeleka huduma hiyo isipokuwa utaratibu wa Serikali hatuna mafungu yanayoturuhusu moja kwa moja kwenda kufanya kazi hizo. Hivyo nimwambie tu Mhe. Mwakilishi atupe ushirikiano pamoja na ku-*share* kwenye *cost*, sisi tuko tayari kuhakikisha kwamba wananchi hao nao wanaondokana na usumbufu huo wa barabara kama vile Mhe. Jaku, anavyoeleza.

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, napenda nimuulize Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano, suali moja la nyongeza. Ni muda mrefu sasa ambapo hupata ahadi kuhusu kipande kidogo cha barabara ya Kangani Kukuu, kipande hicho ambacho huambiwa kila bajeti inavyofika huambiwa kitatengenezwa, lakini hadi hii leo ni bajeti ya saba hii bado kipande kile hakijatengenezwa. Je, Mhe. Naibu Waziri, huoni aibu kunidanganya mimi pamoja na wananchi wangu.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, kwa idhini yako na kwa niaba ya Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano, naomba kumjibu Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi, suali lake la nyongeza kama ifuatavyo:

Mhe. Mwenyekiti, kwanza suala hili naamini kwamba liko nje ya lile suali la msingi lililoulizwa, hili ni suala ambalo linajitosheleza, lakini kwa sababu limekuja katika mfumo wa nyongeza tutalijibu.

Mhe. Mwenyekiti, kipande anachokizungumzia Mhe. Muwakilishi, ni miongoni mwa barabara inayotoka maeneo ya Kangani kupita Tasini, na ni miongoni mwa barabara ambayo imo katika mpango wetu katika bajeti inayokuja. Nimuhakikishie Mhe. Mwakilishi, kwamba sio dhamiri ya Serikali kwamba kudanganya, ni yale yale matukio yanayotokana na uchache na upungufu wa fedha ndio inayopelekea baadhi ya miradi kushindwa kutekelezwa.

Na lengo letu na imani yetu kwamba tukipata fedha zitakazokidhi miradi yote ambayo tumeiahidi kama Serikali tutaweza kuitelekeza. Nikuombe Mhe. Mwakilishi, usiondoshe imani yako kwa Serikali bado tuna tatizo la upungufu wa fedha lakini malengo na dhamira kutaka kujenga barabara na miradi mengine yote inayoahidiwa na Serikali ipo pale pale na itafanikiwa.

Nam.130

Wafanyakazi wa Manispaa Zanzibar Wasiokuwa Waaminifu.

(Mhe. Mjumbe aliyetaka kuuliza swali hilo ameliondoa)

Nam. 88

Kukodishwa Vyumba Kwenye Wodi ya Wazazi – Mnazi Mmoja

Mhe. Farida Amour Moh'd – Aliuliza:-

Ukiachilia mbali Mapinduzi Kongwe na Mpya kuna taarifa kwamba ndani ya wodi ya wazazi katika hospitali na Mnazi Mmoja kuna baadhi ya vyumba vinakodishwa kwa wazazi pale wanapojifungua.

(a) Taarifa hizi ni kweli.

(b) Je, mapato yanayopatikana kwenye wodi hizo huingia kwenye mfuko gani.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya – Alijibu:

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mhe. Waziri wa Afya naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi suali lake Nam.88 lenye vifungu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo.

Ni kweli, katika wodi ya kujifungulia katika hospitali ya Mnazi Mmoja kuna vyumba viwili nje ya wodi mbili kuu ambavyo kila chumba kilikuwa na vitanda viwili jumla ni vinne.

Kila kitanda kilikuwa kinalipiwa shilingi elfu 3 kwa siku. Vyumba hivyo mara nyingi vilikuwa vinalipiwa na watu wanaotakiwa kufanyiwa operesheni ambazo si za dharura, pale mja mzito aliyetimia muda wake wa kuzaa na hawezi kuzaa mwenyewe kwa sababu mbalimbali inayohitaji operesheni ya lazima.

Mama huyo hupangiwa siku ya kuja na kulazwa kwa kufanyiwa operesheni. Pesa za vitanda hivyo zilikuwa zikikusanywa na Mshika Fedha aliyewekwa kwa ajili ya michango ya chumba cha upasuaji.

Mhe. Farida Amour Mohammed: Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa Mhe. Naibu Waziri, kakiri kama ni kweli vyumba vile vipo, na vyumba vile vinatumika kwa wagonjwa aidha waliokuwa wanajitayarisha kwa kujifungua au waliofanyiwa operesheni. Na kwa kuwa eneo lolote linalotengwa kwa malipo linahitaji liwe na huduma nzuri. Je, Mhe. Naibu Waziri, kwa nini eneo lile ni chafu, halisafishwi na hata yale mashuka hamna unapoingia uende ukatandike mwenyewe. Wizara yako itachukua jitihada gani ya kuwaambia watendaji waliweke katika hali nzuri eneo lile.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Kama hivyo ndivyo ilivyo kwa kweli si vizuri, hospitali si tu vyumba hivyo viwili bali hospitali nzima inatakiwa isafishwe, iwe safi, kwa sababu kama hospitali chafu hata huyo mgonjwa akienda kule hatapona kwa sababu maambukizi yatakuwa makubwa.

Kwa mantiki ya vyumba hivi, hivi sasa havipo kwa sababu hapo katikati vilileta vurugu kubwa, tumeamua kuwapa manesi na madaktari wanaokuwa katika zamu za usiku. Lakini sehemu nyengine ya hospitali nafikiri sasa hivi kama umekwenda baada ya mageuzi makubwa yaliyofanyika hospitalini uchafu haupo tena. Kikubwa kilichokuwa kinatufanya hospitali ile iwe chafu ni watu kuhamia pale, walihama makwao wakahamia pale kuja kuuguza wagonjwa, lakini tulisema yalishindikana. Kwa hiyo tukapata maamuzi kwamba tuweke ulinzi uliokuwa madhubuti na tuliweka na sasa hospitali inapendeza.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, je kama mpango unaendelea kuwachangisha wananchi kama mpaka hivi sasa upo, haoni kuwa Wizara inakwenda kinyume na maagizo ya Mhe. Dkt. Ali Mohammed Shein kwa ajili ya wananchi wake. Na pili mpaka jana jioni niko hospitali ya Mnazi Mmoja katika sehemu ya wazazi kuna dawa, nyuzi za kushonea kwa wazazi bado hospitalini hazipo, ana mpango gani wa dharura kuwa zipatikane kwa muda huu.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Mwenyekiti, nimesema hivyo vyumba sasa hivi tena havilazi wazazi, kwa hiyo nafikiri suala lake la mwanzo halina tatizo. Lakini suala kwamba labda nyuzi hakuna za kushonea wazazi, nyuzi hizi anazozisema sio za kushonea wazazi ni nyuzi ambazo zinafanyiwa operesheni kwa wagonjwa wote, na vifaa vya hospitali vinakuwepo vinakwisha, vikiwa vinakwisha ndio vimekwisha, tunajaribu kutafuta kwa wakati, tunajaribu kutuma *tendor*, lakini sasa ikiwa hazijaingia tukifika pale inabidi tuwaeleze wananchi ukweli wa mambo ili tuweze kumfanyia operesheni mgonjwa.Hatuwezi kusema kwamba hatumfanyii mgonjwa kwa sababu hakuna uzi ambao anatakiwa ashonewe kwa sababu Rais alisema na

kwa bahati mbaya na kwa saa ile uzi haupo tumuache mgonjwa tusimwambia mwananchi aende akanunue.

Mhe. Mwenyekiti, tulisema nafikiri huko kwamba kuna utaratibu umeandaliwa kwa mwaka ujao wa fedha tutakuwa tunanunua vifaa kwa ujumla kwa tenda nzima na sio taratibu ile ndogo ndogo ya kuleta vifaa vikawa vinaisha, inategemea kwamba tatizo hilo huko mbele tunaweza tukalitatua, tuombe Mungu tupate fedha.

Nam. 133

Wanafunzi Kupoteza Nuru ya Macho Zanzibar.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Aliuliza:-

Jumuiya ya wasioona Zanzibar (ZANAB) imekuwa na kilio cha muda mrefu wanafunzi wa Nyerere na Mwanakwerekwe kupoteza nuru ya macho kutokana na kuzibwa kwa madirisha ya skuli.

(a) Kwa nini Wizara ya elimu imeamua kuziba madirisha na kuwanyima mwanga wanafunzi jambo ambalo ni hatari kwa afya ya macho yao.

(b) Je ni lini Serikali itahakikisha madirisha yote yanabakia kama yalivyojengwa badala ya kuzibwa na kuathiri afya ya macho kwa wanafunzi wake.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali - Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, kwa idhini yako, naomba kumjibu Mheshimiwa Mwakilishi swali lake namba 133 lenye sehemu (a), na (b) Kwanza napenda kutoa maelezo ya utangulizi:-

Ni kweli kuwa katika baadhi ya skuli, maeneo ya madirisha ya skuli yamezibwa kwa kutumia matofali na hivyo kupunguza mwangaza katika madarasa na inaweza kusababisha athari za macho kwa walimu na wanafunzi. Skuli ya Nyerere na baadhi ya Skuli za Mwanakwerekwe C, Kijitoupele na nyengine zimezibwa madirisha hayo kwa matofali na kubakisha nafasi ndogo tu ya kutopitisha hewa kutokana na kukithiri kwa vitendo vya wapita njia kurusha mawe, vinyesi na uchafu wa aina mbali mbali kwa madhumuni ya kuwakera walimu na wanafunzi.

a) Wizara haijaamua kuyaziba madirisha ya skuli bali uamuzi wa kuziba sehemu za madirisha umepitishwa na skuli zenyewe kwa kushirikiana na kamati zao za skuli. Hata hivyo, Wizara imezitaka uongozi wa skuli kutafuta njia mbadala za kujikinga na vitendo hiyo vibaya kuliko kuziba madirisha ya skuli. Napenda kutoa wito kwa jamii na vikundi vya Polisi jamii katika maeneo ya skuli zetu kushirikiana na kamati za skuli katika kudhibiti vitendo vya hujuma zinazofanywa kwa walimu na wanafunzi kwani vinavunja moyo na vinarejesha nyuma juhudi za walimu na wanafunzi.

b) Wizara yangu itaendelea na juhudi za kuielimisha jamiii ili ielewe umuhimu wa kuzilinda na kuzihifadhi skuli zetu kwa faida ya watoto.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa ufumbuzi umepingwa na wataalamu na unaathiri nuru ya macho lini matofali hayo yataondolewa na kuwekwa nyavu zenye uwezo wa kupitisha hewa na kuzuia kitu chochote kinachorushwa, na pili Wizara inachukua hatua gani ya kudhibiti vitendo hivyo kwa wanafunzi au wanafunzi hawana haki kwa mujibu wa katiba ya Zanzibar.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti kwa idhini yako na kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali hatua zimechukuliwa kama ambavyo nilizungumza katika suala langu mama kama Wizara imeitaka uongozi wa skuli kuyatoa matofali hayo kwenye madirisha. Na mfano wa hayo nnao muhtasari wa kikao ambacho wamekaa skuli ya Nyerere na kupitisha katika bajeti zao za maendeleo ya mazingira katika mwaka huu wametenga laki nane kwa ajili ya kazi hizo. Na skuli nyengine katika vikao vyao nao watafanya hivyo hivyo kuhakikisha kama wanayatoa matofali yale na wanaweka wavu, na hii naomba niikabidhi kwako ili iwe ushahidi kwa Mhe. Jaku, na wengine waone hatua ambazo zimechukuliwa na Wizara.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa katika suali la msingi Mhe. Jaku, anaelezea habari ya uzibwaji wa madirisha, na kwa kuwa unapofunga madirisha pale ni kwamba unazuia hewa safi kuingia mle ndani, na kwa kuwa wanafunzi ni wengi kwa hiyo hewa inakuwa inakosekana sana na matokeo yake inabidi kusababisha matatizo ya kiafya kwa wanafunzi wetu jambo ambalo linaweza likapelekea tatizo hasa kwa maisha ya wanafunzi wetu. Na kwa kuwa Mhe. Naibu Waziri, amesema kwamba wamefunga madirisha kwa sababu ya kuhofia kurembewa mawe mle ndani pamoja na vinyesi, je kama mngejenga uzio katika ile skuli wangefika hawa

ambao wanarusha mawe *that is A*, na B kujenga uzio mukanusuru afya za wanafunzi na kuacha afya za wanafunzi ziathirike na hatimae kuathiri maisha yao ni ipi gharama zaidi, yaani gharama ya kuzuia kujenga uzio au kupoteza wanafunzi wetu pale gharama kubwa ni ipi zaidi.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti, kwa idhini yako na kwa niaba ya Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali naomba kumjibu Mhe. Saleh Nassor Juma wa Jimbo la Wawi suali lake la nyongeza.

Mhe. Mwenyekiti, suali lake lilikuwa ni kubwa lakini zaidi alitaka kujua kama athari kubwa ni ipi; athari kubwa Mhe. Mwenyekiti, ni kupoteza nuru ya watoto wetu au kupoteza maisha ya watoto. Lakini naomba ifahamike kama lengo la Wizara ni kuzikinga skuli zetu zote kwa kujenga ukuta, lakini Mhe. Saleh, ni shahidi wa bajeti yetu ambayo tunapitisha hapa kuna skuli nyingi ambazo zinataka kumalizwa, kuna skuli ambazo zinataka matengenezo makubwa na tujue kama tuna skuli nyingi, tuna karibu skuli 226 kwa *primary* tu, *secondary* tuna skuli karibu 189, mbali skuli 37 za *nursery*. Kwa hivyo kama Wizara tunaona athari na tunataka kama skuli zetu ziwe na uzio lakini bajeti haituruhusu Mhe. Mwenyekiti, tuna kilio cha bajeti.

UTARATIBU

Mhe. Salim Abdalla hamad: Mhe.Mwenyekiti, Mhe. Saleh Nassor Juma, Mwakilishi wa Wawi alipouliza suali, alisema ni lipi bora kuathiri afya ya wanafunzi au kujenga uzio ili wanafunzi wapate hewa safi. Sasa Mhe. Saleh, aliposema kuwa afya za wanafunzi zinaathirika sijui huku tunapokuwa wengine tunavuta hewa, tunavuta hewa safi na tunatoa hewa chafu na hewa chafu ni nzito kuliko hiyo hewa safi tunayoivuta matokeo yake huwa inakusanyika na hewa hii inaitwa *Carbondioxide.*

Kuwafungia watoto madirisha ukaacha nafasi ndogo tu unawaua kisaikolojia. Kwa hivyo, kwa kuwa suala halikujibika vizuri natoa rai yale madirisha yazibuliwe na halafu kutiwe waya ili upepo upite katika hali ya kawaida na hicho kinyesi na taka taka zisiweze kuingia.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti, nadhani nilijibu

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Mwenyekiti, naomba niulize, lile ni swali la nyongeza au ni utaratibu?

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Salim Abdalla Hamad amesema kwamba ni utaratibu, lakini hata mimi nimejiuliza. Mimi nimefikiria kwamba sio suali la nyongeza isipokuwa alikuwa anaelezea anavyofahamu yeye. Kwa hivyo, labda Mhe. Naibu Waziri wa Elimu tujue kama ataweza kulijibu au vipi, kama ataweza kulijibu basi naweza kumruhusu.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti, tusitawaliwe na jazba tuwe tunasikiliza vizuri wakati tunapotoa majibu. Kama alikuwa Mhe. Salim kanisikiliza vizuri katika majibu yangu nilijibu na nikasema kwamba nina *minutes* za vikao ambavyo Skuli ya Nyerere tayari wamekaa na nikataka ipitishwe kwa Wajumbe wote, ili kuondoa matofali yale na kutia waya.

Kwa hivyo, hilo lilikuwa tayari Mhe. Mwenyekiti, nimelieleza, lakini Mhe. Salim Abdalla bahati mbaya sana hakunisikia.

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014 – Wizara ya Katiba na Sheria

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe tumebakisha Waheshimiwa tisa ambao wameomba kuchangia katika hoja hii ya Wizara ya Katiba na Sheria. Sasa ningewaomba sana Waheshimiwa Wajumbe matarajio yetu makubwa tumalize leo hii na kama ikiwezekana tumalize mchana huu. Sasa ningewaomba sana Waheshimiwa kuangalia muda ambao wanautumia na vile vile yale ambayo yameshazungumzwa basi tusiyarejee.

Kwa hivyo, tujali muda na tuzungumze kwa *point* fupi ili tufahamike vizuri. Nawashukuru sana tunaanza.

Mhe. Hassan Hamad Omar: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwanza kabisa nimshukuru Mwenyezi Mungu (*SW*) aliyenijaalia kuwa katika hali ya uzima na afya inaniruhusu kusimama mbele ya Baraza lako tukufu.

Mhe. Mwenyekiti, napenda kuchukua fursa hii kumpongeza Mhe.Waziri wa Katiba na Sheria katika kitabu chake hiki kwa mpangilio mzuri, kimesomeka vizuri na tumekitambua. Lakini sasa kwa kujali muda wako naomba niende moja kwa moja katika mchangio wangu. Mchango wangu wa mwanzo utajikita katika Mahkama katika ukurasa wa 14 kifungu 38.

Mhe. Mwenyekiti, imeelezwa umuhimu wa chombo cha Mahkama na jukumu la kusimamia utoaji wa haki. Mheshimiwa katika chombo hiki ni muhimu sana ndani ya nchi yoyote kwa sababu chombo hiki kimepewa uwezo kikatiba kusimamia utoaji wa haki, na katika utoaji wa haki lazima kuwe na uadilifu wa kutosha, bila ya kuwa na uadilifu basi haki haipatikani. Mhe. Waziri tunamuomba sana katika kusimamia basi awashajihishe wanasheria hawa wanaotoa haki kusimamia vizuri majukumu waliyopewa. Kwa sababu watu wakishazozana mwisho kimbilio ni katika sehemu ya Mahkama ambayo ndio hatma ya mwisho katika kupata haki.

Mhe. Mwenyekiti, nikiangalia katika kiambatanisho nambari 5A kimeeleza ufunguaji wa kesi za Mahkama mwezi wa Julai/Machi 2012, mpaka 2013 kufikia kesi zisizopungua 2549 zikiwemo kesi za watoto.

Mhe. Mwenyekiti, hapa katika hoja yangu nazungumzia kuhusu kesi za watoto. Naomba Mhe. Waziri atakapokuja hapa atupe ufafanuzi kesi za watoto hizi zilikuwa zinahusiana na nini ili tupate kujua. Kwa sababu kimaumbile tunaona katika watoto ndio wanaofanyiwa unyanyasaji mkubwa, kufanyiwa vitendo visivyo halali. Watoto ndio hufanyiwa vitendo viovu ikiwemo ubakaji na mambo mengine. Kwa hivyo, Mhe. Waziri akifika hapa atueleze kesi hizi zilikuwa zinahusiana na nini na watoto ili tupate uchanganuzi zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, nikiondoka katika sehemu hiyo niende moja kwa moja katika ukurasa wa 30 Ofisi ya Mufti. Kwanza kabisa hapa nimpe pole Mzee wetu Sheikh Soraga katika ajali aliyoipata ya kumwagiwa tindi kali. Jambo hili halifurahishi na ni jambo baya sana na Mwenyezi Mungu ampe afya njema aungamane na sisi tena.

Mhe. Mwenyekiti, katika Ofisi ya Mufti imetajwa ndani ya kitabu hiki kama jambo kubwa ni kusimamia katika migogoro. Lakini Mheshimiwa tujiulize leo Mhe. Waziri anasimama hapa kutuomba pesa aidhinishiwe kwa ajili ya Ofisi ya Mufti ambayo inasimamia migogoro. Sasa jambo la kujiuliza, hebu tuangalie siku hadi siku migogoro hii si inazidi? Kwa sababu tukiangalia Ofisi ya Mufti inasimamia migogoro ya Kiislamu hapa Zanzibar, lakini siku hadi siku inakuwa migogoro inazidi.

Mhe. Mwenyekiti, Mwezi wa Ramadhani *Inshaallah* umetufikia na hapa ndipo penye migogoro mikubwa ikifika Mwezi wa Ramadhani hatuelewani. Kuna watu wanatangulia kufunga na wengine wanatangulia kufungua. Kwa hivyo, ofisi hii inafanya kazi gani kutowaweka Waislamu pamoja. Mhe. Waziri utakapokuja hapa utueleze bayana tumeangalia siku hadi siku migogoro inazidi misikitini, madarasani na sehemu nyenginezo za mambo ya

kidini na ofisi hii ipo, sasa atueleze kazi zale ni zipi? Kwa sababu sisi tumeidhinisha fungu hapa katika kufanikisha mambo hayo lakini bado ni matatizo makubwa sana.

Vile vile mgogoro mwengine ni kuandama kwa mwezi. Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyozungumza kuwa mwezi wa Ramadhani tayari na hapa hutokea migogoro ya kuandama kwa mwezi si aghalabu sana kupata muafaka tukawa kitu kimoja Waislamu. Wale wanaotangulia kufunga kama nilivyoelezea na wengine wanachelewa, wengine wanafungua siku ya Ramadhani wengine wanaendelea. Hili ni tatizo. Mhe. Waziri, akiwa msimamizi mkuu wa jambo hili tunataka aje atupe maelezo ya ziada na wapi wamefikia katika hatua hizi.

Mhe. Mwenyekiti, haitoshi katika Ofisi hii ya Mufti kwa sababu ofisi hii inasimamia migogoro ya Waislamu tuna Masheikh wetu wale wamewekwa ndani. Na masheikh katika nchi ni watu wa kushajihisha katika mambo ya amani, lakini utaangalia utasema sasa ofisi hii inafanya kazi gani katika kuwasaidia na wao kama Waislamu katika Mwezi huu Mtukufu wa Ramadhani watakuwa na madrasa, sasa sijui yeye atasimamia vipi katika kuwasaidia.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea katika mchango wangu niende katika Ofisi ya Vizazi na Vifo katika ukurasa wa 36 kifungu cha 101. Mheshimiwa kifungu hiki naomba ninukuu.

Kifungu cha 101 kinasema kwamba:

> "Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka 2012/2013 imesajili jumla ya vizazi 31,540 wakiwemo wanaume 15,930 na wanawake 15,610 Unguja na Pemba. Vile vile afisi hii imesajili vifo 1885 vikiwemo vya wanaume 1,072 na wanawake 813 Unguja na Pemba".

Mimi niseme tu nimpongeze Waziri kwa hatua hii iliyofikia ni nzuri, lakini pamoja na uzuri hakukosi kasoro. Mheshimiwa katika ofisi hii kumekuwa na kero kubwa sana ya upatikanaji wa vyeti vya kuzaliwa. Mhe. Waziri ni shahidi baada ya kuteuliwa kwake aliahidi kama baada ya wiki mbili mtoto kuzaliwa atapata cheti cha kuzaliwa na hatokifuata tena Unguja kwa ahadi aliyoitoa kule Pemba. Lakini limekuwa ni jambo zito halina ufumbuzi, imekuwa kikwazo kikubwa mtu anatimiza miaka mitatu bado cheti cha kuzaliwa hajakipata hili ni tatizo. Mhe. Waziri tumuombe asifumbie macho akija hapa atupe maelezo ya ziada, watu wanazaliwa siku hadi siku na wanakufa lakini vyeti vya kuzaliwa ni tatizo.

Ukiangalia katika vyeti vya kuzaliwa umuhimu wake kama huna pamoja na sifa zilizotajwa katika kupata kitambulisho cha Mzanzibari Mkaazi basi sifa

kubwa ni hiki cheti cha kuzaliwa, mtu awe na sifa mbili zile awe na umri wa miaka 18, awe mkaazi wa maeneo, lakini kama hana cheti cha kuzaliwa bado imekuwa ni kazi kubwa. Kwa hivyo, Mheshimiwa watu wanakosa haki zao za msingi kwa sababu ya cheti cha kuzaliwa, hivyo tunaomba hapo akija atupe maelezo ya ziada vipi vyeti vitapatikana kama ilivyo nchi zetu nyengine.

Mhe. Mwenyekiti, nije katika Rasimu ya Katiba ambayo itakuwa ni mchango wangu wa mwisho kwa leo. Mheshimiwa Rasimu ya Katiba imeshaletwa na hata Waheshimiwa Wawakilishi na Wajumbe wengine wote wameshapata. Kazi kubwa mimi natanabahi ni kuwa makini na rasimu hii. Rasimu hii kuna mambo mengine ni mazuri lakini mambo mengine hayajakidhi haja, kama Wazanzibari tunatakiwa kitu kimoja kilio hiki ni cha muda mrefu na nichukue nafasi hii kumpongeza Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano kwa kujaalia kuweza kutupa fursa hii.

Sasa watu wengine ukizungumzia Muungano wanakuona adui na Muungano ndio mama wa kuzungumzia *source* ya mambo yote ya aina ile. Sasa bila ya kuzungumzia Muungano hayo mengine yatapatikana wapi? Hizi kero zote ni za Muungano lakini kwa kuwa tumeungana. Kwa maana hiyo mtu akizungumzia Muungano asionekane adui lazima tuujadili Muungano wetu uko vipi, bila ya kujadili uwe vipi hatutafikia tunakotaka kufika.

Hii rasimu imependekeza serikali tatu, serikali tatu sawa lakini itakuwaje? Wenzetu wa Tanganyika mpaka leo hawajapata jila la kuita, Tanganyika kwa sababu hawaitaki kuirejesha, sisi tunajivunia Zanzibar kwa sababu ni nchi mbili huru zilizoungana tumejivunia na tunajilaki kwamba Zanzibar, lakini wao ukitaja Tanganyika hawaitaki sasa tunaelekea huko na kama tunaelekea huko watafute jina mapema ya kuipata hiyo serikali nyengine ambayo ni ya Bara. Hata waite Mwalimu Nyerere lakini tukifika huko wawe wameshapata jina lao, sisi tunajinadi Zanzibar na ni nchi mbili huru zilizoungana ndio tukapata Tanzania. Lakini sasa tuko katika mchakato wa rasimu ya katiba.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nawaomba Waheshimiwa kuwaelimisha wananchi wetu na tunakoelekea, tunayo nafasi hii adhimu tukiikosa hapa ndio tutafika miaka 50 zaidi sisi hatupo tena ulimwenguni.

Mhe. Mwenyekiti, kwa haya machache katika mchango wangu naomba nikae kitako na Mhe. Waziri ataponipa maelezo ambayo yatanifurahisha *Inshaallah* nitampitishia hoja yake. Ahsante sana.

Mhe. Omar Ali Shehe: Mhe. Mwenyekiti, nashukuru kunipa nafasi hii mchangiaji wa pili kwa siku ya leo ili na mimi angalau niweze kuchangia ofisi hii muhimu. Mhe. Mwenyekiti, naomba nianze kwa kumpongeza Mhe. Waziri

pamoja na watendaji wake wote wa wizara kwa namna anavyosimamia na kutekeleza majukumu yake ya kikazi siku hadi siku.

Mhe. Mwenyekiti, Wizara hii ya Katiba na Sheria ni wizara muhimu sana, ni wizara muhimu kwa kuwa moja kati ya muhimili wetu imo kwenye wizara hii, lakini vile vile katika wizara hii tuna Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, tunayo Ofisi ya Mwendesha Mashtaka katika wizara hii, tunayo Tume ya Kurekebisha Sheria, tuna Ofisi ya Mufti, tuna Wakala Usajili wa Biashara na Mali, tuna Ofisi ya Mrajis wa Vizazi na Vifo, tuna Ofisi ya Msajili wa Haki Miliki, kuna Ofisi ya Wakfu. Kwa ufupi wizara hii Mhe. Mwenyekiti, ni wizara inayosimamia haki za wananchi, inayosimamia haki za raia wa nchi, lakini vile vile wizara hii imebeba jukumu kwamba ni wizara inayosimamia mambo ya kiroho, lakini tusisahau kwamba ofisi hii inajumuisha hata sehemu ya uchumi. Kwa sababu kuna taasisi ambazo zinasimamia sehemu ya uchumi wa nchi yetu.

Kwa hivyo, mimi niungane tu na wale wote waliokubali kwamba wizara hii ni wizara nyeti na katika kuizungumza kwake lazima Wajumbe tuwe makini sana ili tuifanyie haki katika utendaji wake.

Naomba nianze Mhe. Mwenyekiti, na Mahkama Kuu. Kama nilivyoeleza kwamba Mahkama yetu kwa mujibu wa katiba yetu ndio taasisi iliyopewa mamlaka ya kutoa haki na ni moja kati ya mihimili mitatu ya dola, ambapo tuna serikali, Baraza la Wawakilishi na Mahkama. Kwa msingi huo basi, kwa sababu ni taasisi moja muhimu sana ni taasisi ambayo inatakiwa iwe kimbilio la wananchi.

Kwa vyovyote vile serikali inatakiwa iandae mazingira maalum ya kuiwezesha Mahkama kutoa haki. Mahkama haiwezi kutoa haki kama haijaandaliwa mazingira ya kutoa haki, kama ilivyo mihimili mengine ya dola Mhe. Mwenyekiti, tumekuwa tukipigania kwamba mihimili mitatu ya dola iwe ni huru na ijitegemee hasa katika upande wa bajeti.

Mhe. Mwenyekiti, tumekuwa tukipiga kelele kuhusu Baraza la Wawakilishi tumepewa ahadi kwamba mambo yako mbioni na muda mfupi tutapata haki hiyo ya Baraza kumiliki uwezo wake wa kibajeti. Lakini naomba hapa nisisitize kwamba Mhe. Waziri azingatie hilo, kwamba kama vile tunavyopigania Baraza lipewe haki ya kumiliki bajeti yake ndivyo hivyo na Mahkama inavyotakiwa iwe na uwezo wa kumiliki bajeti yake. Sasa naomba nimuulize Mhe. Waziri atakapokuja, jee amefikia hatua gani katika kuifanya Mahkama ijitegemee kibajeti?

Kwa sababu Mhe. Mwenyekiti, hatuwezi tukawa na Mahkama ambazo ndio zenye tegemeo la kutoa haki za wananchi kama hazina uwezo. Kwa sababu tunalalamika na ndivyo ilivyo, katika Baraza hili tumekuwa tukishuhudia mara nyingi sana sasa hivi Baraza hili linataka kugeuzwa kuwa ndio sehemu ya Mahkama kitu ambacho ni *wrong*. Wananchi wanafanya hivyo kwa sababu wamekatishwa tamaa na vitendo vinavyotokea katika Mahkama. Kwa hivyo, msingi wake hasa ni kwamba uwezo wa Mahkama katika kujisimamia wenyewe, katika kuwawezesha Mahakimu na Majaji unakuwa ni mdogo. Kwa hiyo, rai yangu katika hili naomba serikali Mhe. Waziri atakapokuja aje anieleze ni hatua gani aliyofikia.

Mhe. Mwenyekiti, katika Mahkama naomba pia nizungumzie suala la kutenda haki. Nasisitiza sana kwa sababu wenzangu walisema na mimi naomba nirudie kwa umuhimu wake kwamba imeonekana sasa hivi Mahkama zetu zina matatizo si vizuri kuzisema Mahkama lakini sasa inabidi tuziseme. Na hili naomba serikali au Mhe. Waziri atakapokuja hapa aje aniambie je, wameweza kufanya utafiti kuona tatizo hasa hili linalofanya Mahkama zilalamikiwe ni tatizo gani. Je, wamewahi kufanya utafiti wa kujua kwamba matatizo yalioko kule kama yanavyosemewa kwamba ni tatizo la rushwa au ni tatizo la ukosefu wa maadili. Kwa sababu wakati mwengine unaweza ukasema kwamba matatizo ya rushwa yanasababishwa na kipato kidogo cha Mahakimu na Majaji na watu wengine, unaweza ukasema hivyo na ina-*sound* kusema hivyo.

Lakini wakati mwengine unaweza ukamuwezesha mtu katika kiwango hicho cha kumridhisha lakini bado akaendelea na vitendo vyake, maana yake hapo sasa si tatizo la uwezo ni tatizo la kukosa maadili. Mhe. Waziri je, wizara yake imefanya utafiti na kujua tatizo hasa linalokumba Mahkama hii katika upande huu ni tatizo gani? Kwa sababu tusiangalie kwamba ni uwezo tu lakini vile vile na tatizo la mahakimu wetu, kama ikiwa tunachukua tu Majaji waliokuwa hawana maadili mazuri hatuwezi tukafika pahala. Sasa naomba Mhe. Waziri atakapokuja aje anieleze jee, kuna utafiti wowote uliofanywa unaopelekea tatizo hili kuzidi, vitendo hivi vya rushwa katika Mahkama zetu?

Mhe. Mwenyekiti, katika hali hiyo hiyo naomba Mahkama kwa kweli ifanye haki kwa watuhumiwa, kwa sababu zi vizuri sheria zipo nchi hii inaongozwa na sheria, na si vizuri kwa kweli kufika pahala sheria tukazipa mgongo tukaendeshwa na vitu vingine. Sasa hivi inaonekana kwamba sheria zetu takriban tunazipa mgongo na kuendeshwa na vitu vyengine.

Dhamana ni haki ya mtuhumiwa. Sasa tunapofika pahala kwa kweli mtuhumiwa hapewi dhamana kama sheria zinavyoelekeza hilo ni tatizo, kuna watu sasa hivi wako ndani kwa kipindi kirefu sana Mheshimiwa lazima

tuzungumze vitu kama hivi. Watu wanawekwa ndani bila ya kupewa dhamana hatutaki tuingilie uhuru wa Mahkama ni kosa kabisa, lakini hapa ndipo pahala ambapo ni penye kuzungumza matatizo ya wananchi.

Kuna watu ambao wamewekwa kizuizini muda mrefu hawapewi dhamana, hawahukumiwi wakajulikana tatizo ni nini. Mimi ninachosema Mhe. Mwenyekiti, kwa nini watu ambao wanawekwa ndani kipindi kirefu hawapewi dhamana kwa tatizo gani na tunavyojua kwa mujibu wa sheria zetu dhamana ni haki ya mtuhumiwa yeyote, tunajua sipendi niseme nani lakini wako watu kwa kipindi kirefu wako ndani hawapewi dhamana kwa nini Mhe. Waziri, atakapokuja hapa naomba atueleze katika hilo.

Mhe. Mwenyekiti, tuna tatizo vile vile katika maamuzi. Imejitokeza kwamba hata pale Mahkama zinapotoa maamuzi kunakuwa na tatizo kubwa la utekelezaji wa maamuzi ya Mahkama, hili ni tatizo kubwa, sasa tatizo liko wapi? Mahkama tayari ishatoa *ruling* kwamba hiki iwe ni hivi na hivi lakini kinyume chake hakuna utekelezaji. Hebu Mhe. Waziri atakapokuja hapa atupe darsa tatizo liko wapi? Tatizo ni kwamba wale watu huwa hatujui utaratibu wa kuifanya hukumu ile itekelezeke au tatizo linakuwaje? Au ni nini nafasi ya Mahkama baada ya kutoa *ruling* kuona kwamba maamuzi yake yanatekelezwa tatizo liko wapi? Mhe. Waziri atakapokuja hapa hebu atuelekeze kidogo tufanye nini na kesi hizi hasa ziko kwa upande wa serikali, kwamba pale serikali inapotolewa maamuzi jambo linalohusu serikali mara nyingi tumekuwa tukishuhudia na ripoti zetu zinakuja hapa, hasa kwa upande wa serikali tatizo linakuweko wapi? Maamuzi hasa yenye kuipa haki serikali hayatekelezwi. Kwa ufupi ni hivyo. Kwa hivyo naomba Waziri atakapokuja tuelezwe ile *procedure* inayotumika katika kutekeleza maamuzi ya Mahkama.

Ilikuja kesi hapa mwaka jana au mwaka juzi Mahkama tayari ishaamua kwamba kuna wavuvi fulani wapewe haki zao kesi ikaja Barazani hapa kwamba maamuzi ya Mahkama hayatekelezwi. Kuna mashirika kadhaa huko huamua vya kuamua Mahkama ikaamua lakini katika utekelezaji wa maamuzi ya Mahkama hakuna.

Mhe. Mwenyekiti, naomba nizungumzie maslahi, kunakuwa na maslahi duni sana kwa hasa Mahkama za Mwanzo. Hii katika ngazi za Mahkama kuna Mahkama ya Mwanzo. Mahkama ya Wilaya, Mahkama ya Mkoa na kuendelea. Lakini kuna tofauti kubwa sana ya maslahi baina ya Mahakimu katika Mahkama za Mwanzo na ile ngazi ya wilaya, kwa sababu ukitoka kwenye Mahkama ya Mwanzo ngazi ya pili ni wilaya, lakini tofauti yao ni kubwa sana. Sasa kwa nini kuwe na tofauti kiasi hichi na kazi wanayofanya ni kazi moja?

Mhe. Mwenyekiti, maana yake wakati mwengine kesi inatoka Mahkama ya mwanzo inakatiwa rufaa katika ngazi ya wilaya, kesi ni ile ile, maamuzi ni yale yale na hasa hawa Mahakimu wa mwanzo ndio wakati mwengine wanakuwa na kazi sana, hawa ngazi ya wilaya wakati mwengine hawana kesi kama haijaanzia katika ngazi ya mwanzo. Sasa naomba Mhe. Waziri atueleze ni sababu gani inayopelekea ngazi ya mwanzo maslahi yakapishana baina ya ngazi ya mwanzo na ngazi ya wilaya. Je, umechukua hatua gani katika kulirekebisha hilo?

Mhe. Mwenyekiti, katika upande huo huo wa Mahkama naomba nizungumze nafasi ya Jaji Mkuu. Jana Misri kule kulipita mapinduzi, Rais kapinduliwa na Jaji Mkuu wa Misri kawa ndiye Kaimu Rais. Nilikuwa nalieleza hilo kumpa nafasi Jaji Mkuu kwamba Jaji Mkuu ni mtu mkubwa sana katika nchi hii, lakini Jaji Mkuu wetu utamuona ni mtu wa kawaida tu, ndivyo mwenyewe alivyo kwa sababu Jaji wetu mkuu hapendi kujikweza na ndio utamaduni wake na ndio sifa yake hapendi kujikweza. Lakini sisi hatuchukui Jaji Mkuu kama ni mtu, Jaji Mkuu ni taasisi ambayo inapaswa kupewa heshima. Hebu Mhe. Waziri atapokuja atueleze Jaji wetu huyu mbona yuko katika hali ya kawaida tunamhitaji kumuona Jaji Mkuu ni kiongozi mkubwa sana katika nchi. Viongozi wa nchi hii ni Mhe. Rais, Spika pamoja na Jaji Mkuu, tunahitaji tumuone naye maslahi yake yakiimarishwa hasa katika masuala ya ulinzi na vitu vingine.

Lakini la mwisho katika Mahkama naomba nikuulize Mhe. Waziri. Nakumbuka kulifanyika kikao katika nchi za Maziwa Makuu na kikao kile waziri binafsi alihudhuria, na kikao kile kilitoa azimio kwamba nchi zote wanachama zianzishe Mahkama maalum katika kuharakisha kesi za udhalilishwaji. Azimio hilo lilitoka sasa ni kazi ya wanachama kutekeleza agizo hilo. Sasa Mhe. Waziri naomba atakapokuja atwambie utekelezaji wa azimio lile la nchi za Maziwa Makuu limefikia hatua gani kwa upande wetu Zanzibar? Na atwambie basi ni kesi ngapi ambazo za udhalilishwaji zimefika kwa mwaka huu, na ni hukumu ngapi ambazo zimetolewa kwa mnasaba wa kujibu suala hili.

Mhe. Mwenyekiti, niende kwenye Ofisi ya *DPP*. Ofisi ile ni muhimu sana pamoja na ofisi ya Mwanasheria Mkuu. Wanasheria wote hawa wanafanya kazi kubwa sana, na ofisi ile ndio takriban kipindi cha nyuma kila wizara ilikuwa ikisimamia kesi wenyewe, lakini sasa serikali inaanzisha utaratibu kwamba kesi zote za serikali wanasheria au mawakili watoke katika ofisi ya *DPP*. Hapo kama walivyoeleza wenzangu naomba niungane na mkono wa wenzangu kwamba kuna tofauti kubwa sana ya maslahi baina ya wanasheria ambao wote ni wanasheria *by profession* na ni kazi moja. Na nataka niseme kwamba mchakato hasa wa kesi unaanza katika Ofisi ya Mwendesha

Mashtaka, utakapoi-*disturb* ofisi ya Mwendesha Mashtaka Mhe. Mwenyekiti, ni kwamba hakuna kesi itakayosimama.

Tumekuwa tukishuhudia mara nyingi sana hasa kesi zinazohusu upande wa serikali, mara nyingi sana kesi zinazohusu serikali zinashindwa Makamani, huwa tunajiuliza tatizo ni nini? Mimi binafsi inanipitikia kwamba ni udhaifu wa wanasheria wetu walio katika ofisi ya Mwendesha Mashtaka, na ni udhaifu si kwamba hawana uwezo aa! Ni udhaifu kwa sababu inaonekana maslahi yao ni duni hawana uwezo wa kuweza kusimamia kesi hizi, ndio maana basi serikali mara kwa mara hushindwa katika kesi zake Mahkamani.

Kwa hivyo, Mhe. Waziri atakapokuja atueleze, hivi kuna utaratibu gani aliouandaa kuhakikisha kwamba maslahi ya wanasheria wetu walioko katika ofisi ile ya Mwendesha Mashtaka yanaimarishwa angalau kulingana na wenzao kule wanaosimamia kutoa haki Mahkamani. Hili ni tatizo kweli kweli katika hilo.

Mhe. Mwenyekiti, inavyoonekana hasa wakati mwengine watu wanafika pahala hivi ni tatizo la kuweko Ibrahim tu pale? Maana yake hata ule mtiririko wa upelekwaji wa fedha unakuwa sasa hivi ni tatizo katika ofisi hiyo ya Mwendesha Mashtaka. Sasa pamoja na hii naomba Mhe. Waziri atakapokuja atuelezee namna alivyojipanga kuhakikisha kwamba anaiwezesha kikamilifu pamoja na kuimarisha maslahi ya wanasheria wetu walioko katika Ofisi ya *DPP*, kwa sababu maslahi yanapishana sana baina ya wao, Majaji na Mahakimu wengine.

Mhe. Mwenyekiti, naomba sasa niingie katika Ofisi ya Vizazi na Vifo. Naomba tukubaliane kwamba suala la muamko wa kuwa na vyeti vya kuzaliwa ni vyema tukakubaliana kwamba umekuja katika miaka ya karibuni, baada ya kuwepo hili suala la Zan ID. Takriban kabla ya hapo wazazi wengi walikuwa hawana muamko wa kusajili vizazi pamoja na vifo. Sasa kama hivyo ndivyo basi Mhe. Mwenyekiti, limejitokeza hapa tatizo kwamba kuna udhibiti mbovu sana wa utoaji wa vyeti. Wenzangu walieleza na mimi naomba nigusie, tuna udhibiti mbovu. Mhe. Waziri sehemu hii ni muhimu kwa sababu suala la kumsajili kuwa ndiye raia au kuwa ni mkaazi au vyovyote utakavyoita ni suala muhimu. Kuna malalamiko kwamba kuna watu wengi sana sio raia na bado wanapata vyeti hivi, maana yake ukimpa mtu cheti maana yake tayari umempa uraia huyo. Vile vile kuna tatizo kwa upande wa pili kuna watu ambao wanastahiki kupewa vyeti hawapewi.

Sasa Mhe. Waziri kwa unyenyekevu mkubwa naomba utakapokuja uje utueleze ni namna gani wizara au ofisi yako imejiandaa katika suala zima la udhibiti wa vyeti, hasa tukichukulia kwamba wizarani pale Ofisi ya Msajili

inaonekana kwamba pale huwa kuna sehemu ya usajili, lakini vyeti hasa vinapatikana katika ngazi ya mawilayani huko. Kwa hivyo, Mhe. Waziri utakapokuja hebu tueleze unatumia *mechanism* gani katika kuhakikisha kwamba kunakuwa na udhibiti wa utolewaji wa vyeti katika mawilaya, kwa sababu ninachoelewa mimi cheti ni gamba tu, unaweza ukachukua gamba ukaenda ukalitolesha pale *Press* ya serikali halafu Mkuu wa Wilaya akafika akatia saini, bila ya ofisi yako kuwa na taarifa.

Kwa hivyo, Mhe. Waziri utakapokuja utueleze ni namna gani umejipanga katika hilo? Lakini

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, naomba kidogo ukae kidogo kisha utaendelea baadae. Waheshimiwa Wajumbe, naomba tuutambue ugeni uliopo hapo juu ya ukumbi wetu ambaye ni Balozi wa Netherlands, *Ambassador of the Kingdom of Netherlands* nchini Tanzania *(Makofi).*

His Excellency Dr. Adriaan Koekkoek. I hope I pronounced it well. Ni mgeni wa Mhe. Spika, na amekuja kumuaga rasmi baada ya kumaliza muda wake wa kazi hapa nchini. *His Excellency you are warmly welcome, thank you!*

Mhe. Mjumbe, endelea.

Mhe. Omar Ali Shehe: Mhe. Mwenyekiti, kwa hivyo naomba Mhe. Waziri atakapokuja hapa aje aniridhishe kuwa anatumia utaratibu gani au ni utaratibu gani aliouandaa au ni utaratibu gani atakaouandaa, ili kuhakikisha kwamba kuna udhibiti makini katika utoaji holela wa vyeti hasa vyeti hivi ambavyo tunasema kwamba ni muhimu sana kuwe na udhibitiwa kutosha.

Vile vile katika suala hili la vyeti Mhe. Mwenyekiti, tumekuwa tukilalamika kwa niaba ya wananchi wetu, hasa wale ambao wanafanya *late registration. Late registration* gharama yake ni kubwa sana, kwa mtu mnyonge kutoa shilingi 35000 kufanya *late registration* ni tatizo. Hii ni haki ya kila mwananchi, usiifanye haki ile sasa kununuliwa ikawa ghali Mhe. Waziri, pamoja na kwamba unahitaji pesa, kwa sababu wewe hili ni fungu ambalo unaingiza serikalini, lakini sasa usifanye kuwa huu ni mtaji wa kukupatia pesa, suala la haki za watu usilifanye kuwa ni mtaji wako. Hasa watu wa Finya huko wa Jimbo lako wengi hawana vyeti, kwa hivyo wafanyie takhfifu watu hawa pamoja na kwamba umewekewa *amount* ya kuchangia serikalini, lakini tunaiomba serikali iende sehemu nyengine ikatafute mapato na wasitegemee tu mapato kutoka katika kuwapatia watu haki zao hasa haki za kiraia katika nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, ofisi ya Mufti inafanya kazi nzuri na mimi naomba kwanza nimpe pole Katibu wa Mufti Sheikh Soraga na tunamuombea kwa Mwenyezi Mungu amponyeshe haraka na yeye apate nafuu kuungana na waislamu wenzake katika kazi nzuri anazofanya. Baada ya kumtakia dua Sheikh wetu naomba nipongeze kazi nzuri Ofisi ya Mufti inayofanya ya kiroho, lakini katika hili naomba niulize kwamba tunavyo vyuo vya Qur-an na kwa nchi yetu Qur-an ni elimu ya msingi, kwa sababu watoto wetu wote takriban kabla ya kuanza ile elimu ya kawaida ya ki-*secular* wanakwenda katika elimu hii ya Qur-an na mtoto unapomsomesha Qur-an, wataalamu wanasema anakuwa na maarifa mazuri zaidi.

Sasa Mhe. Waziri naomba nikuulize hivi serikali pamoja na wizara yako inaratibu vipi elimu inayotolewa katika madrasa zetu hizi. Kwa sababu vile inavyotakiwa hasa iingie katika mtaala wa kawaida ni lazima tufike pahala vyuo vya Qur-an hivi tuvirasimishe, sasa viwe ni elimu rasmi. Je, wizara yako imejipanga vipi au ina utaratibu gani wa kuona kwamba idadi ya vyuo tulivyonavyo au aina ya walimu. Kwa sababu mara nyingi kesi hutokea kwamba sijui mwalimu wa chuo kambaka mwanafunzi na kadhalika. Sasa huo sio utamaduni wala sio utaratibu. Kwa hivyo, hata walimu nao wanaofundisha katika madrasa na vyuo vyetu wanakuwaje na serikali inaratibu vipi hasa suala zima la hivi vyuo vyetu vya Qur-an.

Mhe. Mwenyekiti, sio kuratibu tu, lakini ni pamoja na kuratibu katika kuvisaidia. Maana yake sasa hivi wale walimu takriban wanahitaji msaada, tufike pahala tufikirie namna ya kuvisaidia hasa walimu wa Qur-an, serikali ifike pahala ivitambue na baadae iwasaidie. Katika suala la Ofisi ya Mufti Mhe. Mwenyekiti, kumekuwa na malalamiko sana, hasa Ofisi ya Pemba kwamba utekelezaji wa bajeti inakuwa ni mdogo sana na unakwenda kwa kusuasua. Ninachotaka kukuambia ni kwamba wafanyakazi wa ofisi yako sasa hivi wana madeni, hata ile kuwaambia watoke Pemba kuja Unguja kwa ajili ya kazi takriban wengi sana wanadai katika ofisi yako hawalipwi, wanatoa pesa zao mfukoni kwa ajili ya kuja huku Unguja kwa shughuli za kikazi, sasa inakuwaje utekelezaji wa bajeti hasa ofisi yako ya Pemba uwe katika hali ya kusuasua je, kuna tatizo gani? Naomba Mhe. Waziri utakapokuja hapa unifafanulie katika hilo.

Lakini la mwisho kabisa naomba niingie kwenye rasimu ya kawaida kwa ufupi sana niseme, kwamba Mhe. Mwenyekiti Wazanzibari tunahitaji Muungano, na sidhani kama kuna Mzanzibari ambaye hautaki Muungano, tunauhitaji Muungano, lakini tunauhitaji Muungano wa serikali mbili. Kwa sababu jana yuko mmoja alizungumza kwamba tuna Muungano wa serikali moja, hapana Muungano ni wa serikali mbili Serikali ya Tanganyika na Serikali ya Zanzibar ndivyo tulivyoungana.

Kwa hivyo, tunahitaji Muungano ambao utalinda maslahi ya pande zote mbili, huu ndio Muungano ambao tunauhitaji. Tunahitaji Muungano ambao utajenga heshima kwa nchi zote mbili zilizoungana na utalinda maslahi kwa nchi zote mbili zilizoungana na utajenga nidhamu kwa nchi zote mbili Mhe. Mwenyekiti, zilizoungana. Sasa huo ndio Muungano ambao tunauhitaji.

Mhe. Mwenyekiti, naomba nimalizie kwa kuulizia kuwa serikali imekuwa ikisema kwamba haina msimamo katika suala zima la mchakato huu wa katiba. Serikali mara nyingi imekuwa ikisema kwamba haina msimamo na msimamo wake unategemeana na msimamo wa wananchi, hiyo ndio kauli ya serikali. Msimamo wa serikali utategemea msimamo wa wananchi wa Zanzibar watakavyoamua.

Swali langu Mhe. Waziri ni kwamba hivi serikali inaratibu vipi msimamo wa wananchi, kwa sababu msimamo wa wananchi unatokea katika hatua tatu. Hatua ya kwanza ni yale maoni yaliyokusanywa; hiyo ni hatua ya kwanza, ambapo wananchi walionesha hisia zao na matakwa yao kwa Muungano.

Lakini hatua ya pili itaingia katika mabaraza ya katiba, pale ni pahala ambapo vile vile tutapata kuona msimamo wa wananchi na hatua ya tatu itatoka kwa Wajumbe wanaotoka Zanzibar katika Bunge la Katiba. Kwa hivyo, maoni ya Wazanzibari yatapatikana katika hatua tatu. Hatua ya kwanza ni hatua ya maoni ambayo tayari yameshatolewa, hatua ya pili ni mabaraza ya katiba ambayo tukijaaliwa karibuni tutaingia, na hatua ya tatu ni Bunge la Katiba ambapo Wazanzibari nao kwa kupitia taasisi zao wataingia katika Bunge la Katiba.

Kwa hivyo, naomba Mhe. Waziri utakapokuja uje kunifafanulia, ni vipi serikali itaratibu maoni haya? Kwa sababu msimamo wa serikali ni kwamba utategemeana na maoni ya wananchi au matakwa ya wananchi. Sasa je serikali inatumia *mechanism* gani, au serikali inatumia utaratibu gani wa kuratibu haya maoni katika hatua hizi tatu ili hatimaye mwisho wa siku Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ije itoe msimamo wake kwa niaba ya Wazanzibari. Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa fursa hii na mwanzo kabla ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu aliyeniwezesha kusimama hapa, huu sio uwezo wangu na wala sio matakwa yangu ni uwezo wake mwenyewe *Allah Subhanahu Wataallah* na kunipa pumzi hizi kuweza kupumua.

Mhe. Mwenyekiti, nimshukuru Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria pamoja na watendaji wake wote kwa hotuba hii waliyotuletea. Pongezi maalum na za

dhati kabisa zimfikie Mhe. Jaji Mkuu Al Hajji Omar Othman Makungu kwa mabadiliko makubwa aliyoyaonesha katika Jengo la Mahakama Kuu ya Zanzibar, kufuatilia matengenezo makubwa. Hivi sasa jengo hilo linaonekana lenye sura nzuri na la kisasa na Waheshimiwa Wajumbe nakunasihini sana baadhi ya wakati tutembelee mahakama ya Vuga. Huwezi kuamini hivi sasa kama kweli ni ile mahakama, kuna viyoyozi ndani mule hatari!

Pili niwapongeze Majaji wetu kwenda Pemba kwa wakati muafaka wa kusikiliza kesi. Ni jambo la kupigiwa mfano na niwapongeze sana, ni tofauti na huko nyuma ilivyokua. Kilio changu Mhe. Mwenyekiti, ambacho nitakuwa mkali kidogo ni kuhusu Mahakama ya Rufaa ya Tanzania, imefika wakati ratiba ya vikao vya kesi viangaliwe upya.

Mhe. Mwenyekiti, naongea jambo hili kwa masikitiko makubwa sana, kwa sababu Mahakama ya Rufaa Tanzania inakutana mwaka mara moja. Sasa kama mtu yupo mahabusu rufaa yake kafungua bila ya hati ya dharura. Mfano kafungua mwezi Mei mpaka aje asikilizwe mwezi Disemba, huu sio utaratibu mzuri, inafika wakati mtu anateseka. Utamkuta mtu keshatumia miaka miwili ndani au miezi sita halafu hukumu yake ni miezi mitatu, hapa atakuwa keshajihukumu mara tatu au mara nne. Kwa hapa nitahitaji maelezo Mhe. Waziri.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu ukurasa wa 16. Kwa hapa Mhe. Mwenyekiti, naomba uniruhusu kidogo ninukuu, ulizungumzia kuhusu kesi 2,897 zimetolewa uamuzi katika kesi 8,913 na kesi 6,039 ndio zilizofunguliwa mwaka 2012/2013 na kesi zilizosajiliwa ni 2,874 idadi ambayo ni ndogo. Katika suala la usikilizaji kesi kuchelewa basi umefika wakati tuwalete wataalamu waje watusaidie ni nini tatizo la kuchelewa kwa kesi kutolewa maamuzi. Kesi zilizofunguliwa adhabu zake zimekuwa zikiwatesa wananchi wakati mwengine.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo nikiendelea na mchango wangu nije kwenye kesi ya Msikiti wa Mtume Muhammad *Swalallahu Alayhiwasalam* iliyokuwa Mwanakwerekwe. Kesi hiyo nambari 66 ya mwaka 2002. Mhe. Mwenyekiti, kesi hiyo ilikuwa ni baina ya Mwinshehe Abdalla Mwinshehe na Katibu Mkuu wa Bilal Muslim Mission.

Mhe. Mwenyekiti, naomba unisikilize kwa makini sana. Kesi hii imetolewa maamuzi kwenye Mahamaka Kuu na baadae Mahakama ya Rufaa Tanzania. Lakini cha kushangaza na kusikitisha ikiwa mahakama haifuatwi sasa atafuatwa nani nchi hii? Je, huu ndio utawala bora kweli tunaokwenda nao. Msikiti umeshatolewa huku wenyewe wapewe, leo Msikiti wavuta unga wameshaanza kuuvuruga wote, huyu kakosa na huyu kakosa.

Mhe. Mwenyekiti, hapa utanisamehe sana. Tunaambiwa jambo likiwa ovu utumie mkono wako, mdomo wako na mwisho uchukie. Kwa hapa nitahitaji maelezo ikiwa Mahakama ya Rufaa Tanzania imeshaleta maelezo kuwa watu hawa wapewe haki yao, basi mpala leo Msikiti huu hawajapewa ni nini tatizo. Tunakwenda mbele au tunarudi nyuma.

Nikiondoka hapo Mhe. Mwenyekiti, nilimsifu sana Mhe. Jaji Mkuu kuhusu mahakama alivyoifanya, lakini cha kushangaza hivi sasa lile jengo limesimama muda mrefu, kuna miti pale inakera wananchi kupita katika njia ile sijui chanzo ni nini. Nitahitaji maelezo kuhusu jengo lile, sijui kama pesa hakuna au vipi ni muda mrefu sana mpaka muda huu.

Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa nikipiga kelele sana kuhusu tarehe ya Kiislamu, imepigwa danadana huu mwaka wa tatu, hakuna jawabu nililopata. Nilileta swali hapa mpaka kwenye *order paper* likatiwa, lakini kwa masikitiko makubwa sana na unyonge wa hali ya chini kabisa likazungushwa hivi hakuna jawabu lililokwenda. Hiki ni chombo cha wananchi sio chombo cha Mhe. Hija Hassan hiki, wananchi ndio wanatutuma kuja kuwasemea kama kuna tatizo basi serikali itoe kauli. Hii Waheshimiwa ni dhamana kwa wananchi mbele ya Mwenyezi Mungu tutakwenda kuulizwa, sisi tunatumwa na wananchi. Kama serikali inaona hili suala ni zito basi itueleze ni nini tatizo Lake, asilimia 99 hapa ni waislamu, kama sheria hairuhusu basi nijibiwe ili wananchi wasikie. Suala hili nimelipigia kelele kwa muda mrefu tokea kuingia Barazani humu.

Mhe. Mwenyekiti, Abubakar kwanza alikubali liko kwa Mhe. Makamu wa Pili wa Rais na kwa Mhe. Makamu wa Pili wa Rais sijui limelala limepata kitanda au ndio linatengenezwa. Kuna kesi hivi juzi imetolewa suluhisho mahakamani, baada ya suluhu kufanywa nje inafanywa mahakamani. Kuna mtu na mkewe wakagawana watoto, wakaambiwa mtoto mmoja chukua wewe na mmoja abaki. Mtoto wa miaka mitatu huyu baba atamlea vipi? Suluhu badala ya kufanywa nje watu wamegombana mimi na Mhe. Hija Hassan twende mahakamani tushakubaliana, basi suluhu inafanywa mahakamani, sijui ndio utawala bora huu?

Mhe. Mwenyekiti, wenzangu wamechangia sana hapa Mhe. Mtando, Mhe. Omar Ali Shehe kuhusu kitengo cha Ma-*DPP*. Wale jamaa ni kioo cha hii nchi, sio mara ya kwanza au ya pili kuzungumza suala hili, jamani wafikirieni ni binadamu wale, imeshafika muda wale kazi wanayofanya wanahitaji kuangaliwa. Mhe. Mwenyekiti, umesema suala likishazungumzwa lisirudiwe tena, lakini natia msisitizo tu.

Mhe. Mwenyekiti, nije katika Mahakama ya Manispaa ya Zanzibar. Mahakama ile sijui kama ipo kwa kisheria na kwa mujibu wa kanuni za nchi hii, mahakama ile imekuwa haitendi haki kwa wakati huo sijui hivi sasa. Mimi mwenyewe kabla sijawa Mheshimiwa yameshanikuta mambo nikiyazungumza hapa wengi mtashangaa. Ni watoto wa mjini sisi, huu uheshimiwa kesho haupo, walikuwepo wangapi humu. Alikuwepo Mwakilishi wa Jimbo la Muyuni kakaa miaka 15 kaondoka nimekuja mimi na atakuja mwengine.

Mhe. Mwenyekiti, mahakama ile haitendi haki huo ndio ukweli ulivyo. Mimi nilishtakiwa binafsi yangu nikataka kutia wakili, nikaambiwa huna ruhusa ya kutia wakili pale kwenye mahakama ile. Sasa haki hiyo itapatikana wapi. Mhe. Abubakar Khamis Waziri utakapokuja hapa utueleze mahakama ilivyo kisheria na taratibu gani zinafuatwa? Na kwa nini mtu asitie wakili kutetewa mule?

Mhe. Waziri nikuombe sana kwa heshima na taadhima, wanyama sasa hivi wamekuwa wakipata shida wanabebeshwa mizigo mizito, naomba utuletee sheria nyengine hapa punda wamekuwa wakiteswa sana, ng'ombe anabebeshwa mizigo kwenda hawezi.

La mwisho kabisa kwa kumalizia nimuombe Mhe. Waziri huu mwezi Mtukufu wa Ramadhani keshokutwa unakaribia panapo uhai Je, serikali itatoa kauli gani kuhusu mahoteli yatakayokuwa wazi na watu wanaovaa nguo fupi. Kwa hayo machache Mhe. Mwenyekiti, mimi sitounga mkono hii hoja mpaka nitakapopata maelezo kamili. Ahsante.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote hatuna budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kutufikisha mpaka leo tukiwa hai na kutupa afya na uzima wa kuingia humu Barazani na pengine baadae kwenda kuswali swala ya Ijumaa.

Baada ya dibaji hiyo, naomba nikushukuru wewe kwa kunipatia nafasi ya kutoa mawazo yangu kuhusiana na hoja iliopo mbele yetu. Mhe. Mwenyekiti, hoja iliopo mbele yetu ni Hotuba ya Waziri wa Katiba na Sheria. Hii katiba na sheria kabla sijaingia ndani ningeomba nizungumze kidogo kuhusiana na katiba kama utangulizi wa mchango wangu.

Mhe. Mwenyekiti, katiba ni mkataba baina ya watawala na watawaliwa. Kwa mtazamo huo Mhe. Mwenyekiti, katiba inatakiwa itoke katika mishipa ya watawaliwa, katika *veins* ya wale wanaotawaliwa ndio katiba inatakiwa itoke. Mhe. Mwenyekiti, la kusikitisha sana ni kwamba tangu uhuru wa nchi hii

mpaka leo hakujawa na katiba iliyotokana na wananchi. Hatuna katiba iliyotokana na wananchi, tena katiba zote mbili.

Kwa mfano, katiba ile ya Jamhuri ya Muungano ilikuwa ni katiba ya Tanganyika tu, ambapo mwaka 1977 Mhe. Julius Kambarage Nyerere na chama chake cha Mapinduzi waliweza kuitisha Bunge la Katiba, ambalo uwakilishi wa Zanzibar haukuwa mzuri, kwa sababu haukuangalia vigezo. Kwa hivyo, maslahi ya Zanzibar katika katiba hii ya Jamhuri ya Muungano hayakutunzwa sana, kwa sababu watu waliopelekwa pale ni akina Shaybu Tifu kutoka Mkanyageni, mtu ambaye ukimuuliza jina lake lazima apate jirani yake pale amuulize jina yule anaitwa nani, alishiriki katika Bunge lile la katiba. Kule kusini aliondoka mzee wangu Kassim Hana na yeye ni halikadhalika, kwa vile ndani ya katiba hii maslahi ya Zanzibar hayakutungwa.

Kwa hivyo na hii katiba ya Jamhuri ya Zanzibar vile vile kwa kweli na sisi hatujawa na katiba iliyotokana na sisi wakaamua tangu Mapinduzi mwaka 1964 mpaka leo hatujapata katiba inayotokana na sisi. Kwa sababu hii katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 ilikuwa ni *two men show*. Mwaka 1984 walikutana mzee Aboud Jumbe Mwinyi na Mhe. Abubakar Khamis Bakary akiwa ni *draft man* akakaa pale Ikulu akaandika ndio ikapatikana hii. Hii kwa kweli haina *legitimacy* na kwa mnasaba huo Mhe. Mwenyekiti na sisi Wazanzibari tunahitaji katiba ambayo inatokana na sisi. Hii katiba ni ya bwana Abubakar Khamis Bakary na bwana Aboud Jumbe Mwinyi. Kwa hivyo, nataka hasa katiba iundwe na sisi.

Baada ya dibaji hiyo nichukue fursa hii Mhe. Mwenyekiti, kumpongeza Mhe. Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano Mhe. Jakaya Mrisho Kikwete, pamoja na Serikali ya Jamhuri ya Muungano kwa kuweza kutuletea mchakato wa kupata katiba mpya. Nimpongeze katika hili kwa sababu mchakato huu ni kwamba katiba itatokana na sisi. Nashukuru kwamba Mhe. Abubakar katika kipengele cha rasimu anasema kuwa makini katika kuona kuwa inasomwa rasimu ili katiba inayokuja ilinde maslahi ya Wazanzibari na nchi nzima. Kwa hivyo, napenda nimpongeze Mhe. Abubakar.

Mhe. Mwenyekiti, kuna matatizo kidogo kwenye suala zima la hii rasimu, matatizo yaliyojitokeza katika rasimu hii Mhe. Mwenyekiti, kwanza mipaka ya nchi hizi mbili haikuwa *identified*. Hii rasimu bado ina matatizo na umakini mkubwa unahitaji kwa Wazanzibari kuona kuwa hatuna sisi tena kwa ndugu zetu wa damu.

Kwa mfano, hii katiba kongwe. Naomba Mhe. Mwenyekiti, uniruhusu ninukuu; eneo la Jamhuri ya Muungano ibara ya 2 kifungu kidogo cha

kwanza cha Katiba hii ya Jamhuri ya Muungano, inasema "eneo la Jamhuri ya Muungano" Kwa mujibu wa sheria nambari 15 ibara ya 6 hii sheria ya mwaka 1984 inasema;

Sheria nambari 15 ibara ya 6 inasema;

"Eneo la Jamhuri ya Muungano ni eneo lote la Tanzania Bara na eneo lote la Tanzania Zanzibar na ni pamoja na sehemu yake ya bahari ambayo Tanzania inapakana nayo".

Mhe. Mwenyekiti, ndio nikasema kwamba hii rasimu ika-*identify* maeneo, lakini nilipoangalia hapa katika rasimu hii tuliyoletewa, eneo la Jamhuri ya Muungano ndio eneo lote la Tanzania Bara, ikijumuisha sehemu yake ya bahari na eneo lote la Zanzibar ikijumuisha sehemu yake ya bahari. Sasa hii rasimu hapa haifai tunataka tujue mipaka ya Zanzibar. Ndio juzi namshukuru Mhe. Mwanasheria Mkuu wa Serikali akasema sijui kisiwa cha Fungu Mbaraka ni chetu. Tatizo halikuwa *identified* na haya maeneo. Sasa Mhe. Mwenyekiti, Watanzania wakiwemo Wazanzibari katika hili tuwe makini sana.

Mhe. Mwenyekiti, katika rasimu hii ili maslahi ya Zanzibar yaimarike basi lazima kuwe na *sovereignty*. Moyo wa nchi ni ile dola. Rasimu inasema kuwe na serikali tatu. Serikali ya Tanzania Bara na Serikali ya Zanzibar pamoja na hiyo ya Muungano. Hii ya Tanzania Bara na hii ya Zanzibar si *sovereignty states*, s*overeignty* itapatikana kwa Jamhuri, jambo ambalo ni tatizo.

Mhe. Mwenyekiti, hii nchi haikupatikana hivi hivi tu. Hii nchi kwa kweli ilipatikana katika mashaka makubwa na katika kipindi chote hicho sisi tunapapatua ili kuona hii nchi inapata thamani. Lakini sasa tayari wakati wake umefika, kwa sababu tunaingia katika mchakato huu wa katiba mpya ili kuinusuru Zanzibar na kuifanya iwe na mamlaka yake. Sasa katika hili naomba Waheshimiwa yaani Muungano uendelee kuwepo, lakini vile vile Zanzibar iwe na mamlaka yake kamili, sio katika kupangiwa tu.

Unauona ujanja wa hii rasimu Mhe. Mwenyekiti, inasema kwamba *foreign affairs* ni *issue* ya Muungano, lakini *international relations* kila mtu anakuwa na yake, sasa hii ni kutudanganya. Mimi sio mgomvi katika mambo ya *International relations* pamoja na diplomasia. Lakini huwezi kuwaambia Wazanzibari kwamba mambo ya nje yatakuwa ni ya Jamhuri, lakini uhusiano wa kimataifa kila mtu atakuwa na yake. Huku ni kutudanganya.

Mhe. Mwenyekiti, tunataka Zanzibar iwe inaweza kujiamulia mambo yake na iwe inaweza kujiunga na taasisi zozote za kimataifa. Kuna taasisi huwezi kujiunga ikiwa hamna *sovereignty state*, hata hapo FIFA hatuwezi kujiunga.

Leo mnatudanganya kwamba munaweza kujiunga. Mashirika mengine ni lazima nchi iwe ni *sovereignty state* na taasisi nyengine za kimataifa ni lazima nchi iwe ni *sovereignty state.* Kwa hivyo, nadhani hii katiba ni lazima Waheshimiwa tuwe makini sana katika kuona kuwa maslahi ya Zanzibar tunayalinda na isiwe kama vile Kassim Hana na Shaybu Tifu walivyofanya mwaka 1977 ndio ikazua mgogoro huu ambao mpaka sasa hivi tunao.

Mhe. Mwenyekiti, jengine ni kuhusu sarafu. Mimi sitaki T.*Shilling* iondoke hata siku moja. Lakini haitakuwa dhambi kwa Zanzibar tukawa na sarafu yetu. Kuna Euro na Waingereza wana pauni. Ilimradi sarafu yetu haitokera Muungano. Kwa hivyo, mimi nadhani suala la sarafu kila mtu awe na yake. Kwa hivyo, hapa kwetu pakiwa na hiyo Zenji dola au pakiwa na Zenji *shilling*. Sisi tutakuwa na fedha zetu na wao watakuwa na zao na hii T. *shilling* itatumika hapa na tukaenda kule Bara tutatumia, japokuwa hii yetu sisi isitumike kule, lakini tutatumia T. *shilling* haikeri Waheshimiwa musiwe na wasi wasi katika hili.

Mhe. Mwenyekiti, sasa niende katika suala la Mahakama. Mhe. Mwenyekiti, kama kuna taasisi ambayo inatakiwa iwe makini ni mahakama, huu ni muhimili wa dola miongoni mwa mihimili mitatu. La kusikitisha Mhe. Mwenyekiti, mahakama zetu zina tatizo na wanaonekana hawa watendaji *executive*, wao wako *more superior* ukilinganisha na hii mihimili mingine iliyobakia, ni tatizo! Mhe. Omar Ali Shehe kasema pale kwamba Jaji Mkuu kule Misri, baada ya Mapinduzi ndio wana shida ya nchi sasa hivi. *Interm President* ni Jaji Mkuu. Sasa hapa Tanzania tukiiangalia mahakama ina matatizo na mahakama inadharaulika sana, lazima ichukue *status* yake mahakama Mhe. Mwenyekiti.

Kwanza tuangalie *status* za hawa Mahakimu hususan Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo Mhe. Mwenyekiti wanadhalilika kimaslahi, kwamba hakimu anapewa si zaidi ya shilingi 350,000/=, yaani Hakimu wa Mahakama ya Mwanzo hazidi hapo akiajiriwa, sasa hakimu huyu atafanya kazi vipi na sisi hatutaki rushwa, yaani muna-*create* mazingira ya hawa wachukue rushwa.

Kwa kweli Mhe. Mwenyekiti, Mahakimu wa Mahakama ya Mwanzo wanataka waangaliwe sana na hawa ni wanyonge mno, kwa sababu inasikitisha kuona kwamba Hakimu wa Mahakama ya Mwanzo hawezi hata kununua kipando, maslahi madogo ni tatizo. Kwa hivyo, tunahitaji kufanya *reform* ya Mahakama.

Mhe. Mwenyekiti, ukiachilia mbali hawa mahakimu na kwanza nataka niipongeze serikali kwa kupandisha viwango vya Mahakimu wa Mkoa na

Mahakama Kuu na hapa naipongeza serikali lakini hawa Mahakama ya Mwanzo wanadhalilika tuwasaidieni jamani.

Hata hivyo, kipengele chengine ambacho mahakama inadhalilika sana Mhe. Mwenyekiti ni kwenye majengo. Mhe. Mwenyekiti, Hakimu anatakiwa awe *very comfortable* akikaa anataka kuhukumu basi awe ametulia *physically and mentally* ndio atapata kuchunga ile haki.

Kwa kweli inasikitisha Mhe. Mwenyekiti, kwamba mahakama zetu zote na ile Mahakama ya Mkoa pale Chake Chake ukienda kuiangalia, basi hakimu awe makini kweli, kwa sababu kuna feni linatoa sauti vibaya na huku anataka kutoa hukumu na huku zogo la feni ni tatizo, na pale afadhali lakini tukiangalia majengo ya Mahakama ya Mfenesini ni *worst*, je unafikiri hakimu atakuwa *comfortable* kusikiliza kesi na baadaye kutoa hukumu vizuri.

Vile vile jengo la Mwanakwerekwe ni baya sana, pia Mahakama ya Makunduchi kama miezi miwili nyuma nilitembelea pale hata umeme hakuna. Kwa hivyo, hakimu anataka kutoa hukumu wakati jasho linamtoka na hali hiyo ni tatizo. Mhe. Mwenyekiti, namuomba Mhe. Waziri wakati atakapokuja kufanya majumuisho anieleze katika kipengele cha mahakama ni lini ataweza kuboresha hizi mahakama zetu ambazo kwa kweli majengo yake ni mabaya, sambamba na suala zima la kuwapatia mafao hawa Mahakimu wetu wa Mahakama ya Mwanzo.

Tume ya Kurekebisha Sheria; na hii imezungumzwa sana katika ukurasa wa 22 mpaka 25. Mhe. Mwenyekiti, sheria za nchi yetu zinatakiwa ziende sambamba na mazingira, yaani zi-*adopt* sheria *according to environment*, kwa sababu sheria ikiwa haiendi sambamba na mazingira ni tatizo, pia sheria ikiwa haiendi sambamba na katiba ya nchi ni tatizo.

Mhe. Mwenyekiti, tukiangalia kwenye ibara ya 21(2) na (3) cha Katiba ya Zanzibar, Mhe. Mwenyekiti naomba uniruhusu ninukuu.

> Katiba ya Zanzibar kifungu cha 21(2) na (3) vinaeleza hivi:-
>
> (21) “Uhuru wa kushiriki shughuli za umma, haki ya kufanya kazi na kupata ujira.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, unazo dakika tano.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Mwenyekiti, ahsante. Tukiangalia vipengele hivi vya Katiba Mhe. Mwenyekiti, naomba kunukuu.

(2) Kila Mzanzibari anayo haki na uhuru wa kushiriki kwa ukamilifu katika kufikia uamuzi juu ya mambo yanayomhusu maisha yeye maisha yake au yanayolihusu taifa.

(3) Kila Mzanzibari anayo haki ya kufanya kazi na anastahili fursa na haki sawa, kwa masharti ya usawa wa kushika nafasi yoyote ya kazi na shughuli yoyote iliyoko chini ya Mamlaka ya Zanzibar".

Mhe. Mwenyekiti, ukiviangalia vipengele hivi ni kwamba vinatoa nafasi kwa kila mzanzibari kushiriki au kuweza kushiriki katika kila nafasi. Lakini inasikitisha kwamba sheria zetu tunazozitunga hivi sasa haziendi sambamba na mazingira tu, kwa kiasi fulani hazikidhi kuipa nguvu katiba yetu. Kwa mfano, hivi sasa watu wenye ulemavu wanayo haki ya kupata ajira, pia waweze kushiriki katika mambo mbali mbali. Jambo la kusikitisha ni kwamba hivi sasa kupata *information* ni tatizo na hasa wenye ulemavu wa macho au masikio ni tatizo.

Kutokana na hali hiyo, naomba sheria za nchi sasa zilingane na hawa. Kwa mfano, chombo cha habari kinapotaka kujisajili lazima masharti yake kama vile Gazeti letu la Zanzibar Leo waweze kutoa angalau nakala moja au mbili za *Braille*, ili na hawa wenye ulemavu wa uoni waweze kupata kupapasa na kujisomea taarifa.

Jengine Mhe. Spika, hivi sasa kuna haja ya kukazia kuwa na Sheria ya Mavazi hapa Zanzibar, kama tunavyofahamu ongezeko la UKIMWI ni kubwa na wala hakuna sheria kama hiyo, kwa sababu mavazi kwa kiasi fulani yanachangia ingawa Mhe. waziri wa Katiba na Sheria ni mkaidi katika hili. Lakini mavazi yanachangia katika suala la ongezeko la UKIMWI. Kwa hivyo, kuwe na sheria ya kudhibiti mavazi.

Halikadhalika naomba nimalizie kwa suala zima la Ofisi ya Mkurugenzi wa Mahakama (*DPP*). Mhe. Mwenyekiti, Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka ndio yenye kuangalia mashtaka, yaani mwenendo wa kesi katika mahakama zetu, ili haki itendeke pale basi inayo nafasi kubwa ofisi hii. Jambo la kusikitisha Mhe. Mwenyekiti, kwa kiasi kikubwa sana inachelewesha watu kupata haki zao pale mahakamani.

Kwa mfano, inachelewesha kwa msingi kwamba inaweza ikaenda kesi pale ikakaa mwaka mzima wanafanya utafiti tu au uchunguzi na huku watu wakisota rumande au jela. Kwa kweli inasikitisha kwamba Sheikh Farid hapa na ukimsema watu wanakuona mbaya, lakini ni mzanzibari pamoja na

wenzake, na hivi sasa karibu mwaka wao wako jela na watoto wao wanahangaika na hili ni tatizo, Mhe. Spika dhamana ni haki ya mshtakiwa.

Kwa hiyo, kumnyanyasa Sheikh Farid Hadi, Sheikh Mselem Ali na wenzao kule ni tatizo na tukisema tunaambiwa wengine ni Uamsho, lakini wale ni wazanzibari na sisi hatuzungumzi kama Uamsho, kwa nini Sheikh aliyekamatwa juzi tu Dar-es-Salaam kwa kesi hizi hizi Sheikh Issa Ponda amepewa dhamana, sasa iweje Sheikh Farid Hadi na wenzake.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, muda umekwisha.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Mwenyekiti, naomba nimalizie kwa kumtaka Mhe. Waziri wakati atakapokuja hapa kufanya majumuisho, basi anieleze ni sababu gani iliyokwamisha akina Sheikh Farid na wenzao kupewa dhamana hadi leo hii? *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, nakuombeni sana tujali muda, kwa sababu wachangiaji bado ni wengi na pia tunataka kumaliza leo wizara hii. Kwa hivyo, nakuombeni sana tuheshimu muda na wala sitaki kusomewa kanuni Waheshimiwa Wajumbe. Kwa maana hiyo, tujaribu kujipanga vizuri, najua tunaweza basi tutaweza kuwamaliza wote, laa si hivyo itabidi wengi waje wachangie kwa maandishi. Tunaendelea na Mhe. Subeit Khamis Faki anayefuata Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi na baadaye Mhe. Hija Hassan Hija.

Waheshimiwa Wajumbe, samahani ni Mhe. Rufai Said Rufai ndiye ambaye amejitayarisha badala ya Mhe. Subeit Khamis Faki. *(Makofi)*

Mhe. Rufai Said Rufai: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana nadhani mambo ni makubwa na moyo ndio hivyo tena. Awali ya yote tumshukuru *Subhanahu Wataala* kunijaalia na mimi mchana huu kupata nafasi ya kuweza kutoa mchango wangu juu ya hotuba ya Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria iliyowasilishwa hapa Barazani jana.

Mhe. Mwenyekiti, mimi sitakuwa na marefu kama gunia, isipokuwa nitajitahidi kujali muda wako, ili niweze kutoa mchango wangu.

Nianze mchango wangu kwenye ukurasa wa 30 kifungu cha 83 kuhusu Ofisi ya Mufti Zanzibar. Mhe. Mwenyekiti, kama sikosei leo tuko mwezi 25 Shaabani na mbele yetu tumeelekewa na mwezi Mtukufu wa Ramadhani. Kwa kweli kila inapofika mwezi Mtukufu wa Ramadhani kuandama kwake na kila inapofika mwezi wa Shaabani hapa huwa tuna mivutano kwa waislamu na kila mmoja ana ufahamu wake.

Jambo hili limekuwa ni tatizo kwa Wazanzibari ambao ni Waislamu, na suala hili ni la muda mrefu sana tokea watu wanakamatwa wanazuiwa kusali au kufunga, lakini mpaka ikafika wakati ikaonekana wenye kufunga au kufungua mwanzo waachiwe.

Mhe. Mwenyekiti, mwezi unapoandama tayari kuna kundi wenye itikadi yao, kwamba ni popote pale utakapoonekana mwezi Mtukufu wa Ramadhani basi wako tayari kufunga mwezi huo. Vile vile kuna kundi itikadi yao mpaka uonekane katika anga hii ya Afrika ya Mashariki wao ndio wanaweza kufunga. Kwa hivyo, suala hilo lipo hapa Zanzibar na linakuwa sasa ni kubwa na watu wanavutana katika maeneo tofauti hasa maeneo yale ya shamba.

Kutokana na hali hiyo, naiomba sana Ofisi ya Mufti Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu hali ya sasa Zanzibar tumeingiwa na wingi wa vyombo vya habari. Kwa mfano, kuna vyombo vinafuata muandamo wa Zanzibar, yaani Afrika Mashariki hapa vyengine vinafuata muandamo popote mwezi Mtukufu utakapoonekana. Kwa hivyo, wanaopata tabu ni Waislamu walioko vijijini, ambapo wengi wao redio ya Zanzibar haiwafikii na hawaipati, kwamba watapata mawasiliano kupitia kule, sasa watu wanakuwa wanatatizika katika hali hii.

Mhe. Mwenyekiti, naiomba sana Ofisi ya Mufti kushirikiana na hivi vyombo vya habari, ili kuweza watu kupata taarifa katika vyombo hivi vyote ambavyo tunavyo hapa Zanzibar.

Suala moja tu Mhe. Mwenyekiti ni muhimu kwamba watoe maelezo pale ambapo umeonekana mwezi kwa wale wanaofuata popote duniani utakapoonekana na wale wanaofuata katika eneo la Afrika Mashariki itakapoonekana, kwamba leo mwezi umeonekana kwa wale wanaofuata muandamo wa mwezi popote duniani, ili wananchi wanapopata taarifa kwa yule ambaye lazima uonekana Afrika ya Mashariki, basi atajua kwamba aa leo sio upande wangu.

Vile vile kwa yule atayesikia mwezi umeonekana Afrika Mashariki umeonekana basi atajua kwamba tayari kufunga, ili kuwaondoshea matatizo wananchi wetu hasa wa vijijini ambapo vyombo vya habari ni vichache kwao.

Lakini mimi sipendelei kuona kwamba kuna mivutano na kulazimishana kwamba lazima mwezi uonekane Afrika ya Mashariki hapa ndio afunge au yule anayesema kwamba popote duniani utakapoonekana duniani afunge tukawa tuna mivutano. Kwa kweli dini hii Mhe. Mwenyekiti si dini ya

mivutano, kwa sababu tumeshaambiwa *dini ni nasaha*, basi ni vyema tunasihiyane katika mambo yote yanayohusu mambo ya dini.

Mhe. Mwenyekiti, ninaishauri sana Ofisi hii ya Mufti iwaelimishe wananchi katika kupitia vyombo vya habari walivyonavyo, ili waweze kutoa taarifa hii kwamba mwezi huu leo umeonekana kwa kimataifa na leo umeonekana kwa Afrika ya Mashariki.

Sasa watu katika misimamo yao, basi waweze kusimama na kuendeleza funga zao kwa mwezi Mtukufu wa Ramadhani, na pale utakapoandama wa Mfungo Mosi pia taarifa kama hizi ziweze kutumika, ili kila mtu katika ile imani yake, basi aweze kusimama na imani yake kwa ajili ya kutekeleza wajibu ambao ameuona unafaa kwake.

Katika Ofisi hii ya Mufti nitoe shukurani zangu za dhati kabisa katika kuwapa taaluma wafanyakazi wake wote kwa suala zima la ugonjwa wa UKIMWI hasa kwa kupitia utaratibu wa mafunzo ya dini ya Kiislamu. Mhe. Mwenyekiti, namshukuru sana Mhe. Mufti pamoja na uongozi wake kwa kuliimarisha hili kwa wafanyakazi wake wote.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, nadhani Mhe. Mufti asibakie na ofisi yake tu katika kutoa taaluma hii, kwa sababu Zanzibar tunaambiwa asilimia 99 ni waislamu, ambao wanayo haki ya kufuata miongozo ya kitabu chao pamoja na Mtume wao, hivyo waislamu wanaijali sana Ofisi ya Mufti.

Kwa hivyo, masuala haya kama tayari ameshatoa taaluma kwa ofisi yake, basi ni vyema sasa wafanyakazi wake wakateremsha taaluma hiyo ya UKIMWI katika Mafunzo ya Kiislamu chini kuna waislamu wenyewe, ili na wao waislamu waweze kufuata muongozo wa Uislamu kama vile unavyoelekeza, kwa ajili ya kulipunguza hili janga la UKIMWI.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli janga la UKIMWI kama kweli ofisi hii itasimamia vizuri, basi ni vyema suala moja kubwa kabisa kulikemea ni suala la mavazi. Suala hili la mavazi hivi sasa hapa Zanzibar hajulikani nani muislamu na yupi si muislamu, yaani kila mmoja ana mitindo tofauti ya kujionesha aonekane amevaa vizuri au amevaa vibaya.

Kwa hivyo, kama hii ofisi itafanya kazi, na itakuja chini kwa waislamu wenyewe na kuwapa taaluma hii ya kidini, basi nadhani hii asilimia 1.0 tuliyonayo hapa Zanzibar kama itasimamia vizuri ofisi hii, basi inaweza ikapungua na isipige tena hatua kwenda mbele, ili wananchi wetu wakaepukana na janga hili baya la UKIMWI.

Vile vile ofisi hii inashughulikia masuala ya madrasa na vyuo vya *qur-an*. Lakini tukiangalia takwimu ofisi imepitia katika madrasa na vyuo ni ndogo sana, yaani haijafanya wajibu wake wa kuzitambua madrasa zetu zilizopo hapa Zanzibar.

Kutokana na hali hiyo, naomba kuishauri sana ofisi suala hili ikalipa kipaumbele la kuzitembelea vyuo vya *qur-an* na madrasa, ili kuhakikisha watu hawa wa Ofisi ya Mufti wanakwenda katika maeneo husika.

Mhe. Mwenyekiti, kama watafanya kazi hii hizi taarifa zinazotoka hapa kwamba kuna baadhi ya walimu na mimi nasema sio wote, kwa sababu mtu mbaya ni mbaya tu hata awe sheikh au nani, kama anao ubaya wake basi huo utakuwa ni ubaya wake binafsi.

Kwa maana hiyo, suala la mtu lisichukuliwe kwamba ni walimu wote wa madrasa wenye matatizo haya ya kuharibu wanafunzi wao, isipokuwa ni baadhi ya watu ambao wenye tabia kama hiyo na pengine ni za kimaumbile, lakini anayo taaluma na sisi tunaijali taaluma yake ni muhimu kwa vijana wetu na wala hatuipendi tabia yake. *(Makofi)*

Kwa hivyo, watu wenye tabia hizi mbaya tunawaomba sana waache tabia hizi, ili wawe wanachokifundisha ni masuala mazima ya kumjua Mwenyezi Mungu na Mtume wetu. Mhe. Mwenyekiti, ni vyema wasivunje hadhi za walimu wengine kutokana na tabia zao mbaya. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, Ofisi ya Mufti isimamie matatizo haya, ili kuondosha hatari ya vijana wetu ambao hivi sasa uhuru umekuwa mkubwa, vyombo vya habari, utandawazi umekuwa mkubwa, kwa hiyo ni rahisi kabisa vijana kuvutika na mambo hayo. Kwa hiyo, ninaiomba ofisi kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti, kwamba isimamie hili la kupitia vyuo tulivyo navyo hapa Zanzibar.

Hata hivyo, Mhe. Mwenyekiti suala la posho kwa walimu wa madrasa ni muhimu. Kwa maana hiyo, tutoke pale tunaposema tunayo elimu ya dunia na akhera, sasa huyu mwenye kufundisha elimu ya akhera basi anahitaji mambo mengi hapa duniani. Kwa mfano, kwanza anahitaji usafi wa nguo zake na kiwiliwili chake, maisha kuweza kuishi hapa pamoja na mambo mengine mbali mbali.

Sasa ikawa elimu ya akhera hatuijali na zaidi tunaijali elimu ya dunia, basi tujue duniani tupo, lakini tuhakikishe kwamba tutaondoka na kama ni kuondoka pia utakwenda kuulizwa hii elimu ya akhera uliipa hatua gani wewe mpaka umeweza kuwaelimisha watu wakaijali akhera zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, tulijibu swali hili hapa duniani kabla hatujaenda huko akhera. Jambo la msingi walimu hawa tuwajali kama tunavyozijali taasisi nyengine za serikali, ili na wao waweze kuwafundisha wanafunzi wetu vizuri na waweze kuyamudu maisha yao, kwa sababu madrasa zetu nyingi hasa za vijijini ni watu maskini sana wazee wa watoto hao wanaofundishwa.

Kwa hivyo, kuna madrasa mzee anatakiwa apeleke shilingi 100 kwa wiki, ambayo hivi sasa shilingi 100 maslahi yake ni madogo sana, basi na hiyo pia inakuwa haipatikani kwa walimu wetu, angalau kupata sabuni na mambo mengine. Lakini hapa lazima Ofisi ya Mufti namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti, kwamba aboreshe hali hizi za madrasa ili angalau posho na wala sisemi mshahara, basi kuwe na posho fulani la kujaaliwa walimu wetu wa madrasa. *(Makofi)*

Nikiendelea na mchango wangu sasa naomba niende kwenye mahakama. Mhe. Mwenyekiti, katika suala zima la mahakama niseme kwamba hii nchi imejengeka kwa mihimili mitatu mikuu na sisi tunajidai kwa hilo.

Vile vile kuna vyombo vyengine vinaomba navyo viwe kama muhimili ndugu zetu wa habari kutokana na hali yao ya kuimarisha mambo ya habari na wao wanaomba hilo uwe ni muhimili wa nne, lakini hivi sasa tuseme tunayo mihimili mitatu. Lakini Mhe. Mwenyekiti, tatizo ninaloliona katika mihimili hii mitatu muhimili wa dola ndio unajaliwa zaidi kuliko mihimili hii miwili mingine.

Mhe. Mwenyekiti, tunaye Jaji Mkuu ambaye anasimamia muhimili mzima huu wa mahakama na tunamfahamu ni mzee wetu na aliwahi kuwa Mwanasheria Mkuu katika Baraza hili la kipindi cha mwaka 2010 mpaka 2015 wakati wa mwanzo. Lakini Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli serikali haijamuweka pahala la kumtunza Jaji Mkuu inasikitisha sana.

Mhe. Mwenyekiti, Jaji Mkuu anaishi kijijini kama ninavyoishi mimi. Tukiangalia suala la miundombinu ya maeneo anayoishi hayafai na kama itanyesha mvua basi Mhe. Jaji Mkuu anashindwa kuingia nyumbani mwake kutokana na tope na maji yanayotuwama katika hilo eneo analoishi. Kwa kweli hii ni aibu mtu kama yule akae maeneo ambayo hayaridhishi, mimi nadhani muhimili huu hatuupi haki yake.

Katika hili Mhe. Mwenyekiti, nataka nikupe hadithi moja tu.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, nenda kwenye *point* acha hadithi na muda uliobakia ni dakika tano tu!

Mhe. Rufai Said Rufai: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana. Wawakilishi walioanza katika serikali hii miaka ya 1980 mpaka 1984 wakati wa Rais Mstaafu wa Zanzibar Mzee Aboud Jumbe Mwinyi kuna Mwakilishi mmoja alitakiwa akamuwakilishe Rais wa Zanzibar hapo Tanzania Bara, yaani Rais alitakiwa aende kule lakini kwa bahati mbaya kutokana na dharura za Rais, basi alimtuma Mwakilishi wake aende akamuwakilishe.

Mhe. Mwenyekiti sote tunafahamu Wawakilishi wetu tuliokuwa nao wakati huo tunalingana na wengine tuliopo hivi sasa basi Mheshimiwa yule akachukua ile nafasi akaenda kumuwakilisha Rais. Kwa kweli heshima aliyoipata basi ni sawa kama alikuwepo yule Rais mwenyewe tena ni Mwakilishi wa kawaida. *(Makofi)*

Lakini leo tunaye Jaji Mkuu ambaye ni mwenye muhimili mmoja wa dola hana matunzo masikini. Sasa tusimchukulie mtu alivyo, isipokuwa tuichukulie sheria inavyomueleza kama inavyomueleza Rais au Spika pamoja na Jaji Mkuu basi apewe zile haki zake.

Kwa mfano, leo hii Mhe. Mwenyekiti Chukwani bado tunayo matatizo ya umeme pamoja na kwamba tumeambiwa mgao basi lakini Chukwani bado tunayo matatizo ya umeme, ukikatwa umeme yuko gizani hata kile kijenereta hana Mhe. Mwenyekiti huu ni udhalilifu kabisa. Nadhani ni vyema serikali ione kwamba hii mihimili inayo haki yake na itekelezwe.

Mhe. Mwenyekiti, unanihimiza sana, lakini nimalizie kuhusu suala zima la Zakka katika ukurasa wa 67 kiambatanisho cha 8A kinaonesha ule mgao wa Zakka. Mhe. Mwenyekiti, jana Mhe. Mohammed Mbwana Hamad alitoa maelezo kwa urefu kabisa tena kwa fasaha kabisa.

Kwa hivyo, mimi naomba kushauri sana kama Zakka huu ndio mgao wake basi tuite jina jengine na wala tusiite Zakka hali ya kuwa Ofisi hii ya Mufti inafahamu nini Zakka na ina wajibu gani pamoja na watu gani wanaopewa. Kwa kweli huu si utaratibu wa mgano wa Zakka, lakini nataka niseme hapa kwamba mara nyingi ndani ya Baraza hili tunasema katika wilaya 10 tulizonazo hapa Zanzibar Wilaya masikini kuliko zote ni Wilaya ya Micheweni, tupige kelele Mawaziri, Wawakilishi, Manaibu mawaziri, Wakurugenzi tuseme kwamba wilaya masikini kuliko zote ni Micheweni.

Mhe. Mwenyekiti, sasa leo ukiitoa Wilaya ya Chake Chake waliopata mgao mdogo kabisa basi ni Wilaya ya Micheweni. Katika hiyo Wilaya ya Micheweni watu ambao wanaostahiki wapewe hiyo tunayoita Zakka, basi

hakuna mtu hata mmoja na sisi tunapiga kelele kwamba Wilaya masikini ni Micheweni.

Zakka maana yake ni kumtoa mtu katika umasikini na kumuingiza kwenye utajiri, ili na yeye mwakani aweze kutoa Zakka, lakini wale masikini hatuwapi. Vile vile ndani ya wilaya hizi kuna Wilaya inaitwa wengineo.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, unayo dakika moja ya kumalizia.

Mhe. Rufai Said Rufai: Mhe. Mwenyekiti, ahsante. Kuna vikundi 7 na watu 108. Kwa hivyo, hii Wilaya wengineo ndio wilaya pekee iliyopata fedha nyingi kuliko hizo wilaya tunazozijua sisi na hili ni tatizo, yaani wengineo ndio waliopata fedha nyingi za Zakka kuliko zile wilaya ambazo zinajulikana, na mimi nilifikiri wengineo ni wilaya ndogo ya Kojani na Tumbatu.

Mhe. Mwenyekiti, namuomba Mhe. Waziri wakati atakapokuja kufanya majumuisho, basi aje anieleze kwa sababu hata wanaotakiwa kunufaika hapa ni wilaya, lakini kuna wilaya wengineo ni wilaya gani hii?

Mhe. Mwenyekiti, nashukuru na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, ahsante sana. Sasa ni zamu ya Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi, nakuomba sana ujali muda na baadaye atakuja Mhe. Hija Hassan Hija na tunataka kumpisha Mhe. Mwanasheria Mkuu kwa kuwa na yeye anazo hoja za kujibu na anayo shughuli maalum ya kufanya jioni.

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi: Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa napanga *point* zangu. Mhe. Mwenyekiti, nimpongeze Mhe. Waziri kwa hotuba yake hii ambayo wananchi wote wanaitegemea kusikiliza majibu ya Wajumbe hao yatakapotolewa na wizara hii. Kwa sababu wizara hii ndio wanayoitegemea wananchi wote kupata masuala yao ya kisheria na ya haki yakiwemo ya dini yetu ya Kiislamu.

Mhe. Mwenyekiti mimi nianze ukurasa wa 30 kifungu cha 83 Ofisi ya Mufti wa Zanzibar. Mhe. Mwenyekiti, Ofisi ya Mufti wa Zanzibar ina dhima kisheria ya kutoa miongozo kuhusu masuala ya kidini Zanzibar. Sasa nataka niseme hivi sasa tupo katika dunia ya utandawazi, hakuna Muislamu yeyote aliyeruhusiwa kula hadharani mchana wakati wa Mwezi Mtukufu wa Ramadhani, kwani Ofisi ndio msimamizi wa shughuli hizi za kidini.

Kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti, niseme kwamba leo iweje waislamu ao Ofisi hii ya Mufti ishindwe kukusanya maulamaa wake kujadili kuandama kwa

suala hili la mwezi, ili watu wasifunge bila ya kuandama kwa mwezi. Kwa sababu ifikapo kila mwezi wa Ramadhani Mhe. Mwenyekiti huwa kuna mzozano mkubwa sana baina ya Waislamu. Wengine hufunga kabla ya mwezi kuandama na wengine hufunga baada ya mwezi kuandama.

Mhe. Mwenyekiti, kwa nini mwaka wa kiislamu unapoingia watu iwe kuna mzozano na watu unapoingia mwaka mpya wa kiislam husherehekea kwa pamoja bila ya mzozano. Na watu wanaposimama Arafa Makka watu husimama kisimamo kwa pamoja. Leo iweje mwezi huu mtukufu wa Ramadhani iwe kuna mzozano? Namuomba Mhe. Waziri atakapokuja hapa anipe jibu zuri ili wananchi waweze kuelewa Mwezi huu Mtukufu wa Ramadhani.

Mhe. Mwenyekiti, nije katika Mahakama kifungu cha 34 ukurasa wa 14. Mhe. Mwenyekiti, nitanukuu tena kidogo.

"Mahakama ndio chombo chenye jukumu la Katiba na kusimamia utoaji wa haki, katika kufanikisha jukumu hilo usikilizaji wa kesi za jinai, madai, pamoja na rufaa za jinai na madai ni jambo la msingi."

Nataka niseme Mhe. Mwenyekiti, Mahakama kweli ni chombo cha wananchi ambacho wanakitegemea ili kupata haki zao za kisheria. Zipo kesi ambazo zimerundikana na bado hazijapata ufumbuzi. Bila ya kupata ufumbuzi kesi hizi inakuwa ni tatizo kubwa.

Je, Mhe. Waziri inakuwaje kesi za mitaani au kesi za kawaida ambazo dhamana zake na masharti yake ni madogo kesi zile zikawa zinakosa dhamana kwa muda mrefu? Mhe. Mwenyekiti, namuomba Mhe. Waziri atakapokuja anipe jibu ili niweze kuelewa, si hivyo Mhe. Mwenyekiti, siwezi kuzuia fungu wala siwezi kumzuilia mshahara wake lakini nitamkamata Mhe. Waziri mpaka anije jibu kamili ili niweze kuelewa.

Mhe. Mwenyekiti, nikija katika ukurasa wa 36 kifungu cha 100 kwenye Vizazi na Vifo. Mhe. Mwenyekiti, Afisi ya Mrajisi Vizazi na Vifo, hapa nataka niseme kwamba Wazanzibari wote ambao wamezaliwa Zanzibar huwa wana kumbukumbu zao. Kumbukumbu hizi huwa zinatunzwa katika Ofisi husika. Kama umezaliwa hospitali Wizara ya Afya ndio inayopelekewa vipande vile, na kama umezaliwa nyumbani huwa Masheha ndio wanaohusika na vipande vile.

Leo Mhe. Waziri, kwa nini watu wetu wanapodai vipande vyao huwa wanapatishwa tabu? Ni kwa nini tunao watu wameshafikia umri wa miaka 80 sasa hivi na hapo nyuma ilikuwa watu wale hawana uandikishwaji wa vyeti.

Lakini hivi sasa wanapodai haki zao Mhe. Waziri huwa wanababaishwa sana na wakienda pale huambiwa na mtoto mdogo letu kumbukumbu zako, kumbukumbu hizo atazipata wapi? Namuomba Mhe. Waziri, lingeundwa Baraza la Wazee wakakaa pamoja na serikali ili kulishughulikia suala hili la wazee ambao hawana vyeti na wao wakaweza kupata hazi zao.

Mhe. Mwenyekiti, nije katika ukurasa wa 31 kifungu cha 87 kinasema Ofisi pia imepata msasa wa mafunzo kuhusu njia bora ya kulingania dini ambapo vijana 14 wamepatiwa mafunzo hayo nchini Misri na India. Niseme kwamba mpaka hapa tulipo bado tunapeleka vijana wetu kwenda kusomea mafunzo ili waje kulingania dini? Hadi hii leo tuseme dini bado inalinganiwa tu? Hebu Mhe. Waziri utakapokuja naomba unipe majibu mazuri ili watu wetu wasije wakabakia kubabaishana na kupigana mapanga kwa wakati kama huu.

Mhe. Mwenyekiti nije katika kifungu cha 89 (32) Kifungu hichi kinasema kwamba nitakinukuu kinasema:

"Katika kuimarisha nyenzo za taaluma, Ofisi imeanzisha maktaba ya kiislamu na sasa imo katika jitihada za kutafuta vitabu zaidi kuimarisha maktaba hiyo, katika hatua nyengine Ofisi ya Mufti inaendelea kutekeleza mpango wa kutoa elimu ya kupambana na Ukimwi kwa mbinu za Kiislamu."

Namuomba Mhe. Waziri huoni ni vyema ukatuwekea wazi hili suala hizi mbinu za kiislamu ili waislamu wazielewe na kujinusuru na janga hili la ukimwi.

Mhe. Mwenyekiti, na mwisho nije katika Rasimu ya Katiba, kifungu cha 48. Niseme hapa kwa kuwa vyama vyote vya siasa na taasisi zote wametoa maoni yao katika katiba na mapendekezo yote yakachukuliwa. Je, Mhe. Waziri huoni kuna haja ya kulielimisha Baraza lako tukufu ili wakawa na msimamo mmoja kuhusu rasimu hii?

Mhe. Hija Hassan Hija: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, nachukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia uhai na uzima na muda huu kuweza kuzungumza masuala muhimu ya nchi yetu. Naomba pia nikupongeze na wewe kwa kunipa nafasi hii na nitajitahidi kutumia dakika 20 hadi saa tano na nusu 5:30 ambapo itakuwa ndio dakika 20 nimuachie Mhe. Mwanasheria Mkuu na yeye apate nafasi kwa ajili kuja kusaidia maelezo muhimu.

Mhe. Mwenyekiti, narejea ile kauli ya Mhe. Salmin Awadh Salmin ya jana aliyotukumbusha kwamba Baraza sio Mahakama wala Baraza sio Serikali. Wajumbe wako Mhe. Mwenyekiti, wanatambua kwamba sisi wajibu wetu ni

kutunga sheria na kuwasemea wananchi mbele ya serikali. Lakini wananchi wamejenga imani na Baraza kwa sababu wamechoshwa na matendo ambayo si mazuri wakati mwengine ya serikali na Mahakama zetu. Kwa hiyo tunapozungumza mambo ambayo yanawagusa wananchi isionekane kwamba Baraza linaingilia mihimili mengine lakini baada ya wananchi kujenga imani na chombo hichi Mhe. Mwenyekiti.

Na mimi nichukue nafasi hii niwaombe wananchi waendelee kutufuatilia na kutupa malalamiko yao kama wanayo. Na niwaombe Wawakilishi waweze kuwatetea wananchi kwa manufaa ya nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, kuna watu hujiuliza nini Mahakama? Kuna wengine wanaamini kwamba Mahakama ni chombo cha kutoa haki. Kuna wengine wanaamini kwamba ni chombo cha kutafsiri sheria na kuna wengine kama mimi naamini kwamba ni chombo cha kutoa haki kwa kufuata sheria. Katika tafsiri yoyote ambayo itazungumzwa lakini Mahakama ni muhimili wa dola ambao lengo lake hasa ni kutafsiri sheria na kutoa haki kwa wanaohusika.

Mhe. Mwenyekiti, siku moja nilimsikia Jaji mmoja analalamika kwamba Wawakilishi hawazungumzii uchache wa fedha kwenye Mahakama zetu, wao kazi yao kubwa ni kuzungumzia kwamba Mahakama hazifanyi haki, kesi haziendeshwi. Nataka nikumbushe kwamba Baraza hili limekuwa mstari wa mbele kutetea maslahi ya Mahakama zetu kwa maana ya kwamba zipatiwe fedha Mahakama zetu na maslahi ya wafanyakazi.

Mhe. Mwenyekiti, lakini tujiulize je, tatizo la Mahakama zetu kushindwa haki ni kwa sababu ya fedha? Mimi nasema inawezekana ikawa ni sababu moja lakini sababu nyengine ambayo mimi naiona ni ukosefu wa maadili kwa baadhi ya watendaji wetu. Sababu ya pili ambayo mimi naiona ni kwamba bado kuna dalili za rushwa katika Mahakama zetu ambazo zimeikabili. Mwisho kwa mtazamo wangu ni kwamba Mahakama zetu zinashindwa kufanya kazi kwa sababu kuna muingilio kwa kiasi fulani wa siasa katika Mahakama zetu.

Mhe. Mwenyekiti, nimechambua hizi kesi ambazo Mhe. Waziri ametuelezea katika kitabu chake ni kesi 6039 ambazo zimesajiliwa kwenye Mahakama zetu katika kipindi hichi cha mwaka wa bajeti uliopita. Ukiangalia kesi ambazo zimepatiwa majibu au zimetolewa hukumu ni kesi 2772 sawa na asilimia 45.9 ya kesi. Kwa maana ya kwamba mwaka mzima wa kesi zetu zilizosajiliwa, majibu ambayo kesi zimeamuliwa ni kesi asilimia 45.9. Ukiangalia kesi ambazo zina hali ngumu ni kesi za Mahakama za Kadhi.

Mhe. Mwenyekiti, Mahakama za Kadhi, Mhe, Mwenyekiti wamesajili kesi 1222 lakini kesi ambazo zimepatiwa majibu ni kesi 311 sawa na silimia 25.5. Kwa maana kwamba kwa mwaka mzima kesi ambazo zimetolewa majibu kwa mwezi ni kesi tatu kwa wastani wa Mahakama zetu ambazo ni Mahakama 11 za Kadhi. Hii ni hatari kwamba mwaka mzima Mahakama zetu za kadhi zimetoa hukumu kesi tatu kwa mwaka. Mahakama hizi 11 tulizonazo, ni dhahiri kwamba kesi 1222 zimebakia katika mtiririko wa malalamiko ya wananchi wetu.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nimuombe Mhe. Waziri aiangalie hali hiyo kwamba leo Mahakama za Kadhi zinatoa maamuzi kesi 311 kwenye kesi 1222 ambazo zimesajiliwa kwa mwaka uliopita. Mhe. Mwenyekiti, nadhani huu sio utaratibu mzuri, lazima tupatiwe jawabu la msingi kwa nini Mahakama zinashindwa kutoa haki na wala si kweli kwamba kwa sababu ya uchache wa fedha peke yake. Lakini inaonekana ni kwa sababu ya kwamba uadilifu umepungua, na rushwa bado Mahakama zetu imezikabili.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo sasa nizungumzie suala zima la Mahakama kwa upande wa utoaji wa maamuzi. Wenzangu wamezungumzia kwamba Mahakama zetu zimekuwa zikitoa maamuzi, lakini hakuna utekelezaji wa maamuzi mbali mbali. Mimi nimefanya utafiti nimepata kama kesi nne hapa ambazo zimetolewa maamuzi na Mahakama mbali mbali. Mahakama za Mwanzo, Mahakama za Mkoa hadi Mahakama Kuu na hadi Mahakama za Rufaa lakini zimeshindwa kutekeleza maamuzi yake. Sasa Mhe. Mwenyekiti, hii ni hatari. Mahakama imeamua kesi mbali mbali lakini hakuna maamuzi na hatimaye yule anayetoa haki baadaye anashindwa kupata haki kwa sababu hakuna maamuzi ya serikali ya kusimamia haki ile.

Mhe. Mwenyekiti, nataka nitaje kesi tatu ambazo zinasikitisha. Kesi moja ni ya kuwania shamba. Mahakama imeamua kesi shamba lililokuwepo Mwanakwerekwe na Mahakama imetoa haki lakini tunaambiwa eti hakuna kanuni tu za kutekeleza ile hukumu imeshinda ni mwaka wa tatu huu. Mahakama imetoa haki lakini hakuna utekelezaji wa hatua ile ya hukumu. Sasa Mhe. Mwenyekiti, kwa nini basi tusiamini kwamba Mahakama zetu zinashindwa kutekeleza haki kwa sababu kuna nguvu za watu fulani au kuna mkono wa fedha?

Mhe. Mwenyekiti, ili niweze kupitisha bajeti hii naomba Mhe. Waziri na nitampa hizi *copy* aje anipe jawabu kwa nini Wizara yake chini ya Mahakama imeshindwa kutekeleza hukumu hizi huku wakiwa wametoa haki kwa wananchi husika. Vyenginevyo mimi nitashindwa kuiwezesha bajeti hii kwa sababu sioni msingi wa kufanya hivyo.

Mhe. Mwenyekiti, jambo jengine ambalo nataka niliseme ni kesi maarufu ya ndugu yangu Mahmoud Gulam Ismail na Bi Sabrina Bashir Hassan Ali, ambayo hii ilianza mahakama ya Mwanakwerekwe. Na hii ni kesi ya ndoa ambayo ilikuwa kwenye Mahakama ya Kadhi ilianza Mwanakwerekwe, Mahakama ya Wilaya, kule yakatoka maamuzi ambayo kila mtu alilalamika na magazeti yakaandika taarifa mbali mbali kwamba kesi ile iliashiria kuna rushwa. Magazeti yaliandika na Mhe. Waziri mwaka jana akakiri kwamba suala hili lipo kwenye meza ya *DPP*. Sasa naomba nipate jibu imefikia hatua gani.

Lakini baada ya hapo bi Sabrina alikata rufaa Mahakama ya Kadhi Mkoa kule ikatolewa haki kwamba mwenye haki ya kuchukua malezi ya mtoto chini ya miaka saba ni mama na hiyo ni kwa mujibu wa Sheria. Hata ile Sheria ya Mtoto ambayo Baraza hili tumeidhinisha kwamba mtoto chini ya umri wa miaka saba ana haki ya kupata malezi kwa mama. Lakini Mahakama ya Kadhi Mkoa ikatoa maamuzi hayo na ikampa haki mama.

Hatimaye kama ilivyo sheria Bwana Mahmoud akakata rufaa kwenye Mahakama Kuu, ambayo ni haki yake ya msingi. Mahakama Kuu wametoa maamuzi baada ya kurejesha haki ile kwa baba na zaidi Mahakama kuu wamefanya suluhu. Sasa naomba kujua Mhe. Waziri je, kufanya suluhu katika kesi hii ni haki ya Mahakama au walipaswa wamsikilize mdai na watoe maamuzi sio kufanya suluhu?

Mhe. Mwenyekiti la kusikitisha hapa ni kwamba Mahakama sasa imetoa suluhu lakini upande wa pili wameomba kupitia kesi, wameomba mapitio upande huu wa bi Sabrina tayari wanatishwa kwamba hawana ruhusa ya kufanya mapitio. Jambo ambalo mapitio ni haki ya msingi kwa mdai. Mhe. Mwenyekiti, ili niweze kupitisha bajeti hii vile vile naomba nipate maelezo ya kina kwa nini Mahakama hizi wanaweka vikwazo juu ya maamuzi ya wateja kupitia mapitio ya maamuzi ya kesi ili watu wajiridhishe na kuweza kufungua madai mengine kama kuna msingi huo.

Mhe. Mwenyekiti, kama hilo ndilo nadhani si busara Mahakama kuendelea kuwatisha wananchi kwa msingi ambao si sahihi. Hii itatoa tafsiri kwamba Mahakama zetu zinakabiliwa na rushwa na kwa hivyo mwenye nguvu ndiye mwenye haki na asiye na nguvu hana haki ya mzingi. Naomba nipate maelezo ya kesi hiyo kwa nini haki ya kufanya mapitio imezuiliwa kwa wananchi wetu?

Jengine ambalo nataka niseme ni ndoa na talaka. Mhe. Mwenyekiti, mwaka jana tulizungumza kwamba bado Zanzibar tunakabiliwa na ndoa feki na talaka feki. Kwamba kuna watu wanapoamua kupata mke au mwanamke

wanadiriki kubadilisha majina, lile jina linakuwa la kikristo lakini anabadilisha jina la kiislamu ili apate mke. Jambo hilo mwaka jana tulimwambia Mhe. Waziri lakini inaelekea kesi ile bado inaendelea.

Hivyo hivyo Mhe. Waziri bado kuna talaka ambazo zinalalamikiwa kwamba sio talaka sahihi. Sasa mimi kwa msingi huo na naomba nisimtaje yule aliyehusika lakini nina talaka hapa Mhe. Mwenyekiti. Talaka ambayo imeshukiwa imepatikana kwa shilingi laki mbili. Talaka hii Mhe. Mwenyekiti inahofiwa kwamba ilitolewa kwa gharama ya shilingi laki mbili. Mwanamme hadi leo hajui kama Mahakama ya Kadhi mke wake wamemuachisha. Maana yake hakuna mwenendo wa kesi iliyokwenda, mwanamme hadi leo hajaitwa vipi unaweza kumuachisha mke huyo?

Mhe. Mwenyekiti, naomba nikukabidhi talaka hii na unipatie *file* na mwenendo wa kesi hii kwa nini mwanamke huyu ameachishwa kwa mumewe bila ya mume kuitwa na wakati mume huyu yupo Zanzibar hajaondoka wala hakuna sehemu ambayo ameitwa. Talaka hii Mhe. Mwenyekiti imetolewa ndani ya nusu saa hakuna utaratibu ambao ulifuatwa. Mhe. Mwenyekiti, nakuomba sana talaka hii nikukabidhi *copy* lakini majibu yako yote nakuomba unipatie *file* la mwenendo wa kesi hii lini aliitwa na kesi ilienda vipi hata ikabidi Mahakama yako itoe maamuzi ya talaka hii na leo huyu mwanamke ameolewa. Naomba nisimtaje kwa sababu ya usalama wake na mume yupo Unguja hajaitwa hadi leo kuambiwa kwamba mke wako ameolewa na ameachishwa na Mahakama hii.

Mhe. Mwenyekiti, vipi tutoe ruhusa ya fedha hizi na haya wanayafanya Waislamu, ingelikuwa wanayafanya *George* na *John* tungesema bahati mbaya, lakini wanayoyafanya ni waislamu. Tena ni katika nchi ambayo tunaambiwa 99% ni waislamu. Ni dhahiri kwamba hili ni tatizo na lazima talaka hii Mhe. Mwenyekiti, nipate jibu, na jibu ni kwamba unipatie mwenendo wa *file* ya kesi hii lini waliitwa, kesi ilikuwaje. Mimi ninavyojua kwamba huyu mtu alifika Alhamis asubuhi saa 3:00 saa 4:00 akapewa talaka bila ya mtu kujua. Mhe. Mwenyekiti, naomba hii nikukabidhi naomba wale wafanyakazi waje kuichukua wampatie Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria ili anipatie jibu la talaka hii imekwenda vipi.

Mhe. Mwenyekiti, naomba nizungumzie masuala muhimu ya Ofisi wa *DPP*. Mhe. Mwenyekiti, sisi hatumzungumzi *DPP* kwa utashi, kwamba labda alikuwa Katibu wa Baraza sasa hivi ni *DPP*, tunazungumza kwamba huwezi kupata kesi kama hujawatunza Maafisa wa *DPP*. Mhe. Mwenyekiti, naomba sana Mhe. Waziri kwa heshima kubwa, maslahi ya Maafisa wa *DPP* ni lazima yazingatiwe. Ninazo taarifa kwamba hivi sasa kwenye meza ya *DPP* kuna barua sita za maafisa wa *DPP* kutaka kuacha kazi. Sasa maafisa sita wakiacha

kazi maana yake hiyo kazi itakuwa haitendeki, maana yake kesi itakuwa haziendeshwi. Nakuomba sana Mhe. Waziri, lazima utupe majibu kwa nini maslahi ya wafanyakazi hawa hayazingatiwi?

Mhe. Mwenyekiti, suala jengine kwa sababu ya muda nizungumzie suala zima la Rasimu ya Katiba. Mimi binafsi siungi mkono hii rasimu ilivyo. Hii rasimu ilivyo hakuna wa kunishawishi nikaiunga mkono. Na niombe Wazanzibari wenzangu na niombe Wawakilishi wenzangu kwamba hivi rasimu ilivyo haitekelezeki na siiungi mkono. Lazima tuzingatie maslahi ya nchi kwanza. Na tugombane kwa misingi yoyote lakini kwanza maslahi ya nchi. Maslahi ya nchi ni lazima tuwe na ile misingi minne ya nchi kwa maana ya watu, mipaka, serikali na uhusiano wa kimataifa.

Mhe. Mwenyekiti, niwaombe Wazanzibari wenzangu na hasa Wawakilishi kwamba tusiangalie maslahi yetu, tusiangalie kwamba Katiba mpya ikija hivi mimi nitakosa Uwaziri au Uraisi, tusiangalie hivyo, tuangalie jinsi gani Wazanzibari watapata haki na maendeleo ya nchi yao. Na hayo hatuwezi kuyapata kama hatukuweza kuwa na mamlaka kamili ya Zanzibar ndani na nje ya nchi. Kwa hivyo ukijiangalia wewe tu binafsi basi nchi itapotea. Mwakilishi akijiangalia yeye na Uwakilishi wake maana Katiba mpya ikija na marekebisho kwamba mimi nitakosa uwakilishi utakuwa ni muflis. Lakini tuangalie vipi nchi yetu itadumisha maslahi yake ndani na nje ya nchi.

Mhe. Mwenyekiti, mimi niwaombe sana Wazanzibari wenzangu tusiangalie sera za vyama. Mimi chama changu kina sera ya serikali tatu, lakini niko tayari kuziacha ili kuunga mkono maslahi ya Zanzibar. Na wale wenzangu wenye sera ya serikali mbili, moja, na nusu serikali, basi wakubali kuacha msimamo wao kwa maslahi ya Zanzibar. Mhe. Mwenyekiti, Wazanzibari wanahitaji kulindwa, kutetewa na kusaidiwa katika maslahi yao ili tuwe viongozi wazuri kwa maslahi ya wananchi wetu.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo siungi mkono hotuba hii mpaka nipatiwe ufafanuzi wa talaka ile na kesi ya bwana Bashir na mwengine vipi imefikiwa na kwa nini mahakama haifanyi haki? Mhe. Mwenyekiti, niseme hivyo na nitangulize kusema tu kwamba siungi mkono hotuba hii mpaka nipate maelezo hayo.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, kwanza na mimi nitangulie kukushukuru kwa kunipa fursa hii na kunikubalia udhuru wangu. Lakini pili nitangulie kusema kwamba naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Naamini hata wale wana shakashaka zao zitaondolewa na naamini mwisho wataunga mkono kwa asilimia mia moja vile vile.

Pia niipe pongezi na niishukuru sana Kamati yetu ya sheria na utawala, kwanza kuwa na wajumbe ambao makini, lakini na pia tunashukuru kwa kupata Mwenyekiti kwanza kijana, mahiri, na ambaye naamini atatusaidia katika kuifanya kazi hii ya Wizara yetu kwa umakini zaidi.

Mimi nilikuwa nina mambo machache tu, ambayo yalizungumzwa na mimi naomba nimsaidie Mhe. Waziri na Waheshimiwa Wajumbe katika kutoa baadhi ya ufafanuzi.

Kwanza ni suala ambalo alilizungumza alipowasilisha Mhe. Wanu taarifa ya Kamati kuhusiana na suala la ujenzi wa Ofisi kwamba kweli ilikuwa imekwama kwa muda mrefu kutokana na ukosefu wa fedha. Kwa sababu kama tulivyoripoti hadi mwezi wa machi tulikuwa tumepatiwa milioni 800 (mia nane) lakini naomba niwahakikishie Waheshimiwa Wajumbe hadi kufika mwisho wa mwezi wa Juni tumepatiwa fedha zote ambazo zilitengwa kwa mwaka huu yaani bilioni moja na milioni mia nane kwa ajili ya kuendelea na kazi ya ujenzi. Kwa hiyo tunaamini kwamba kwa fedha hizo kazi za ujenzi zitakwenda kwa haraka zaidi sasa hivi na zitakwenda kwa asilimia kubwa kuweza kukamilisha, labda yatabakia mambo mengine madogo madogo.

Jengine ni lile suala ambalo labda pengine kama palikuwa na mapungufu ni kwenye *OC* ambako tulikosa milioni tisini na nane, kati ya fedha zote zilizokuwa zimetengwa. Tunategemea labda katika mwaka ujao tutapata fedha nyingi zaidi tuweze kutekeleza majukumu yetu.

Jengine ambalo Mhe. Mwanasheria mkubwa Mhe. Mshimba alitaka mahsusi mimi nimpe ufafanuzi kuhusiana na kifungu cha 94 (6)(b) Cha Katiba nadhani hakukitizama vizuri sana, lakini kinahusu maslahi ya Kaimu Jaji yaani yule mtu ambaye atateuliwa kwa mkataba wa kile kifungu ambacho kinaruhusu. Sasa kimesema tu kwamba yale maslahi ya yule Kaimu Jaji ndiyo ambayo yanawekwa na Tume ya Utumishi ya Mahakama lakini sio ya Majaji wote. Majaji wote kama ilivyo kawaida yanapendekezwa katika taasisi inayohusika na baadaye hatua zinachukuliwa. Hii inahusu Kaimu Jaji na kifungu kimeeleza vizuri sana.

Nashukuru kwanza kwa maneno ya ukarimu aliyotwambia Mhe. Ismail Jussa na mimi nasema yanatushajihisha sana. Na kusema kweli nirudie yale maneno wanayosema wazungu kwamba, *the best reward for a job well done is an opportunity to do more.* Yaani mtu akifanya vizuri basi zawadi yake kubwa mpe fursa afanye zaidi. Kwa hivyo na sisi tunashukuru kwa kutuamini huko tutaendelea kufanya kazi zetu vizuri.

Kwanza nikubaliane naye kuhusu lile aliloshauri la kuwaelimisha Waheshimwa Wajumbe kuhusiana na sheria namba 7 ya mwaka 1984. Kusema kweli sheria hii ni muhimu kwa sababu ndiyo inayotusaidia kupata ufafanuzi, maana sheria wakati tunapoitunga tu ndio inakuwa ni maneno lakini wakati wa kuifanyia kazi ina mambo mengi, na jambo la msingi ni namna gani tunaitafsiri ile sheria yenyewe. Kwa hivyo kuifahamu na hii sheria namba 7 ndio imetuwekea muongozo wa namna gani sheria tunaweza tukaitafutia.

Kwa hivyo mimi nitashirikiana na Ofisi ya Baraza katika hili lakini nichukue ahadi kwamba angalau kwa kuanzia kama vile PAC inapopewa mafunzo maalum basi na Ofisi yetu itachukua juhudi angalau kwa kuanzia kamati yetu ya Sheria na Utawala kuipa mafunzo maalum kuhusiana na suala hili. Na pengine yenyewe itasaidia kuwawezesha na wengine vile vile.

Lakini jengine alizungumzia kuhusu kuanzishwa kwa kitengo cha mikataba na akasema kwamba ni vizuri basi kuanzisha na kitengo cha mafuta. Naomba niliahidi Baraza hili kwamba hatua tumeanza kuzichukua na niungane hapa na yale aliyoyasema Mhe. Mtando vile vile kuhusiana na matatizo katika mikataba ya serikali. Na niseme ni kweli kwamba kuna matatizo mengi sana. Matatizo yanaanzia hata kumjua yule tunayefunga naye mkataba, kwenye mabenki huku kuna kitu anasema *know your customer*. Sasa sisi yule tunayefunga naye mkataba wakati mwengine hata ile kumjua kwamba huyu ni nani? Kweli ni kampuni? Kusema kweli ule utaratibu na ndio hilo jambo la msingi na la awali ukishamjua unaweza ukasema aa wewe hufai kuingia mkataba na serikali, lakini tunayaainisha na tunayafanyia kazi.

Lakini na jengine ni kujenga uwezo. Kwa sababu mambo haya yanahitaji sana kujenga uwezo. Na hilo ndio jambo ambalo tumeazimia kulifanya kwa nguvu zetu zote na kwa kutafuta msaada wa kila aina ili tuweze kujenga uwezo. Lakini hili la kitengo cha mafuta naomba nimuahidi kwamba azma hiyo tunayo na tuna watu ambao tumeanza kuwapeleka katika mafunzo na itakuwa pia katika kitengo hiki hiki cha mikataba. Tutakuwa na *special unit* ambayo pia itashughulika na suala hili. Lakini labda niseme kwamba kwenye mkataba kuna mambo 2. La kwanza ni kuhusiana na masuala ya kisheria lakini la pili ni kuhusiana na masuala ya kiuchumi. Kwa mfano sisi Ofisi ya Mwanasheria Mkuu hatuwezi kujua kwamba bei hii inayotaka kununuliwa gari au inayotaka kujengwa jengo ni sawa au si sawa, ni ghali si ghali, au masharti mengine ambayo ya kiuchumi. Lakini tunaahidi kwamba tutaweka masharti ambayo tutashirikiana na wenzetu na hilo kulipatia ufumbuzi vile vile tujiridhishe kwamba hili nalo kiuchumi ni sawa na linakubalika.

Suala la kanuni kile kitengo chetu ambacho tunakusudia kukianzisha cha *legislative drafting* na *legal policy* basi moja katika kazi yake itakuwa ni hii. Kwa hivyo *inshaallah* hilo tutalichukulia hatua.

Na jengine ambalo alizungumza Mhe. Mtando ni kuhusiana na mikataba, nadhani nimelijibu au nimelieleza na kwa sababu ya muda sipendi nirudie tena kwa kweli najua leo ni siku ya bajeti ya mashekhe na siku ya kishekhe maana yake *yaumul jumaa*. Lakini yeye alizungumzia kuhusiana na maslahi ya watendaji na alizungumzia pia mahsusi katika ofisi yetu kama ilivyo katika ofisi nyengine.

Mimi hapa labda kwanza niseme naomba nichukue fursa hii kuishukuru sana serikali kwa kupandisha na kuyaweka vizuri maslahi ya mahkama kwa upande wa majaji na mahakimu. Siku zote katika kutafuta basi muombee mwenzako apate. Kwa hivyo serikali imeanza na tumechukua juhudi kubwa kuhakikisha kwamba na wengine wanapata. Lakini labda naomba niwafahamishe kitu kidogo tu kwa nini labda inaonekana ile tofauti baina ya Mahkama wengine ni kubwa. Katika utumishi kuna nafasi za namna mbili.

Kuna nafasi za kiwadhifa yaani tunaita *establishment post* na kuna nafasi za kiutendaji yaani tunaita *duty post.* Nafasi ya kiwadhifa kwa mfano ni kama hii Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, hapa ukiwa na *PHD* na Mhe. Mtando ana jina lake anasema *PHD visa* ukiwa nayo yote ni sawa sawa maslahi nyote mnakuwa ni sawa. Ni sawa sawa kwa mfano nafasi ya Ukurugenzi, nafasi ya Ukurugenzi ikiwa mtu ana *PHD* na mwenye *Diploma* au *Ceritificate as long as* wameteuliwa Wakurugenzi basi mshahara wao, maslahi yao yanakuwa ni sawa sawa.

Sasa serikali kwa *nature* ya ule muundo wa mahkama iliamua kuzifanya nafasi za mahakimu ni *establishment post,* yaani kwa mfano katika muundo wa kiserikali kuna Mkuu wa Mkoa lakini kimuhimili kuna hakimu wa Mkoa. Kwa hivyo ikapewa hadhi kwamba yule hakimu wa Mkoa ni nafasi ya wadhifa na hakimu wa Wilaya imepewa nafasi kama ni nafasi ya wadhifa. Na mara nyingi utakuta hakimu wa Wilaya inawezekana katika Wilaya mmoja au wawili.

Sasa hayo utayakuta kwamba ndio maana ule muundo wenyewe pia umebadilika na ile mishahara pia imebadilika, kwa sababu ya kupewa hiyo hadhi ya *establishment post.* Kwa kawaida katika hizi nafasi kwa mfano za kiutendaji za wanasheria ni kama vile madaktari *unless* una nafasi ya kiwadhifa huwezi kuwafanya madaktari wote wakawa na *establishment post* zitakuwa ni *duty post.* Huwezi kuwafanya wanasheria wote wakawa na *establishment post* watakuwa na *duty post.* Cha muhimu ni kweli maana sisi

ndio tunaowaona wenzetu tunaowaongoza hawa kazi wanazozifanya, lakini mimi ninachowahakikishia kwamba tuna raslimali kubwa sana katika wanasheria tulionao kwa sababu kusema kweli inahitaji fedha nyingi kumfunza mpaka ukaweza kumuita Mwanasheria. Na hizi kazi nyengine wanazofanya ni nyeti si kila kitu wanakishughulikia *DPP*. Unaweza ukapigwa chenga hilo jambo lisifike mahkamani la mamilioni na mabilioni kusema kweli. Kwa hivyo kazi wanazofanya ni nyeti na kusema kweli naamini serikali imesikia hilo na tunaamini kwamba hatimaye na tunawashukuru sana Waheshimiwa Wajumbe kwa kuliona hilo na kuungana nasi katika kutetea maslahi ya watendaji hao.

Jengine la mwisho ambalo alilizungumzia Mhe. Mtando lilikuwa suala la ununuzi wa gari nikashangaa kwamba sahibu wangu anaona kwamba nikipata gari ningefikiri atanitetea. Lakini mwaka juzi tulipewa 65 milioni, mwaka jana 60, mwaka huu tunataka 80.

Kwanza niseme tu Mhe. Mwenyekiti kusema kweli mimi nilipofika au ofisi ile ilikuwa na tatizo kubwa sana la usafiri. Maana ukiachia gari ya Mwanasheria Mkuu ambayo ndio ilikuwa kila kitu hapakuwa na gari hata moja nyengine labda na vespa mbili zilizokuwepo. Kwa hivyo tulichukua juhudi maalum kushughulikia suala hili na zile 65 milioni za mwanzo tukanunua *pickup,* lakini tukanunua kibajaji kwa ajili ya kusambazia barua na mambo madogo madogo ili kupunguza matumizi ya hii gari nyengine.

Lakini pia tukanunua na ile rai ya Mhe. Hamza sisi tulianza kuitekeleza mwanzo kwamba madereva wetu wote tukawanunulia vespa na tunawagaia na mafuta ya kuweza kuzitumia. Kwa hivyo milioni 60 za pili bahati mbaya zilizama na meli hatukuzipata. Kwa hivyo ndio maana tukaomba hizi 85 ili tuimarishe usafiri kwa sababu tumeongezeka, shughuli zimeongezeka na kwa kweli tunahitaji usafiri ili Ofisi ile iweze kufanya kazi vizuri. Nadhani Mheshimiwa sahibu wangu itakuwa nimemtosha kwa hapo.

La mwisho Mhe. Mwenyekiti mimi naomba nizungumzie kidogo tu kuhusiana na suala ambalo limezungumzwa takriban na Waheshimiwa Wajumbe wote waliochangia suala la rasimu. Na leo sikusudii kuzungumza *particulars* au mambo yaliyomo kwenye rasimu. Mimi naomba nizungumze machache sana kwa sababu kwanza ya muda, lakini nadhani na Waheshimiwa wengi wamezungumza mengi vile vile.

Mimi naomba nianze pale aliposema Mhe. Salmin kasema neno zuri sana na mimi naomba tuliunge mkono sana, kwamba pamoja na yote lakini tuangalie kuimarisha Muungano. Suala ni vipi tutaimarisha muungano? Mimi naamini na naanzia kwenye dini yetu maana dini yetu imetuhimiza tuandikiane

tunapopeana mambo, tunapouziana, usiseme huyu ni rafiki yangu basi mimi ninamuamini. Kwa sababu tulivyoambiwa hivyo ilikuwa ishafahamika, kwamba huyo rafiki yako leo kesho anaweza akakugeuka. Na ili muandikiane hatukuambiwa tuandikiane basi iwemo kwenye karatasi tu aa, yale mnoandikiana kwanza mfahamiane na mkubaliane kwamba haya ndiyo tunayofahamiana.

Mhe. Mwenyekiti nadhani ni msingi wa mahusiano yoyote, mahusiano yenye shaka hayajengi imani kusema kweli. Mahusiano kama yatakuwa na uaminifu na kuaminiana mimi naamini ndio yataimarika na historia ya dunia imeonesha hivyo kwamba katika na nchi ambazo ni imara ni zile ambazo zina miungano lakini miungano yao imejengwa juu ya kuaminiana, kuheshimiana, juu ya kuwa na nyenzo ambazo zitaondoa shaka.

Kwa hivyo mimi nasema kwamba yale maneno ya Mhe. Salmin kwamba tuimarishe Muungano ni kweli. Lakini njia nzuri ni kwamba tuondoe hizi shaka. Yaani tuitumie *process* hii ya mchakato huu katika kuondoa shaka za muungano, bahati nzuri tumepata *experience* au uzoefu wa miaka 50. Tatizo letu kubwa tunaona haya kuzisema hizi shaka ndio shida yetu. (*Makofi)* Maana muungano kusema kweli umejaa shaka nyingi ndio tatizo lake kusema kweli.

Na mimi nasema kama kwa shaka hizi ziliomo tushukuru maana hii mimi Mhe. Hamza anavyozieleza shaka za muungano napenda sana, maana yeye mwenzangu hodari mpaka huigiza. Kwamba ingekuwa tunayajua, tatizo letu hii Katiba iliyopo sasa hatuisomi vizuri, lakini kama tunaisoma vizuri basi nadhani tungezimia! Tungezimia kama yule mtu aliyempiga kwa kipemba anasema alompiga ngea simba akidhani ni ng'ombe alipojua kwamba ni simba akazimia kumbe keshampiga chenga. Sasa na sisi ni hivyo hivyo kwamba pengine hatusomi hiki kilichopo sasa hivi tukajua hizo shaka ziliomo na tukatafuta njia tuzione wengine. Maana yake mimi inanishangaza Mhe. Mwenyekiti wengine wanakuona adui ukizizungumza shaka za muungano. Watakupa majina ukizizungumza shaka za muungano. Sasa mimi nadhani labda nitumie ile lugha tunayoifahamu au turudi kwenye jadi, maana unaambiwa ukishindwa kote basi rudi kwenye jadi. Kule kwetu tunasema labda mimi nasema labda tumeliwa na chechele.

Mhe. Mwenyekiti sijui wengine kwenye lahaja nyengine wanachukuliwa na chechele maana yake nini. Lakini si hili jengo la Baraza unakuja kila siku, siku ukiliwa na chechele hulioni kabisa utaishia kambi ya jeshi kule. Utatafuta geti la Baraza liko wapi, maana haiwezekani kama hapa tumepata fursa ya kuzizungumza hizi shaka tuziondoe tuimarishe huo muungano wenyewe, tunagombana kwa kuzizungumza shaka. Tunaitana majina kwa kuzizungumza

shaka, tumegawanyika kwa kuzizungumza shaka za muungano. Sasa kama si kuliwa na chechele ni kitu gani? Kwamba hili ndio geti la Baraza la Wawakilishi Mhe. Mwenyekiti kila siku unakuja hapa leo hulijui, unapokuwa hulijui tunakuwa na mashaka. Na kwenye kiswahili Mhe. Mwenyekiti na Waheshimiwa Wajumbe kila kitu kina jina lake mtoto wa ng'ombe huitwa ndama na wa kuku akaitwa kifaranga. Sasa ukimuona mtu ndama anamuita mtoto wa ng'ombe ujue kuna mawili; ama hajui Kiswahili au ana jambo anaficha.

Na ukisikia kifaranga anakiita mtoto wa kuku basi lazima ujue huyu bwana ana matatizo ama Kiswahili kidogo anajifundisha sasa au ana kitu anakificha, asingeita mtoto wa kuku. Sasa mimi ndio nasema kule kwetu ukiliwa na chechele wazee wetu hukwambia aa soma *suratul mulk*. Ukianza ile aya ya kwanza mpaka ukimaliza aya ya 30 njia utaijua.

Sasa na mimi labda nitoe rai niwape zindiko lile la kwetu la Masipa kwamba kwa chechele huyu aliyetula katika hili tukitaka labda tuzinduke tuwaombe leo bajeti ya mashekhe wakitoka hapa waende wakaanze kutusomea ile *suratul al imran* kuanzia aya ya 102 labda wakifika mpaka 128. Mimi naamini atakayesoma akafahamishwa maana yake akajua tafsiri yake naamini baada ya wiki tutazinduka. Na yakija mabaraza ya Katiba ninaamini kwamba tutaweza!

Ninalokusudia kusema Mhe. Mwenyekiti sisemi hili kwa utani! Anayetaka kwenda kusoma wakasome, leo mashekh nasema wapo, Mufti yupo, Makadhi wapo lakini ninalokusudia kusema, kusema kweli jamani tunachelewa katika hili. Fursa hii katuletea Mungu kwa sababu tulianza kuungana, tena chombo hiki imekuwa kielelezo cha kuungana watu. Maana tulianza kupitisha azimio lile la mafuta mwaka 2009 kabla ya *GNU*, tukaja Baraza hili hili tukapitisha *GNU*, sasa siku zote ukiungana mkawa mmeondoa tafauti zenu Mungu huwaletea neema!

Sasa kwa sababu ya kuungana kule 2009, na tukafanya tena 2010 ninachoamini mimi kwamba hii rasimu ya katiba mchakato wa katiba imekuja ni neema Mungu aliyotupa kwa kuungana kule. Sasa kama leo tunataka kuvunja lile, maana tutarudi kweli ya kule hata tulikotoka, mimi nawaomba sana tuthamini hayo na tuthamini kwamba hii ni zawadi Mungu ametuletea kwa sababu ya nia zetu na kuungana kwetu 2009, 2010 na mpaka leo kwamba tuna *GNU*.

Mimi Mhe. Mwenyekiti nimalizie kwa kuunga mkono hoja. Ninashukuru sana.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Mwanasheria Mkuu ninafikiri wengi wetu wameyasikia uliyoyasema na vile vile tumeyafahamu na sote kwa pamoja tumuombe Mwenyezi Mungu atufikishe pale ambapo sote tutaridhika. Waheshimiwa Wajumbe muda uliobakia ni mchache sana, tutakapofika jioni tutawapa nafasi wachangiaji wawili tu kumalizia wameniomba sana wana mambo muhimu na baadae nitampa nafasi Mhe. Waziri kuja kufanya majumuisho.

Kabla ya kuakhirisha kikao naomba kuwatangazia Wajumbe wanawake kuwa yale mafunzo yetu leo yanaendelea baada tu ya kutoka hapa, kwa hivyo naomba sana sote tuhudhurie kwa pamoja na faida zake zinaonekana. Ahsanteni.

(Saa 5.50 asubuhi Baraza liliakhirishwa hadi saa 11.00 jioni)

(*Saa 11.00 jioni Baraza lilirudia)*

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Ali Mzee Ali: Mhe. Mwenyekiti, nikushuruku sana na mimi kunipa nafasi nizungumze. Kwanza Mhe. Mwenyekiti, nataka kusema hivi, leo ni Ijumaa ya mwisho, Ijumaa ijayo tutaingia katika Mwezi Mtukufu wa Ramadhan. Namuomba Mwenyezi Mungu atujaalie sote Ramadhan tuipokee, atupe nguvu za kufunga, tutekeleze wajibu wetu na mwakani na mwakani na mwakani. Vile vile nataka niseme hivi Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti, jana ilikuwa tarehe nne ndio siku niliyopeleka ombi langu la kuzungumza, nilikuwa nawaombaWaheshimiwa wenzangu, ndugu zangu mliomo ndani na wananchi wote kimoyo moyo tusome kulhuallahu tatu kwa kumkumbusha mwenzetu Dkt. Omar Ali Juma, ambaye alikuwa mwenzetu, kiongozi mwenzetu na Mwenyezi Mungu amsamehe madhambi yake na ampe kila la kheri ndani ya kaburi.

Mhe. Mwenyekiti, marehemu Dkt. Omar Ali Juma, alikuwa mwenzetu, sifa yake kubwa alikuwa si mkabila, mpenda watu na katumikia nchi hii katika nafasi mbalimbali na wote waliotangulia mbele ya haki Mwenyezi Mungu awape kila kheri.

Mhe. Mwenyekiti, leo tunazungumzia Wizara ya Katiba na Sheria, wengi wamezungumza uzito wa Wizara hii na majukumu ambayo Wizara hii wanayo, nisingependa nirudie sana yale waliyosema huku katika vyombo vya kusimamia haki Mahakama, Kadhi, Mwendesha Mashtaka, Mali na Amana, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu, hizi zote zote Wizara hii kwenye chombo hiki.

Na wote hawa wanafanya kazi ya haki na uadilifu, mengi yamesemwa, mengi wameambiwa, sasa sitapenda kurejea yale isipokuwa napenda kutoa nasaha kwao pamoja na Waziri anaesimamia mambo haya, naomba wote waliokabidhiwa dhamana hizi na Rais, Rais sio mas-ul, Rais kamteua Jaji Mkuu, kamuapisha na kaapa atatekeleza haki. Rais kamteua Mwendesha Mashtaka kaapa atafanya haki, Rais amemteua Kadhi na kaapa, Rais amemteua Mwanasheria Mkuu wote hawa wameapa kuwa watafanya haki na watatoa haki. Sasa watakapokwenda kinyume wajue Rais hana makosa wako ndio watajibu mbele ya Mwenyezi Mungu, kwa hivyo wachague kumtumikia Mwenyezi Mungu na haki au kutumikia dunia na mambo mengine.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nawashauri, leo tupige mstari wale wanaosemekana wanafanya maovu haya, maovu haya wawache, watimize haki. Nchi ambayo wananchi wake hawana haki hawana utulivu ni balaa tupu, sasa nimeona nisiende sana na nisiende mbali sana lakini wao wananisikia na watu wa dini. Lakini nilitaka tu kumnukuu Mhe. Ali Juma Shamuhuna, alitoa mada, mada yake ilikuwa nafasi ya viongozi wa dini katika kufanikisha muwafaka.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Shamuhuna alisema hivi. Dhana ya uadilifu kwa Waislamu, dhana ya uadilifu taqwa, anasema hebu tutizame dhana ya uadilifu jinsi inavyojenga imani miongoni mwa Waislamu na binaadamu hatimae huzaa matunda ya umoja na mshikamano. Dhana ya uadilifu imegawika katika maeneo makubwa mawili, kati ya mja na mola wake, kati ya mja na jamii anayoiongoza. Sasa Mheshimiwa kakumbusha na mimi nakumbusha, viongozi wa dini, viongozi wanaotoa haki wawe neno taqwa wamuogope mungu, sote tutakwenda kwa Mwenyezi Mungu, kwa hivyo Mungu tumuogope na leo Ijumaa ya leo tukitia nia njema basi Mwenyezi Mungu atakuwa na sisi, atatuongoza. Mimi nasema vyombo vyote vinavyoongoza sheria na haki wanatakiwa kutenda haki, haya si maneno yangu mimi ni maneno ya Mwenyezi Mungu na maneno haki, haki ni ngumu sana.

Mhe. Mwenyekiti, sasa ninakwenda katika mada nyengine ambayo ni Katiba na Sheria. Nataka nichukuwe nafasi hii kumpongeza kwa dhati Dkt. Ali Mohammed Shein, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na Makamo Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi kwa kutekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi, kwa vitendo na kwa nadharia. Dkt. Shein, huu ni mwaka wake wa tatu, ameapa kwa kuwa atatekeleza na ataisimamia na ataihifadhi Katiba ya Zanzibar na anaitekeleza, sasa nawaombaWajumbe wa Baraza hili ambao sote tumo ndani ya mfumo wa Umoja wa Kitaifa kwa Katiba hii kwa Ijumaa ya leo, tumpe kila mashirikiano, tuwe nae pamoja aweze kulipeleka jahazi hili mpaka hapo tufike salama na amani. Itakuwa ajabu Mawaziri hawa ambao ni wa umoja wa kitaifa na sisi tuko *back*

banchers tukawa hatumpi msaada, tumpe msaada wa haki na kweli kweli, kwa sababu yeye ni sehemu ya Baraza lako hili, sasa tusivunje maadili haya.

Mhe. Mwenyekiti, sasa nataka niende katika suala la Katiba na Sheria. Dkt. Shein, mwaka 2001 alikuwa Waziri wa Nchi, Katiba na Utawala Bora, ndio Wizara mpya iliyoundwa. Lakini Dkt. Shein alisema nini, Dkt. Shein wakati anapata Wizara hii na anakuja hapa Barazani alitoa muongozo ambao unasema hivi, alizungumza juu ya muungano na alisema:

"Mhe. Spika, kwa muda mrefu hivi sasa kumekuwa kuna matatizo au kutoeleweka hasa ni chombo gani ambacho kinasimamiwa na kuratibu shughuli za muungano wa Jamhuri ya Tanzania kwa upande wa Zanzibar. Hali hii ilijitokeza pale ambapo Taasisi mbali mbali zilitekeleza mambo ya muungano bila ya kuwa na chombo madhubuti cha pamoja cha kuratibu shughuli hizo.

Mhe. Spika, katika kuondoa kero hiyo na kuyaweka mambo katika muelekeo imara, Serikali imeanzisha Idara hii na kuleta utendaji mzuri baina ya Serikali zote mbili. Mhe. Spika, Idara ya Shughuli za Muungano pamoja na mambo mengine itakuwa na majukumu ya kutekeleza yafuatayo:- Kufanya kazi za SMT, kufuatilia shughuli zote za mashirikiano baina ya Wizara na Taasisi za SMZ kufuatilia masuala ya fedha za SMT itashughulikia. Mhe. Spika, katika kuleta ufanisi Serikali imeamua kuhamisha Idara hii katika Ofisi ya Waziri Kiongozi katika kipindi cha 2001 na 2002. Aidha utaratibu wa kutekeleza majukumu pamoja na malengo ya nchi yataratibiwa na Ofisi hii".

Sasa Mhe. Mwenyekiti, muda wote kabla ya hapo ilikuwa mambo yanakwenda lakini chini ya uongozi wake wa Serikali mambo ya muungano yalihamishiwa ofisi ya Waziri Kiongozi ndio anaratibu mpaka leo. Lakini Dkt. Shein, ni Rais, lakini anao uzoefu Wizara ya Katiba na Utawala Bora, akaona hapana madhali nimeshakuwa Rais niunde Wizara ya Katiba na Sheria, yote kupeleka mambo mbele kwa mara ya mwanzo katika historia ya Wizara hii, Wizara hii iliongozwa na Dkt. Shein, ambaye si mwanasheria, akaja Brigedia Mwakanjuki si mwanasheria, akaja Mhe. Diria si mwanasheria, akaja Mhe. Ali Juma Shamuhuna si mwanasheria, akaja Ramadhan Abdalla Shaaban akamaliza ngwe hii si mwanasheria. Leo Wizara hii inaongozwa na Mwanasheria Mhe. Abubakar.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Aboubakar ni mkongwe katika siasa, amekuwa ndani ya Baraza la Wawakilishi, Katibu wa Kwanza wa Baraza la Wawakilishi, anajua Baraza, amekuwa Mwanasheria Mkuu, amekuwa Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, amekuwa Jaji, amekuwa Waziri, lakini amekuwa mkereketwa

wa Chama cha Mapinduzi na Mjumbe wa *NEC* na vile vile amekuwa mkuu wa Upinzani wakati wa upinzani katika Baraza hili. Sasa Mhe. Abubakar si mgeni anaelewa. Lakini si hivyo tu anasaidiwa na Mwanasheria Mkuu ambaye ni mzoefu, DPP alikuwa ana uzoefu, sasa Dkt. Shein alifanya hivyo.

Mhe. Mwenyekiti, wakati wa Iddi Pandu alikuwa anafanya kazi zote. Sasa kuna Waziri wa Sheria nafikiri na Mwanasheria Mkuu, natumai na ninaomba wasaidiane kufanya kazi hizi kwa ufanizi. Mwanasheria Mkuu anatakiwa kama katiba inavyoeleza na Mhe. Aboubakar yeye ni Mwanasiasa wa kujibu masuala na kuweka mambo sawa kwa kushirikiana wao na sisi tutaipeleka jahazi hii salama wa usalimini.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, tuzungumze hii inayoitwa Katiba. Katiba ni utaratibu wa madaraka na mamlaka katika nchi. Katiba imeweka utaratibu na mfumo wa ukusanyaji kazi mihimili mitatu ambayo tunaijua sote, mmoja ni muhimili wetu huu wa hapa wa Baraza, tumekuwa na kelele nyingi sana, madai mengi sana tunashukuru Mungu Waziri wa Utumishi na Mhe. Rais, amekubali muhimili huu. Kwa niaba ya Wajumbe wa Baraza ninakushukuru sana na tutakuletea utie saini ili Baraza hili liwe kweli ngome ya wananchi. Mhe. Mwenyekiti, Katiba inatoa nafasi baina ya wananchi na wao nakuleta haki za binaadamu na usawa.

Mhe. Mwenyekiti, kihistoria ya Katiba tangu mwaka 1964 mpaka mwaka 1979 kulikuwa hakuna Katiba hakuna Baraza, shujaa wa nchi hii, Jamadari Mkuu Mhe. Aboud Jumbe Mwinyi ndie aliyeanzisha utaratibu wa kuwa na Baraza la Wawakilishi na utaratibu wa kuwa na Katiba, amefanya maendeleo mengine hatua kwa hatua. Sasa Katiba na Sheria lazima tuzifate na kuziheshimu, sisi sote humu ndani tumeapa kwa katiba na sheria na sote tumeshika qur-an tukufu, tuombe Mungu atusaidie. Mwenyezi Mungu anatushuhudia na naiambia nafsi yangu na nawaambia na wenzangu tuliapa tusiichezee Katiba itatudhuru. Kwa hivyo tuiheshimu Katiba na tuienzi Katiba.

Mhe. Mwenyekiti, nataka nimnukuu mtu mmoja amezungumza juu ya Katiba, anasema Katiba ya Zanzibar hii iliamuliwa kwenye Baraza hili mwezi wa Oktoba, naomba ninukuu.

"Mhe. Spika, Wajumbe wa Baraza lako tukufu watakumbuka kwamba tarehe 10/10/1984 walipitisha kwa kauli moja kwenye Katiba hii ukiisoma nyuma kuna kauli, anasema nina furaha uhusu Baraza lako tukufu kwamba Muswada wa Sheria wa kuanzisha Katiba hiyo iliizinishwa na Mhe. Raisi wa Zanzibar tarehe 1/12/1984 na kuwa sheria kamili Mhe. Rais, alitangaza kwamba Katiba hii itatumika rasmi tarehe 12/1/1985. Tamko la

Rais lilipokelewa kwa furaha na shangwe kubwa na Wananchi wa Zanzibar na Watanzania kwa jumla. Natumai Waheshimiwa Wajumbe wataungana na mimi katika kumshukuru na kumpongeza Rais kwa uamuzi wake wa busara kwa kuteua tarehe 12/01/1975 kuwa siku ya kuanza rasmi kutumika katiba ya Zanzibar. hakuna siku njema zaidi ya hiyo, yaani hiyo tarehe 12 January, kwa tarehe 12 January ni siku ya kihistoria, ni siku ambayo wananchi wataithamini sana kwa vile ni siku ambayo nchi yetu ilizaliwa upya na wananchi wake walipoanza kuvuta hewa ya uhuru wa kweli. Kutokana na ukweli huo ni jambo la kufaa sana kwamba mambo makubwa na yenye umuhimu na dhahiri kwa nchi yetu kwa siku hiyo"

Mhe. Mwenyekiti, hayo ni maneno aliyasema Waziri Kiongozi Maalim Seif Sharif Hamad. Kwa kuwa hakuna siku zaidi ya hiyo, sasa nimeona lazima tukumbushane historia wapi tumetoka, wapi tunakwenda. Sasa ninamuomba tarehe 12 January 2014 tutasherehekea miaka 50 hiyo siku tukufu. Tunasherehekea nini, tunasherehekea siku ambayo Wazanzibari, wanyonge, wakulima na wafanyakazi na watu wote wamepata pumzi za uhuru wao. Aliyasema hayo Waziri Kiongozi siku hiyo Mungu amuweke awe hai atafika uwanjani asherehekee na awaambie watu washerehekee akiwa Makamo wa Kwanza wa Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Na natumai atafanya hivyo.

Mhe. Mwenyekiti, sasa Mapinduzi, hatusherehekei Muungano, tunasherehekea Mapinduzi. Nataka niomba na nimnukuu, tunasherehekea nini, tunasherehekea siku ya mapinduzi ya miaka 50, miaka 50 kwa dunia ni miaka kidogo lakini kwa taifa ni miaka mingi sana. Mapinduzi yalifanyika na yakaletwa na Chama cha Afro Shirazi Party, ni Chama pekee katika Afrika ambacho kilifanya mapinduzi, mapinduzi mengi yamefanywa na jeshi, lakini hichi Chama kilifanya mapinduzi. Sasa Afrika ilikuwa kwenye ukombozi, leo Afrika vyama ambavyo vimeleta uhuru vilivyobakia ni Chama cha *ANC* South Afrika, *ZANU PF* Zimbabwe, *FRELIMO* Msumbiji, *NPLA* Angola, Namibia *SWAPO*, Lusotho ni Kingdom kuna Mfalme, Boswana kuna Mfalme na Zanzibar Chama cha Afro Shirazi kikiingia na *CCM* ndio kipo madarakani.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, nakuomba sana na hasa kwa kuturidhia sisi Wajumbe, nakuomba sana, watu wamerudia vyeti vya ndoa, vyeti vya kuzaliwa. Sasa ninataka niiombe Serikali katika kuadhimisha miaka 50 ya Mapinduzi, Taifa hili Dola ya Zanzibar na ninataka nimnukuu Dkt. Salmini Amour. Dkt. Salmini anasema hivi:-

"Ndugu Mwenyekiti, hali kama hii ya wasi wasi, wananchi wa Zanzibar kama wangependa wangeweza kufuata nasaha za Baba wa Taifa au Hayati Mzee Karume, naomba Serikali hii ya Mapinduzi katika siku ya kilele

imtangaze rasmi Baba wa Taifa hili ni Mzee Abeid Amani Karume, sio Amani ni Abeid Amani Karume".

Mhe. Mwenyekiti, hili alilitamka Kamandoo Dkt. Salmin, lakini kwa nini alitamka hivyo. Wewe ni Mjumbe wa CCU, kule utasikia mtu fulani anapewa PHD, fulani anapewa nini, imejengwa hoja hapa kwa nini apewe. Sasa kuna kila sababu za kujenga hoja kwa kuwa Mzee Karume anastahiki kabisa kabisa kuwa Baba wa Taifa hiyo rasmi kwa Taifa la Zanzibar au Dola la Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, Mzee Karume, ana maneno ya hekima, wamesema wenzake hapa kuhusu sheria, tufanye nini. Nitasema maneno ya hekima ya Mzee karume. Mzee Karume anasema"

"Epuka fitna za kidini katika kujenga Tanzania mpya, usikubali wewe kuwa katika kaumu ya ujinga usiwe katika kikundi cha wajinga, tukuza kilicho chako mpaka usahau cha mwenzako.

Furahia ulichonacho kuliko kufurahia cha mwenzako. Poteza maisha yako kwa kuokoa nchi yako. Fuata maelezo ya kiongozi wako"

Mhe. Mwenyekiti, nakuombeni tuyafate miongozo ya maneno ya Rais wetu Dkt. Mohammed Ali Shein, kama kweli wewe mfuasi wa Mzee Karume na unapenda mapinduzi, fuata hiyo. Inawezekana timiza wajibu wako, epuka kila fitna za kigeni isiingie nchi yako. Mzee Karume alipokuwa anahutumia maneno ya hekima alisema hivi.

"Mwanajeshi yoyote ninamuonea uchungu sawa sawa kama ninavyomuonea uchungu watoto wangu"

Maneno haya aliyasema tarehe 11/11/1971 katika mafunzo ya kijeshi yaliyofanywa katika kambi ya Unguja Ukuu, tumesoma hatukutambua, tumejifunza tumetambua. Mwanaadamu haifai kusahau msingi wake wa kujua kuwa anatoka wapi, tulianza wapi, tulipigea, majumba yetu kutiwa moto, vyakula vyetu viling'olewa kama migomba, mihongo, mpunga na kazalika ili tufe njaa kwa sababu ya kutaka haki yetu. Nyinyi wanajeshi mjue kwamba mmo katika ibada kubwa ya kulinda nchi yetu na haki zetu. Zamana ya mwanajeshi Salmin Awadh anajuwa ni kulinda nchi yako na kikomo cha uwezo wako wote na kuondoa kila fitna katika nchi yako pamoja na kutojali fitna za kidini wala ukabila.

Mhe. Mwenyekiti, Dkt. Mwinyihaji, Mhe. Waziri wa Utumishi, tumesema sana kuhusu vikosi vyetu watizame hawa kwa jicho la kheri kwa sababu hawa

wako ndani ya ibada. Sasa hizi ni hoja zinazojenga kwa nini Mzee Karume atangazwe kuwa Baba wa Taifa.

Mhe.Mwenyekiti: Mheshimiwa nimekupa dakika tano ya mwisho kumalizia.

Mhe. Ali Mzee Ali: Mwisho, afadhali tuwe na taifa ambalo halina silaha za kisasa lakini lina moyo wa ushujaa kuliko kuwa na taifa lenye silaha za kisasa lakini vijana wake ni waoga. Afadhali kuwa masikini lakini tunajitegemea kuliko kuwa matajiri kwa kuomba kutegemea taifa jengine.

Mhe. Mwenyekiti, leo niyaseme hayo nirudie tena sitaki niseme kwenye rasimu, lakini nafikiri hayo nimeona niyaseme na nayasema ndani ya moyo wangu.

Lakini niruhusu la mwisho niseme moja tu, kwa sababu nimesikia maneno mengi hapa yanasemwa. Dr. Salmin Amour anasema hivi, mnamo mwaka 1983 tulikuwa na marekebisho ya katiba, mwaka 1992 tulikuwa na Mfumo wa Vyama vingi vimeingia, iko haja Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria ya kupeana historia na elimu wengi ni wachanga ni wadogo historia tuijue. Sasa nini alisema: "Marekebisho ya katika Katiba ya Muungano yataweza kufanywa kwa ridhaa za pande zilizoungana kwa dhamiri ya kuimarisha na sio kubomoa Muungano". Nasema tena, "kwa ridhaa". Naungana na Mhe. Salmin Amour Juma na aliyoyasema 'kwa ridhaa'. Nimeona hilo niliseme kwa sababu lina uzito wake.

Sasa Mheshimiwa Tume ya Urasimu tunatakiwa tukatoe maoni yetu nawaomba wananchi wa Zanzibar tukatoe maoni yetu. Sisi maoni tumeshatoa mbele ya tume pale, mimi nimeshatoa, Mhe. Salmin na wengi washatoa, lakini wananchi wetu wakatoe maoni yao. Lakini la muhimu tujue sisi tuna jukumu la nchi hii na vizazi vyetu. Kwa sababu muda hujanipa Mapinduzi yana maneno yake.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa muda umekwisha tunataka kumaliza leo.

Mhe. Ali Mzee Ali: Haya sasa namaliza mama yetu, hapa ninayo hii *manifesto* ya mwisho, *manifesto* ya Afro Shirazi, kisome hiki hapa manaake karatasi yangu iko nyang'anyang'a ikabidi nii-*droo*. Uhuru wako, binafsi yako katika jamii neema na mapato kwa maisha yasio na wasiwasi, haki ya mfanyakazi kupata mshahara wa kumtosha, elimu bure mpaka chumba cha nane. Kwa nini tukasema hivyo, wakati huo 1955 elimu ya juu kwa mtu wa chini chumba cha saba, leo tunae pale kijana mmoja katiak mashekhe hawa ana *degree* ya Kizungu ya mambo ya ualimu, ana *degree* mambo ya dini, ana

masters mambo ya *public relation* na vyenginevyo. Leo tumesoma kina Mhe. Juma Duni wote hawa ni watoto waliofundishwa na Mapinduzi.

Kidumu Chama cha Mapinduzi,
Yadumu Mapinduzi.

Ahsante sana.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Mwenyekiti, kwanza napenda nikushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii ya kufanya majumuisho juu ya hoja yangu ambayo niliitoa jana. Lakini kabla sijafanya hivyo Mheshimiwa naomba kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia kuwa wazima na tokea jana tuko hapa tunajadili wizara yangu, tumefika wakati huu sote tukiwa wazima na tunataka kufanya majumuisho.

Lakini la pili naomba niwashukuru wachangiaji wote waliozungumza na walionileta kwa maandishi. Kwa kweli michangio yao imekuwa ni dira kwetu sisi ambayo dira hiyo itasaidia sana katika shughuli zetu za siku hadi siku.

Mhe. Mwenyekiti, kuna wachangiaji 21 ambao wamechangia hotuba yetu na kama ilivyo kawaida yetu naomba niwataje:

1. Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala ambayo iliwasilishwa na Mhe. Wanu Hafidh Ameir (Kny. Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala)
2. Mhe. Makame Mshimba Mbarouk
3. Mhe. Ismail Jussa Ladhu
4. Mhe. Abdalla Juma Abdalla
5. Mhe. Farida Amour Mohamed
6. Mhe. Mbwana Hamad
7. Mhe. Mohamed Haji Khalid
8. Mhe. Salmin Awadh Salmin
9. Mhe. Ashura Sharif Ali
10. Mhe. Salim Abdalla Hamad
11. Mhe. Mbarouk Wadi Mussa
12. Mhe. Salma Mohamed Ali
13. Mhe. Hassan Hamad
14. Mhe. Omar Ali shehe
15. Mhe. Jaku Hashim Ayoub
16. Mhe. Saleh Nassor Juma
17. Mhe. Rufai Said Rufai
18. Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi

19. Mhe. Hija Hassan Hija
20. Mhe. Mwanasheria Mkuu
21. Mhe. Ali Mzee Ali.

Waliochangia kwa maandishi ni Waheshimiwa watatu ambao ni:

1. Mhe. Hamza Hassan Juma
2. Mhe. Mahmoud Muhammed Mahmoud
3. Mhe. Subeit Khamis Faki

Wote kwa pamoja naomba niwashukuru sana kwa dhati kabisa kwa michango yao mizuri, michango ambayo itanisaidia sana mimi na watendaji wangu katika kuendeleza shughuli yetu hii.

Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu michango ni mingi lakini michango yenyewe kwa kweli imegawika katika sehemu sita na naomba nizizungumze hizi sehemu sita zilizogawika ambazo kila sehemu hiyo wachangiaji wote niliowataja takriban wamegusia.

Sehemu yenyewe ni suala la Mahkama, suala la Wakfu, suala la Vizazi na Vifo, suala la Mufti, suala la Maslahi ya Wanasheria na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu. Mhe. Mwenyekiti, katika mambo haya yote naomba niseme tu kwamba wachangiaji wote walionesha dosari, wakatoa maelekezo na wakatoa pengine wasiwasi wao katika kutizama na kufuatilia. Kwa kweli mengi tunaweza kuyapatia ufumbuzi na tukaendelea katika ujenzi wetu wa taifa.

Mhe. Mwenyekiti, katika suala la Mahkama kama nilivyosema Mhe. Makame Mshimba, Mhe. Ismail Jussa, Mhe. Abdalla Juma Abdalla, Mhe. Farida Amour, Mhe. Mohamed Mbwana, Mhe. Mohamed Haji Khalid, Mhe. Salmin Awadh, Mhe. Ashura Sharif Ali, Mhe. Salim Abdalla Hamad, Mhe. Mbarouk Wadi, Mhe. Salma Mohammed Ali wote walichangia kuhusu suala hili la Mahkama. Katika michango yao suala kubwa lilikuja mwanzo la suala la pesa hizi shilingi 150 milioni. Je, pesa hizi zote ni kwa jengo la Mahkama Kuu au ni kwa utaratibu gani?

Fedha hizi shilingi 150 milioni zimegawika katika sehemu tatu, kwanza ni ujenzi wa Mahkama za Mwanakwerekwe, Mahkama za Kadhi; shilingi 70 milioni ni ujenzi wa Mahkama iliyoko Makunduchi sote tunajua kwamba Makunduchi jengo lake si zuri na linahitaji ukarabati mkubwa na shilingi 50 milioni ni Mahkama Kuu ya Chake Chake. Naamini kwamba fedha hizi pengine zitakuwa hazitoshi lakini hiki ni cha kuanzia na Inshaallah kila

tukienda tunaweza tukapata fedha za kuongezea ili kuweza kukamilisha ujenzi huu. Na fedha hizi hazihusiani na ujenzi wa Mahkama Kuu ya Zanzibar. Hivi karibuni tumepata pesa ambazo hizo ndizo tunazozitumia kwa Mahkama Kuu ya Zanzibar.

Suala jengine ambalo limezungumzwa sana ni suala la mishahara, hasa ya Mahakimu wa Mwanzo. Suala hili kama mnavyojua Mhe. Mwenyekiti, kwamba lilikuja katika mijadala mingi na tulisema kwamba tunalifanyia kazi. Napenda niwahakikishie kwamba suala hili tumeshalifanyia kazi, kitu kilichojitokeza hapa na hili alilizungumza sana Mhe. Hamza Hassan katika maandishi yake ambayo alinileta.

Kitu kilichojitokeza ni kwamba mshahara wa Hakimu wa mwanzo ukilinganisha na mshahara wa Hakimu wa Mahkama ya Wilaya kuna tofauti kubwa kidogo. Hii ni kwa sababu kama tutakumbuka mazungumzo aliyozungumza Mhe. Mwanasheria Mkuu alisema kwamba kuna nafasi nyengine ambazo zile ni za uteuzi na katika nafasi hizo mishahara yake lazima iwe inalingana na uteuzi huo. Sasa ukitizama Mahkama ya mwanzo na wakati ule ambao tulikuwa tunaongeza mishahara ya wafanyakazi wote, Mahkama ya mwanzo kwa kweli hawakupata nyongeza, au kama walipata basi ilikuwa ni kidogo sana. Na hii ni kwa sababu wengi katika Mahkama za Mwanzo walikuwa wana *certificate in law*, kwa mujibu wa utaratibu ambao umewekwa hii ilikuwa hailingani na yule ambaye ana *degree* ambao wengi ni Mahakimu wa Mahkama za wilaya na kuendelea.

Kwa hivyo, tulipoona hivyo tukajaribu kuwaongeza hawa Mahakimu wa Mahkama ya Mwanzo. Lakini kwa mujibu wa utaratibu ambao umewekwa kiutumishi haikuwezekana kuongeza mshahara moja kwa moja. Kwa hivyo sisi tulichofanya ni kuwaongeza maposho na hayo maposho tukaongeza na ikawasaidia katika maisha. Najua wengi wao kidogo waliona kwamba hawakufanyiwa haki kwa sababu kile ambacho walikuwa wanakitaka ilikuwa ni kuongezwa kwa mshahara. Sasa kwa sababu hiyo, ilitubidi tuharakishe kufanya *scheme of service*, tukifanya *scheme of service* na tukawaweka wale Mahakimu katika ngazi hizo basi kidogo kila mtu atajua kwamba utaratibu wake ni huu na yeye mwenyewe atalazimika kujiendeleza ili aweze kuingia katika *scheme of service*.

Mhe. Mwenyekiti, ukitizama katiba inasema kwamba, ili mtu ateuliwe kuwa Jaji wa Mahkama Kuu angalau awe ni mwanasheria mwenye *degree* na awe ameshungulikia katika shughuli hizo za sheria kwa kipindi kisichopungua miaka saba. Hiyo ndio *qualification* ya kuwa Jaji wa Mahkama Kuu. Kwa hivyo, tulichosema ni kwamba kwanza, kwa mujibu wa *scheme of service* mpya ambayo tumeshaiandika, tumeshaiwasilisha Utumishi ni kwamba

Mahakimu wa Mwanzo sasa hawatakuwa tena Mahakimu wenye vyetu, ni lazima Hakimu yule awe ana *degree*.

Hii Mhe. Mwenyekiti, ni kuwafanya kwamba wale Mahakimu tunawaomba wajiendeleze, sasa ukishakuingia pale una *degree* unakuwa ni Hakimu wa Mwanzo ambapo katika *scheme of service* yako utakuwepo ule mshahara wako, pale kwa mujibu wa *scheme of service* utafanya kazi kwa miaka mitatu. Ukifanya kwa miaka mitatu pale wewe una uwezo au inawezekana kupandishwa daraja ukawa Hakimu wa Wilaya, lakini *subject* tu nidhamu yako katika kazi iwe ni nzuri, huna *record* mbaya ya kuchukua rushwa na kufanya mambo kama hayo yaani *professional ethics* zako ziwe ni nzuri. Kwa hivyo, kwa miaka mitatu ukipanda ukiwa Hakimu wa Wilaya na ukakaa tena miaka mitatu ukapanda ukawa Hakimu wa Mkoa hiyo ni miaka sita, sasa ukikaa tena miaka mitatu katika Hakimu wa Mkoa wewe moja kwa moja utakuwa una-*qualify* kuwa ni jaji na utakuwa umeshakuwa una *experience* ya miaka tisa. Kwa hivyo, hiyo ndio *scheme of service* ya hivi sasa.

Kwa hivyo, ombi langu ni kwamba hasa kwa Mahakimu wa Mwanzo ni lazima wajitahidi, wale wenye vyeti wajaribu kusoma, wajiendeleze ili waingie katika mfumo huu mpya ambao utasaidia sana. Hayo matatizo yote ambayo yalikuwepo hapo mwanzo yatakuwa yamefutika moja kwa moja. Huo ndio utaratibu ambao tumeufanya na tuliwaita tukazungumza nao na naamini kwamba walikubaliana na mimi au na wizara yetu. Sasa utaratibu huu ndio tunaotumia hivi sasa na tumeshaupeleka katika Idara ya Utumishi ili waweze kutupa Baraka zao na tuendelee katika *scheme of service* hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, suala la pili lililozungumzwa katika Mahkama ni suala la rushwa Mahakamani. Mimi sitosema kwamba Mahakamani hakuna rushwa, nakubaliana moja kwa moja na Waheshimiwa Wajumbe kwamba rushwa ipo. Lakini sasa tatizo hili hatuwezi kuwalaumu Mahakimu peke yao, kwa sababu rushwa si suala la kutoa pesa tu, kuna rushwa nyingi hata wewe mkubwa ukienda kwa Hakimu ukimtisha na hiyo ni rushwa na hiyo tunafanya. Wakubwa wengi wanakwenda wanawatisha Mahakimu kwamba lazima waamue kesi hii katika ule utaratibu ambao wanautaka, masikini ya Mungu Hakimu anataka aendelee na kazi ataamua kinyume na utaratibu, kinyume na sheria lakini kutokana na rushwa aliyoifanya mkubwa. Sasa hiyo ni njia moja ya rushwa Mahakamani.

Lakini njia ya pili ni kweli hata kama kuna harufu ya rushwa ndogo ndogo baadhi yetu, lakini sisi raia tuna matatizo nasi, kwa sababu ukienda kwa Hakimu hata hajakwambia chochote utamlazimisha Hakimu yule, utamwambia hii zawadi yako, unatoka shamba una kesi yako unamchukulia

mayai ya kuku 20 unampa. Sasa ile ni rushwa na ile unamlazimisha hakimu atoke katika maadili.

Jengine Mhe. Mwenyekiti, ni kwamba hata kama Hakimu atachukua rushwa na wewe ukaja ukalalamika, wameshakuja watu kutulalamikia na tukawaambia basi sisi tuko tayari kuchukua hatua kwa hakimu huyu lakini na wewe tutakwita. Anasema aa, mimi sitaki tumuachie Mungu tu, sasa kama hutaki usije ukatwambia. Kwa sababu haiwezekani lazima kama tunamfikiria Hakimu fulani kachukua rushwa na wewe ndiye uliyetoa basi uwe mstari wa mbele kwa kusema kweli nilikupa, lakini ukisema tu kwamba kuna Hakimu kala rushwa mimi siamini na hivyo nitasema mnawaonea Mahakimu wangu bure. Kwa sababu hamtupi ushahidi, tupeni ushahidi ili tuweze kuchukua hatua, lakini kama mtasema tu hamtoi ushahidi mimi sikubaliani na nyinyi hata kidogo.

Kwa hivyo, ninachoomba Waheshimiwa na wananchi kwa ujumla suala hili la rushwa kweli ni suala baya, sisemi kama halipo Mahkamani lakini na sisi sote tunawajibika juu ya kupiga vita rushwa. Kwa hivyo, tunawajibika katika misingi mbali mbali tukifanya hivyo naamini tunaweza tukafika pahala pakubwa sana.

Lakini mbali na hayo, namshukuru sana Mhe. Jaji Mkuu mara nyingi takriban mara zote tunakaa pamoja tunazungumza namna gani ya kutatua matatizo haya. Na mtaona kama mmefuatilia kwamba kuna hatua ambazo tumechukua, sasa hatuwezi kuchukua hatua zote kwa mara moja lazima uchukue kidogo kidogo utizame utaratibu na hiyo namshukuru Mhe. Jaji Mkuu ni mtu msikivu tunakaa pamoja na tunakubaliana. Tumeshafanya hatua hizo na tumeanza kuzichukua, kuna wengine tumewahamisha, hivi karibuni Mhe. Rais ameteuwa mwenyekiti mpya wa Mahkama ya Ardhi na mambo kama hayo.

Kwa hivyo, mimi nakubali upande mmoja, lakini upande mmoja sikubaliani kwa sababu hamtwambii hasa, ushahidi hamtupi. Kwa hivyo, kama hamtupi ushahidi tutakuwa hatuna kitu cha kukamata ili kuweza kuwadhibiti wale ambao wanaleta matatizo hayo. Lakini ninachopenda kuwahakikishieni kwamba tutaendelea kupigana katika vita hivi na kwa ushirikiano wenu naamini tutafaulu. Hivyo nawaombeni sana ushirikiano katika masuala haya.

Mhe. Mwenyekiti, suala jengine lililozungumzwa katika suala la Mahkama ni Jaji Mkaazi Pemba. Suala hili mimi mwenyewe ndio muanzilishi, nakumbuka wakati niko mwakilishi wa kawaida nilikwenda hata nikatoa nyumba yangu ya Pemba kusema kwamba tutampa jaji akakae kule kwa sababu ya umuhimu wa suala hili. Lakini bahati nzuri Mwenyezi Mungu akanipa hii shughuli na mimi kitu kimoja nilipofika tu nikasema sasa lazima Jaji Mkaazi Pemba

atakwenda tukijaaliwa, maana yake alipokuwepo Mhe. Ramadhan Abdalla Shabani nimemwambia hakutaka, sasa lakini kuna matatizo na mimi baada ya kuambiwa na wenzangu tukakubaliana. Kwa sababu Jaji Mkaazi Pemba ni Jaji wa Mahkama Kuu, Jaji wa Mahkama Kuu huwezi ukamuweka katika kituo ambacho pengine kwa mwaka mzima atasikiliza kesi tano au kumi, itakuwa ni *wastage* ya *main power* tokea hapo hatuna halafu tukamchukua yule tukamuweka kule. Lakini tulichofanya ni kuhakikisha kwamba kila mwezi lazima Jaji wa Mahkama Kuu aende Pemba na hiyo inafanyika mpaka hivi sasa.

Sasa mimi napenda kuwaambia kwamba hivi sasa hakuna kesi *pending* ambazo zinahitaji uamuzi wa Jaji wa Mahkama Kuu labda iwe Jaji amekwenda kesi yake ameiakhirisha itakuwa kama hivyo, lakini hakuna kesi ambazo hazijasikilizwa na Mahkama Kuu. Hilo ni la kwanza.

Lakini la pili kuna mambo mengine ambayo yanaweza yakatokea katika Mahkama ikabidi lazima umpate au upate uamuzi wa Jaji wa Mahkama Kuu. Sasa hapo kuna kitu kinachoitwa *extended jurisdiction*, yaani ni dhamana ambayo amepewa yule hakimu mdogo kidogo sio Jaji wa Mahkama Kuu na yule anaweza akafanya baadhi ya mambo ambayo Jaji wa Mahkama Kuu anaweza akayafanya. Kwa hivyo, likitokea hilo kuna mrajis kwa mfano wa Mahkama Kuu aliyeko kanda ya Pemba anaweza akawa na *extended jurisdiction* akalishughulikia lile jambo, lakini kama jambo litahitaji lazima kuwe na Jaji wa Mahkama Kuu basi jaji anakwenda kila mwisho wa mwezi. Kwa hivyo, hivi sasa mimi binafsi nimekuwa *convinced*, nimeridhika kabisa kwamba hakuna haja ya kumuweka Jaji wa Mahkama Kuu kwa hivi sasa hasa kwa sababu majaji wanakwenda na utaratibu huu umewekwa na hivi sasa hakuna *complains* zozote zile ambazo tumezipata.

Mhe. Mwenyekiti, suala jengine ambalo lilizungumzwa ni suala zima la Mahkama ya Rufaa, kwa nini Mahkama ya Rufaa inakuja hapa mara moja tu. Mahkama ya Rufaa iko Tanzania na wale siku zote wanatoa utaratibu wao, ratiba yao na wanazunguka kwa Tanzania nzima. Bahati nzuri hapa Zanzibar wanaweka kila mwaka mara moja, lakini sisi Zanzibar pia tumepata *advantage* nyengine kwamba kama kuna kesi hapa basi tunaweza tukaenda Dar es Salaam kwa hivyo pia tunatumia kituo cha Dar es Salaam kama itatokea kesi hiyo.

Kwa hivyo, mpaka hivi sasa nawahakikishieni kwamba hakuna kesi ambazo zina matatizo kwamba hazijapata kusikilizwa na Mahkama ya Rufaa na kitu kama hicho. Napenda niseme tu kwamba, kwa mwaka *almost* ni kesi tano tu za *criminal* na kesi karibu kumi za *civil* ambazo zinasikilizwa na Mahkama ya Rufaa, na kesi hizi wakija mara moja basi wanaweza wakazimaliza zote. Kwa

hivyo, hii kuwepo kwa ratiba moja haina maana kwamba pengine watu hawapati haki au utaratibu huo. Nafikiri haki inatendeka, kesi zinamalizika zote na kama kutatokea haja basi watu wetu hapa wanao uwezo kisheria wa kwenda katika Mahkama ya Rufaa Dar es Salaam.

Mhe. Mwenyekiti, suala la pili ambalo limezungumzwa ni suala la Wakfu. Nakubaliana sana na Mhe. Ismail Jussa aliposema kwamba suala la bei za nyumba za wakfu lazima tutilie maanani uwezo wa wananchi, lakini pia tutizame kwamba bei au maisha sasa yamepanda hata vifaa vimepanda, kwa hivyo unapokuwa katika nyumba ya wakfu na ikaharibika basi bei yake ya kutengeneza mwaka juzi sio mwaka wa leo. Sasa wakati sisi tunatizama wale wapangaji uwezo wao lakini pia na wapangaji watizame maisha na hasa bei za vifaa ambazo zipo.

Lakini suala jengine ambalo lilizungumzwa ni suala la Michenzani. Mhe. Mwenyekiti, suala la Michenzani nyumba za fidia ni 20 ambazo tulipata, nyumba nne wenyewe walikuwa ni hai wakakabidhiwa na Idara ya Nyumba, nyumba kumi na moja zimekabidhiwa Kamisheni zikiwa na wapangaji wake, nyumba tano bado zina utata na suala limepelekwa kwa Katibu Mkuu wa Ardhi kwa kupatiwa muongozo. Kwa hivyo, hivi sasa tunachobishaniana ni nyumba tano tu ambazo naamini tunaweza tukapata ufumbuzi hivi karibuni..

Mhe. Mwenyekiti, katika nyumba hiyo hiyo ya tano ina utata mwengine, kwa sababu sisi Wizara ya Katiba na Sheria tulikuwa na tatizo la nyumba ya kuwaweka baadhi ya watu wetu ambao ni muhimu. Kwa hivyo, nyumba moja Mhe. Rais mwenyewe akatupa kama ni nyumba ya Wizara ya Katiba na Sheria, kama likitokea tatizo kama hilo. Ikatokea bahati mbaya kwamba ile nyumba ambayo tumepewa Wizara ya Katiba na Sheria ndio hiyo hiyo nyumba ambayo Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati walitupa kama ni nyumba ya fidia. Sasa sisi tukawaambia aah! hii ni nyumba ambayo sisi tumekabidhiwa rasmi na Mhe. Rais kwa shughuli zetu. Kwa hivyo, kuna tofauti ya nyumba moja, lakini hiyo naamini tumeshapeleka barua wizara ya ardhi na majenzi naamini tutakubaliana tu hakuna matatizo. Kwa hivyo, hiyo ndio hadithi yote ya hizi nyumba za wakfu, kwa hivyo hakuna tatizo kama linavyoonekana kwamba pengine nyumba za wakfu zile hatujapewa hapana. Nyumba tumekabidhiwa na bado nne na hiyo moja tunazungumza na *Inshaallah* mambo yatakuwa mazuri.

Suala jengine ambalo lilizungumzwa ni suala la zaka. Mhe. Mwenyekiti, zaka ni suala la dini ya Kiislamu, naamini Sheikh Mohamed aliyezungumza pale anajua kwamba zaka kuna mambo 8 ambayo yanatakiwa katika utoaji wa zaka.

1. Ni suala la mafukara ambao ni wale wasiopata hata nusu ya mahitajio yao, hayo ndio masharti ya mwanzo.

2. Ni suala la maskini wale wasiokamilisha matumizi yao.

3. Wanaofanya kazi ya kukusanya na kugawa zaka, pia na wao wanatakiwa wapate hiyo zaka.

4. Watu walioingia katika Uislamu na wao wanatakiwa wapewe zaka.

5. Watu ambao wanaingia katika Istihali ya kukombolewa katika utumwa. Hii katika dini ina maana pana, wanaokombolewa katika utumwa. Hivi sasa Unguja hakuna tena utumwa ule tunaoukumbuka. Lakini Unguja kuna utumwa mkubwa hivi sasa, utumwa wa dawa za kulevya. Mtu utamuona hali yake basi utamsikitikia, sasa ukimkomboa yule katika ule utumwa alionao, mimi nafikiri kidini Sheikh Mohamed atakubaliana na mimi kwamba inakubaliwa kumpa zaka, ili aendeleze maisha yake vizuri.

6. Watu wenye madeni ambayo hawawezi kuyalipa .

7. Mambo ya Kidini anayoyaridhia Mwenyezi Mungu Mtukufu.

8. Ni msafiri aliyekatikiwa na safari kwa kuharibikiwa na mambo yake. Kwa mfano, vipando na vitu kama hivyo.

Kwa hivyo, hayo ndio mambo muhimu ambayo yanatakiwa kwenye utoaji wa zaka. Sasa katika misingi hiyo ofisi yetu ya wakfu imetizama misingi hiyo na ikaweza kugawa masuala hayo ya zaka kwa vikundi hivi. Unaposema kwamba hatukuzingatia hayo. Mimi sikubaliani na Mhe. Mjumbe kwa sababu wakati tunatoa hayo tulifanya mambo mawili makubwa. Kwanza tulitaka vikundi katika kila jimbo. Vikundi vile kwa vyovyote ni vikundi vya watu maskini na ukivisaidia vile maana yake unapunguza umaskini wao. Kwa hivyo, hiyo ndio iliuyosababisha tukapita katika kila jimbo na tukawapa vikundi ambavyo vimeorodheshwa na vikundi hivyo hatukuvitoa tu. Watu wetu walikwenda wakavitizama na kuvigatua kama kweli vinastahiki kupewa zaka na vikundi hivyo ni kwenye majimbo yote pamoja na Jimbo la Micheweni. Kwa hivyo, ukisema kwamba na Micheweni nao hawakupata. Sio kweli. Micheweni kuna vikundi ambavyo walipewa ili kusaidia katika maisha yao hayo. Kwa hivyo, hilo ni suala la zaka Mhe. Mwenyekiti.

Suala jengine ambalo lilizungumzwa ni suala la mahujaji na hili alilizungumza sana Mhe. Salmin Awadh Salmin. Katika kitabu chetu hiki

kwenye ukurasa wa 68 tulisema hapa kuna vikundi viliwasafirisha mahujaji mwaka 2012 na hapa kuna vikundi 11, hivi ndio vikundi ambavyo tunavitambua na hivi ndio vilivyokuwa vimesajiliwa. Kwa hivyo, kama kuna watu ambao wamepata matatizo katika vikundi hivi, basi mimi nitaweza kujibu, kwa sababu vikundi hivi ndivyo vilivyokuwa vimesajiliwa na hivi ndio vikundi ambavyo vinashughulikiwa na Idara yetu ya Wakfu na Mali ya Amana. Vikundi vyengine sivitambui lakini vipo.

Kuna kikundi Mhe. Mwenyekiti, kinaitwa ZADEO. Hii ZADEO kuna mtu anaitwa Al Hajj, kama ni Al Hajj wa kweli maana yake ni mwizi, anaitwa Al Hajj Ameir Haji katika nyakati za mwisho hizo. Huyu Al Hajj Ameir Haji, jina jengine anaitwa Mpakia. Huyu ni tapeli na hausiki na vikundi vyetu na ninawaomba wale wote waliotapeliwa, kwa sababu sisi hawajatutaarifu rasmi, waliokwenda wakamuambia rasmi ni mwakilishi wao. Lakini nawaomba wote waliotapeliwa waje watupe taarifa ili tuweze kumshtaki huyu, kwa sababu hajapewa *authority* yoyote ya kupeleka watu Hijja. Anakusanya yeye mwenyewe pesa, anawaambia atawapeleka Hijja halafu pesa anazila na yeye anaitwa Al Hajj. Kwa hivyo, watu wa aina hii wapo na hao watu ambao aliwasema Mhe Salmin Awadh wanatoka katika mkondo huu, ni fedha ambazo zilikusanywa na huyu Mpakia.

Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, ninachosema ni kwamba Mpakia si mtu mzuri na atakapokuja safari hii waheshimiwa wananchi msimpeni pesa zenu, hajasajiliwa kisheria. Ninawaombeni sana Mtu anayeitwa Mpakia akijakukusanya pesa za Hijja msimpeni na wale wote wenye malalamiko nawaomba sana watuletee malalamiko hayo sisi tutachukua hatua za kumshitaki. Maana yake Mhe. Mwenyekiti, huyu Mpakia alifika hadi kukusanya kwa kila mtu alimwambia atowe dola 575 kwa sababu zinatakiwa *advance*. Baada ya kuzipata hizo akenda kwenye baadhi ya mashirika akawaambia kwamba ana watu wake anataka wasafirishwe, lakini yale mashirika mengine yalikuwa yameshajaa, baada ya kukosa nafasi ndio akawatapeli hawa mahujaji. Kwa hivyo, hayo ndio matatizo ya mtu huyu anayeitwa Mpakia.

Mhe. Mwenyekiti, narudia tena kwamba Mpakia sio mtu mzuri, Mpakia ni mwizi kwa misingi hii na itabidi wale wote ambao walipata matatizo hayo tunaomba watuone ili tuchukuwe hatua hizo.

Mhe. Mwenyekiti, sio Mpakia tu

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, tumsikilize Mhe. Waziri.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Mwenyekiti, sio Mpakia tu ambaye ana matatizo haya, naomba nichukuwe nafasi hii kuwafahamisha Wazanzibari wote, kwamba kuna vikundi vyenye mikasa kama hivi. Hivi sasa kuna kikundi ambavyo kinaitwa Al Madrassa tu Fii Sabilillah Zanzibar. Kikundi hiki kina matatizo hivyo hivyo ni majambazi. Kikundi hiki kina matatizo, maana yake yeye anapita kila pahala akiomba pesa za kufanyia itikafu na anampelekea kila mtu anayemjua, anapeleka Balozi zote anataka dola 15 au pengine dola 5,000 za kufanyia Itikafu na pesa zile hazina hesabu yoyote zikija, hiyo itikafu itafanywa siku mbili au tatu, pesa nyengine zote zinakwenda katika tumbo. Nilipata habari hii na hivi sasa naifuatilia kwa kina, nimewataka hao watu wanaohusika na NGOs tutizame NGOs yake na tutaifunga tukijaaliwa. Najua litatoka zogo kwa sababu hawa wanataka kukaa itikafu tunawafungia tutaambiwa sio Waislamu na kadhalika, lakini hayo hatutoyajali sisi. Ikiwa amekwenda kinyume na utaratibu, basi nawahakikishieni kwamba na huyu tutamfungia. Kwa hivyo, hili ndio suala la mahujaji suala la Mhe. Salmin Awadh kwamba hiki kikundi sio chetu, kikundi hiki ni cha mtu huyu ambapo hakusajiliwa na huyu kweli alichukua pesa za watu na hajazirejesha. Kwa hivyo, mtu anayechukua pesa za watu hajazirejesha ni mtu ambaye anastahiki kushtakiwa.

Mhe. Mwenyekiti, suala jengine ambalo lilizungumzwa ni suala la vizazi na vifo, lilizungumzwa karibu na wajumbe wote. Nawashukuru wajumbe wote Mhe. Makame Mshimba Mbarouk, Mhe. Wanu Hafidh Ameir, Mhe. Ismail Jussa Ladhu, Mhe. Abdalla Juma Abdalla, Mhe. Farida Amour Mohamed, Mhe. Mohamed Mbwana Hamad, Mhe. Mohamed Haji Khalid, Mhe. Salmin Awadh Salmin, Mhe. Ashura Sharif Ali, Mhe. Salim Abdalla Hamad, Mhe. Salma Mohamed Ali na wajumbe wengineo, wote walizungumzia suala la vizazi na vifo.

Mhe. Mwenyekiti, matatizo yaliopo katika vizazi na vifo. Mhe. Mwenyekiti, tunayo matatizo katika idara hii, lakini matatizo haya sio yote yakwetu wizarani. Sisi ni binadamu wizara inaweza kuwa na matatizo yake, lakini kila tukipata changamoto hizi basi sisi tunafurahi kwa sababu ni changamoto hizi ambazo zinatufanya sisi tuweze kujirekebisha.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, utoaji wa vyeti kuna aina mbili. Kuna vyeti ambavyo tunatoa sisi moja kwa moja na hivi ni pamoja na *late registration*, lakini kuna vyeti ambavyo hivi sasa wanatoa mawilayani. Hawa mawilayani ndio wenye matatizo kidogo, kwa sababu utakwenda wilayani utataka cheti usipopata utaona kwamba ni wizara yetu. Nakubali kwa sababu sisi ndio *responsibility*. Matatizo ya wilayani yako vipi.

Mhe. Mwenyekiti, mtu anapozaliwa wilayani. Kwa mfano, Wilaya ya Micheweni yupo sehemu ya Kinyasini, sasa pale akishakujifungua ama baba au mama atamwambia Sheha na Sheha ataandika kile cheti chake. Sasa matatizo tuliyokuwa nayo sisi wananchi ni kwamba mimi nitampa pesa Sheha ili aende wilayani akaniandikishie, nikimpa shilingi 3,000, Sheha leo hendi wilayani, kesho hendi na keshokutwa atapata mtu mwengine atajifungua hendi zitakuwa shilingi 6,000 hizo na mwengine shilingi 9,000. Wakitokea pono atanunua atapeleka kwa mama. Sasa ukenda wilayani, wilaya watakuambia cheti chako bado kitakaa. Sasa kuzipata zile shilingi 9,000 za pono kuzirudisha inachukua pengine mwaka. Hiyo tumeshaikuta na hata pale Wilaya ya Kati, Sheha alikuwa anadaiwa nafikiri ni nyingi tu, kwa hivyo ukenda wilayani cheti hakipo unailaumu wilaya na Sheha anakuambia bado. Hilo ni tatizo moja.

Lakini tatizo la pili kule kule wilayani akishakupeleka Sheha, yule mwandikishaji kule wa wilaya si mtu wengi wa kudumu ni mtu wa wilaya. Lakini leo itakuja shughuli fulani, Mkuu wa Wilaya atamchukua yule yule atampeleka kwenye shughuli ile. Kwa mfano wamekuja watu wa malaria, kwa hivyo hakuna mpiga chapa pale, atamchukua sekretari yule anayetoa vyeti atakwenda kwenye malaria, kama malaria yale ni mwezi mmoja basi mwezi wote atakuwepo kule, ukenda kule bado. Kwa hivyo, hilo ni tatizo jengine.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo kuna ule urasimu wa kutiwa sahihi nayo ni matatizo. Kwa hivyo, matatizo hayo yako ya aina hiyo wilayani. Lakini na kwetu ofisini nako kuna matatizo, hayo matatizo yaliopo tunajitahidi kuyarekebisha ili sote kwa pamoja tuweze kupata hiki cheti ambacho ni haki ya kila mtu.

Mhe. Mwenyekiti, hapa lilikuja suala zima la Mhe. Salma Mohamed ambaye alisema kwamba yeye alikwenda wilayani kuandikisha ZID, alipokwenda wilayani kupeleka kile cheti chake, akaambiwa kile cheti chake ni *fake*. Ni kweli aliambiwa hivyo na mimi alinipigia simu nikamwambia fanya vyovyote hicho cheti uniletee. Cheti hicho akakileta nikakipokea na nikampelekea mrajisi wa vizazi na vifo. Nafikiri nilimuita ofisini nikamwambia hebu kitizame hiki cheti cha mheshimiwa ni *fake*. Akakichukua akenda kukitizama kwenye mafaili yote na ma-*register* yote, akaniambia mheshimiwa hiki sio *fake*. Basi mimi nikampigia simu Mhe. Salma Mohamed nikamwambia hiki cheti chako sio *fake* nenda, akaenda. Alipokwenda wale watoto wakazidi wakamwambia hiki cheti ni *fake*. Mhe. Salma pale pale akanipigia simu mbele ya hao watoto. Mimi nikamwambia hicho cheti tumeki-*verify* sio *fake*. Aaah! mheshimiwa hicho cheti ni *fake*, sisi tumepewa majina ya kutizama. Nikawaambia, sasa mimi ndio waziri nasema hicho sio *fake*, tumesha-*verify*

na Mkurugenzi wangu amesha-*verify* sio *fake*. Lakini bahati mbaya yule kijana kwa ujinga tu hakutaka kusikiliza chochote, akasema hiki ni *fake* na wala hatoi.

Sasa mimi nafikiri tukifika hapo, na wale watoto wakamwambia Mhe. Salma Mohamed kwamba wamepewa *signature* ambazo ndio wanazozitizama kama cheti ni *fake* au sio *fake*. Alinilete Mhe. Salma Mohamed na mimi ninayo hapa. *signature* hizi ni mbili, kuna *signature* ya Mgonja na *signature* ya mtu anayeitwa Mohamed. Mgonja ameshastaafu kazi huu ni mwaka wa nne na Mohamed wakati nilipofanya mabadiliko katika ofisi ile nilimuondoa hivi sasa yuko *DPP Law Review Commission.* Kwa hivyo, *signature* hizi hazifai, tukamwambia hizo zote sizo, lakini bado yule kijana kashika hizi ni *fake.* Sasa mimi nasema ana nguvu gani ya ku-*verify* hivyo vyeti. Mimi nikastaajabu sana na mimi nilimwambia hicho cheti sio *fake*, lakini kashikilia kuwa ni *fake*, basi.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nilikumbuka hadithi tuliyopewa na bibi na wazee wetu, kwamba kuna watoto wengine hata ukiwaambia nyamaza kimya lazima atanyanyua kidole, ndio huyu ni lazima anyanyuwe kidole aonekane, kwa nini sijui. Sasa hii ni hali ambayo tumefika hapa. Hawa ni wafanyakazi ambao hata hiyo adabu ya kufanya kazi haipo. Mimi waziri nimeshamwambia hicho si *fake* bado hataki. Sasa aidha kuna ajenda yake mwenyewe hatuijui au kama si hivyo anawatia doa baya au jina baya wakubwa wake na ndio maana siku zote tunamlaumu Mhe. Waziri pale, kitu ambacho yeye ana nia njema kabisa, lakini ni watu wake.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mfano uhamiaji unapokwenda na cheti wanapoona kwamba wana wasi wasi nacho, basi wanakuja ofisini kwa mrajis wanamwambia mbona tuna wasi wasi na cheti hiki. Mrajis anakwenda anatizama na anamuambia hiki ni sahihi au hiki sio sahihi. Kama wao wana wasi wasi basi watujie sisi sio wao waseme kwamba hiki ni sahihi au sio sahihi sivyo. Kwa hivyo, ajenda yao hiyo hatuijui na mimi nilimwambia Mhe Salma Mohamed anipe jina la huyo jamaa, mimi nitamuandikia barua aseme hizi kapewa na nani, maana yake anasema kapewa hizi *signature*, kwa sababu hawa watu mmoja keshastaafu. Mimi nakwenda pake nateuliwa kama Waziri wa Katiba na Sheria Mgonja ameshastaafu hayupo hasa, tukakaa baada ya kufanya marekebisho Mohamed nikamuondoa pale nikampeleka *Law Review Commission*. Lakini yeye katia ndani ya mtoto wa meza, ukija anatizama anakuambia hiki ni *fake*. Kwa kweli hatutokwenda hivi, hawa wana ajenda yao ambayo ndio wanamtia jina baya Mhe. Waziri pale na Mkurugenzi wa Vitambulisho, kila siku tunapiga kelele kumbe sio wao ni wale watu wao. Kwa hivyo, suala hili Mhe. Salma Mohamed ni kama nilivyokuhadithia hivyo na mimi nitachukua hatua ya kumuandikia barua ili atuambie hii kapewa na

nani. Kweli kapewa na wizara kitu ambacho sio kweli wala sifikirii na halafu tutajua ni njia gani ya kufanya ili kukomesha mambo kama haya.

Mhe. Mwenyekiti, tatizo jengine lililozungumzwa ni vyeti *fake* na Mhe. Salamin Awadh Salmin alisema kwamba kuna watu walikamatwa wakenda polisi, halafu polisi habari aliyokuwa nayo yeye anasema wametolewa pale. Mimi nilikuwa sina habari mpaka ulipoeleza ndio mimi nikatafuta, nikaambiwa ni kweli walikamatwa kwa vyeti *fake* wakapelekwa Mazizini, pale Mazizini akenda mkubwa akasema watolewe. Kutolewa kwao nilifuatilia nikaambiwa kwamba walikwenda polisi kwenye idara iliyokuwa ya *anticorruption*, idara ile imeshafutwa kwa sababu siku hizi tumeshaunda chini ya sheria ya *anticorruption*. Kwa hivyo, ile *department* ya *anticorruption* ya polisi haipo, lakini alikwenda kule na polisi aliyekuwepo kule sijui akayachukua mafaili wakasema tutayatizama, sijui kama wameyapeleka kwa DPP au hawajapeleka, huo ndio ukweli ulivyo.

Lakini Mhe. Salmin Awadh mimi naomba nikuambie kitu kimoja, polisi wana matatizo sana na hawatusaidii kikazi. Kwa nini, kwa sababu mimi nilipata habari kwamba kuna vyeti *fake* vinavyokuwa-*printed*. Zamani kabla ya Ramadhani ile iliyopita yaani ni mwaka mmoja sasa, mimi nilikwenda Pemba, wakati narudi kuna mtu akaniambia mheshimiwa nataka cheti. Nikamwambia cheti fanya utaratibu. Akaniambia utaratibu utachukua siku nyingi. Akaniambia mimi nakuhakikishia siku moja tu nitapata cheti. Nikamwambia haya, mimi nikawaambia watu wangu pale, lakini hakwenda kwa watu wangu, angekwenda mimi ningewakamata vizuri na nikawatia adabu, lakini hakwenda. Alikwenda katika hivi vichochoro vinavyopigwa vyeti *fake.*

Mhe. Mwenyekiti, mimi binafsi nikachukua jukumu la kuwaita watu wetu tuliopewa kutusaidia kazi katika ofisi yetu, watu wa idara. Nikamwita nikampa hiyo kazi akaifanya vizuri sana. Akanijia akaniambia kuna sehemu tatu, naomba nisizitaje kutokana na unyeti wenyewe. Kuna sehemu tatu ambazo zinafanywa vyeti pahala kadhaa, anayefanya ni fulani na ofisi yake ni hii na pahala kadhaa na mwengine anayefanya ni fulani na ofisi yake ni hii na pahala kadhaa, anayefanya ni fulani na ofisi yake ni hii na wanafanya kwa bei hii shilingi 50,000.

Mimi nikamwita Kamishna wa polisi. Narudia nilimwita Kamishna wa Polisi siri, mimi nikamwambia nifanyie hii kazi, sijui mimi sio polisi, lakini masuala ya uchunguzi najua kwa sababu ni mwanasheria. Mimi nimeshajua ni pahala kadhaa panatolewa vyeti, mimi nachukua shilingi 50,000 au shilingi 100,000 nakwenda namuambia bwana nataka kufasiri sasa hivi hebu fanya mpango, situtamkamata yule mtu. Wallah mpaka leo Kamishna wa Polisi anasema

bado tunachunguza, tunafanya nini maana yake mpaka tuwe na mambo mazuri na nini. Sasa hawa jamani ndio wanatusaidia kazi hawa. Lakini mimi najua, maana yake nilichukua njia nyengine najua kwamba katika hao watu watatu au maeneo matatu hayo, mmoja nasikia alikuwa *X Police Officer*. Sasa labda ile kwenda kumkamata na nini ataona tabu. Lakini anatuharibia vyeti vinakwenda mitaani. Ilipofika Ramadhani iliyopita nikamkumbusha. Kamishna watu Ramadhani hawakumbushani, aah! mheshimiwa maana yake tunafanya uchunguzi wa ndani, haya.

Mhe. Mwenyekiti, tukakaa mpaka hivi karibuni Mhe. Bi Zaynabu alikuwepo ofisini kwangu tulikuwa tukizungumzia habari ya haya mambo ya kubaka, tukamwita na Kamishna, lakini Kamishna mwenyewe hakuja siku hiyo alikuwa na dharura, alikuja msaidizi wake, akaja DPP baada ya kumaliza mkutano, nikamwambia yule msaidizi wake asubiri, halafu nikamuelezea suala hili. Akaniambaia haa! mheshimiwa tutatizama, mpaka leo. Huku watu wanafanya vyeti, wao hawachukui hatua yoyote. Sasa polisi jamani hawatusaidii hata kidogo na mimi nasema haya kwa uchungu, kwa sababu hawa watu tungekuwa tumeshawakamata na kuwazuia na si hasha hao waliokwenda huko Mhe. Salmin Awadh waliochukuliwa hapo Mazizini si hasha, sina uhakika kwamba wameteuliwa na hao hao polisi, sina uhakika na hilo. Lakini hiyo ni *conclusion* yangu kwa historia yote ninayokuambia.

Kwa hivyo, matatizo ni hayo Mhe. Salmin Awadh sisi tutajitahidi, lakini na wenzetu polisi watusaidie, kwa sababu kazi hii si ya mtu mmoja na hii ni ya kila mtu, sasa tukishirikiana sote basi tunaweza kufika pahala.

Mhe. Mwenyekiti, suala jengine ambalo pia lilizungumza Mhe. Salmin Awadh Salmin ni mambo mawili. Kwanza ni lile suala la kesi ya Mwinyi Shehe na moja tayari nimeshaizungumza ya Mpakia, lakini kuna kesi nyengine ya Mwinyi Shehe. Kwa kweli Mwinyi Shehe ninamjua na kesi yake ninaijua, kwa bahati nzuri alikuja juzi wiki iliyopita wakati kuna Baraza hapa asubuhi akaja ofisini kwangu ndio mara ya mwanzo kuipata kesi hii.

Sasa alipokuja na mimi asubuhi lazima nipite ofisini na halafu ndio ninakuja Barazani. Kwa hivyo, nilipofika pale nikamkuta Mwinyi Shehe na mwenzake.

UTARATIBU

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Mhe. Mwenyekiti, mwananchi ambaye amenileta malalamiko sijui kama anayo majina mawili, lakini barua aliyoniletea anaitwa Abdulrahman Bakari Rajab.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Mwenyekiti, ipo nyengine nitamuelezea. Lakini kuna Mhe. Hija Hassan Hija ndiye aliyezungumzia kuhusu Mwinyi Shehe na Mhe. Salmin Awadh Salmin naomba radhi kwa hilo. Lakini naomba niendelee nayo na halafu na hii ya Abdulrahman ipo. *(Makofi)*
Sasa huyu Mwinyi Shehe akaja na mimi nikamwambia asubuhi hutaniwahi njoo mchana, basi alinilitea makaratasi mengi sana na akaniambia haya ndio maamuzi ya mahakama soma na halafu unipe jibu, basi mimi nikamwambia sisomi hivyo na siwezi kukupa jibu hapa. Jambo la msingi ni kwamba wewe nenda kaandike barua eleza maelezo yako yote utie viambatisho vyako na halafu niletee na mimi nitatizama na nitakujibu, aa! Lazima kwa sababu sisi na kesho kutwa Ramadhani na watu hawataki. Kwa hivyo, mimi nikamwambia hata kama ni msikiti na kesho kutwa Ramadhani, mimi siwezi kusoma makaratasi yote hayo hivi sasa na halafu nikakupa jibu, isipokuwa kafuate utaratibu huo.

Mhe. Mwenyekiti, kwa bahati alikuwa amefuatana na mwenzake na yule mwenzake akawa *reasonable*, basi akazungumza naye lakini kila akizungumza naye hataki na pale akatoa maneno pale na kwa bahati mimi nikakaa kimya na nikamwambia maelezo yangu ni hayo, basi yule mwenzake ndiye aliyemchukua akamwambia twende tutakuletea, mpaka leo bado hawajaleta barua kwa hiyo sina la kufanya tena wiki iliyopita tu ndipo alipokuja.

Kwa hivyo, bado hajaleta barua nasubiri barua yake ije niitizame na halafu tujue kama hii kesi ilifika Mahakama ya Rufaa na ikatengua maamuzi ya Mahakama basi kisheria *status court* ndiyo inayobakia. Mhe. Mwenyekiti, kwa maana hiyo yale mambo yaliyokuwepo kama yameshatenguliwa uamuzi wa Mahakama Kuu ndiyo yatakayotizamwa na mimi nikamwambia yote ayalete hayo, ili nitizame Mahakama Kuu na Mahakama ya Rufaa zimesema na bado hajaleta.

Mhe. Mwenyekiti, naomba alete hiyo kama anataka tumsaidie basi tutatizama upo uwezekano kwa kumsaidia kwa mujibu wa sheria tutamsaidia na ikiwa hakuna pia tutamwambia.

Mhe. Abdulrahman Bakari naye tatizo lake ni hilo kama la Mwinyi Shehe. Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli Mhe. Abdulrahman Bakari alikuja ofisini kwangu mwaka 2010 mara tu baada ya kuteuliwa nikakaa kiasi ya miezi 6 akaja, na huyu mtu akija utafikiri sijui mtu gani maana yake zile mbwembwe anazotia utafikiri ni mtu wa usalama gani kutoka wapi sijui labda kwa Obama.

Kwa hivyo, akasema pale na kutisha pale nani, basi mimi nilimwambia utaratibu nielezee na baadaye nikamwambia niletee makaratasi basi akaleta. Mhe. Mwenyekiti, kwenye makaratasi yeye anachodai anasema kwamba hakuwepo wakati ule wa kuuzwa ile nyumba.

Lakini mimi ninayo *judgment* hapa Mhe. Mwenyekiti na nitaomba nimkabidhi Mhe. Salmin Awadh Salmin. Sasa *judgment* inasema kweli hakuwepo, lakini *notifications* zote alipelekewa yeye pamoja na watoto wake waliokuwa wakikaa hapa na yeye alikuwa hayupo na zimo ndani ya *judgment*. Kwa hiyo yeye alidharau na unapoitwa na mahakama na ukadharau basi watu wanatoa maamuzi bila ya yule mwengine kuwepo ndivyo walivyofanya.

Mhe. Mwenyekiti, wakati alipokuja aliniambia basi nilimwambia sasa lete ushahidi wako kwamba wewe ulikuwa hupo, yule mzee akaa na baadaye akaja tena na nilimwambia ulete ushahidi pamoja na maelezo yako na wala hakuleta. Kutokana na hali hiyo, niliomba kesi mahakamani na ikaja hii na maamuzi ya mahakama ni *very clear* inasema hasa kwamba banda hili liliuzwa baada ya kuwa *notified* kwa watoto wake na huyo *court broker* akenda akawapa barua na wakasaini kwenye kitabu.

Kwa mfano, mtoto wa Mhe. Salmin nikaja mimi nikampa barua na kusaini na kumwambia mpe baba yako kimahakama halafu tena hakukwambia, basi hilo litakuwa ni suala jengine.

Hata hivyo, kisheria unaweza ukaleta ushahidi wako kwamba mtoto wako hakukupa pengine baada ya siku ile alipopewa ile barua alisafiri au vipi na yote haya ni mambo ambayo yanakubalika, nilimwambia niletee na wala hajanileta mpaka leo. Mhe. Mwenyekiti, sasa mpaka aliponiuliza na mimi nikamwambia nilimwambia alete kitu fulani, nafikiri ulimwambia na baada ya kumwambia basi jana nakwenda ofisini ndio nakuta barua.

Sasa jana siwezi kuishughulikia Mhe. Mwenyekiti, yaani jana kuamkia leo ndio nakuta hiyo barua ya mambo mengine aliyoileta, lazima nikae niyatizame. Kwa hivyo, kesi ya Mhe. Abdulrahman ndivyo hivi ilivyo, barua hivi sasa iko ofisini kwangu na sijapata nafasi ya kuitizama na jana bila ya shaka nisingeitizama mpaka tumalize bajeti nitaitizama na kama kuna haki yake basi tutampa.

Lakini hii kesi napenda ujue ni ya zamani sana, tokea mwaka 2004 mpaka mwanzo amekuja kulalamika mwaka 2010 ni miaka 6 na hivi sasa ni mwaka 2013 ni miaka 9. Kwa kweli kisheria kuna utaratibu wake, yaani kuna kitu kinachoitwa *limitation* kama hujadai katika kipindi fulani, yaani unayo madai

halali, lakini hujadai katika kipindi fulani kwa hiyo kuna *Limitation Decree* ambayo inakufanya wewe huwezi tena kudai.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nimemwambia alete ndio ameleta jana, basi nitatizama na kama tunaweza kumsaidia basi tutamsaidia na ni wajibu wetu kumsaidia ikiwa kuna njia ya kumsaidia na ikiwa hakuna basi tutamwambia na hii ndio *story* ya Mhe. Abdulrahman.

Jambo jengine ambalo lilizungumzwa ni kuhusu dhamana. Mhe. Mwenyekiti, kweli dhamana ni haki ya kila mtu na hiyo ni general, kwamba tukisema dhamana ni haki ya kila mtu, lakini pia kuna sheria ambazo zinazozizuia zile dhamana kwa mujibu wa sheria. Kwa mfano, katika hiyo Sheria ya Dhamana inasema kwamba dhamana anaweza kupewa mtu yeyote isipokuwa aliyeua hapewi, mwenye kutaka kupindua nchi hapewi, kama siku hizi kuna *economic crime* hupewi.

Vile vile kuna Sheria ya mwaka 2012 inasema kwamba Mkurugenzi wa Mashtaka kwa makosa fulani anaweza kuzuia dhamana ya mtu na hiyo ni kwa mujibu wa sheria, ambayo sisi Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi tumeitunga. Mkurugenzi wa Mashtaka hawezi tu kuzuia hivi hivi atakuwa anakwenda kinyume na maadili yake na atakuwa ni mkosa, lakini tulimtungia sheria na tukamwambia kwa makosa haya au utaratibu huu usitoe dhamana ndivyo anavyotekeleza.

Kwa hivyo, hilo ni suala la dhamana Mhe. Mwenyekiti, ambalo napenda niliseme kwa misingi hiyo hatuna haja wala nia ya kumuweka mtu ndani kwa kitu chochote kile isipokuwa kwa utaratibu wa sheria.

Mhe. Mwenyekiti, suala jengine ambalo limezungumzwa kuhusu *DPP* ni mafao. Kwa kweli mimi nakubali sana *DPP* anao wakati mgumu pamoja na upande wa *AG* na hata watu wa *Law Review Commission*, bado wana wakati mgumu hasa wakiwatizama wenzao wa mahakama.

Lakini naomba tutafautishe baina ya Hakimu au Jaji na hawa watu wengine kama vile Waendesha Mashtaka, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu. Hakimu au Jaji amepewa mshahara kutokana na ile nafasi, yaani nafasi ile ya uhakimu ndio inayofanya mshahara ule na hiyo imechukuliwa kwa mambo mengi tu. Mhe. Mwenyekiti, Hakimu tunajua ni *risk*, yaani yale mambo ambayo yanamkabili hakimu ni tofauti kidogo na Waendesha Mashtaka na Ofisa ya Mwanasheria Mkuu.

Hata hivyo, choyo ni kuona mtu ambaye yuko Ofisi ya *DPP* amekaa kule miaka 6 au 7 sasa anamuona hakimu ambaye ameingia juzi anamshinda na

hilo ni tatizo nakubali. Mhe. Mwenyekiti, hivi sasa ni kweli kama alivyosema Mhe. Hija Hassan Hija kwamba kuna barua Ofisi ya *DPP* wanataka kuondoka, ni kweli maana yake mtu ameshaahidiwa kama atakwenda *ZRB* atapata mshahara wa milioni 3,000,000/= na huku kwa *DPP* anapata mshahara wa lakini 400,000/= au 500,000/=, bila ya shaka lazima wafanye hivyo. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, suala hili tunaliona na tunajitahidi kuzungumza nao. Kwanza hizi kazi zetu wakati mwengine zinataka *commitment* ukiacha mshahara zinataka *commitment*, sasa ukiwa *committed* na zile kazi zako basi nafikiri kidogo. Lakini mbali hayo tunajaribu kuzungumza pamoja na kutafuta njia angalau za kuwasaidia hawa wenzetu. Kwa hivyo, sisi tuna *share* matatizo yao na tunajaribu kukaa pamoja na kutizama njia gani tunaweza kuwasaidia wenzetu hawa. Mhe. Mwenyekiti, suala hili naomba niliseme hivyo tu.

Pia kuna suala jengine ambalo limezungumzwa na hili alilizungumza Mhe. Ismail Jussa Ladhu kuhusu kesi ya watoto. Mhe. Mwenyekiti, kesi ile kweli mwaka jana ilikuwa *register* na nimesema taarifa nilikuwa nayo na matatizo yote yale yaliyotokea tulikuwa tunafanya uchunguzi na tumepata baadhi ya mambo, ambayo hivi sasa tumeyapeleka kwa *DPP* kutizama kweli ina *warrant* kesi ile kuipeleka mahakamani ya suala la rushwa. Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu iko katika *stage* hiyo basi nisingelipenda niseme zaidi ya hapo.

Lakini napenda niseme tu katika kesi hii nafikiri aliizungumzia Mhe. Hija Hassan Hija, naomba nielezee kidogo. Kwa kweli kesi hii ina ubabe wa watu wawili na kama hatukuichukua kwa hadhari inaweza kutuweka pabaya. Mhe. Mwenyekiti, baba wa watoto ni tajiri mkubwa sana ana Hoteli ya *Zanzibar Beach Resort* pia Hoteli ya *Kunduchi Beach,* kwa upande wa mama na yeye *Alhamdulillah* anao uwezo kidogo, sasa kuna *force* mbili zinazoshindana.

Mhe. Mwenyekiti, kweli ilikwenda mahakamani na mahakama ikaamua wale watoto kwa sababu ya yote yale wawekwe kwa bibi zao na mmoja bibi wa baba na mmoja bibi wa mama wakakata apple na mahakama ya Rufaa ikasema hivyo hivyo. Mhe. Mwenyekiti, tunajua na Mhe. Ismail Jussa Ladhu anajua kwamba kuna suala linaloitwa *welfare principle of a child* inatizamwa vizuri, kwamba yule mtoto akipelekwa pahala pale anapopelekwa je atafaidika.

Mahakama ndivyo walivyofanya, kwa sababu baba wa mtoto alikwenda na kusema uongo na kudanganya, akenda kwa Sheha wa Kikwajuni akamwambia mimi nimezaa hivi juzi na nataka cheti cha kuzaliwa cha mtoto haraka haraka kwa sababu anazo fedha basi akampa sheha fedha na kutoa

barua kwa ajili ya kutengenezewa cheti. Sasa sheha ameshasema kwamba huyu mtoto kweli amezaliwa basi sisi tutatoa, kikatolewa cheti kumbe akatumia cheti kile akawasafirisha wale watoto Falme za Kiarabu.

Kwa hivyo, huyu baba wa mtoto mwenye umiliki wa hizo hoteli akatumia njia alizonazo huko na ikabidi wale watoto waletwe huku, yaani warudishwe tena ndio ikenda mahakamani. Kwa kweli mahakamani mimi nafikiri kama ningekuwa na zawadi ya kutoa hasa basi ningeliwapa mahakimu wangu kwa sababu walitumia akili nzuri sana.

Mhe. Mwenyekiti, mahakamani walivyosema ni kwamba huyu mtoto hawezi kwenda kwa baba, kwa sababu baba kwanza ni muongo amedanganya na mtu wa rushwa. Kwa hivyo vitendo vyake ni vichafu kisheria na wala hatuwezi kumchukua mtoto tukamuweka pale atakuwa na atarithi khulka hiyo.

Vile vile mahakama ikasema haiwezi kumuweka kwa yule baba, kwa sababu yule ana hoteli anauza pombe mule na kuna mambo mengi ya ufuska yanafanywa, sasa ukimchukua matoto ukamuweka kule na kila siku unamchukua unakwenda kwenye hoteli kule anaona watu wanacheza *disco*, basi yule mtoto naye ataharibika.

Kutokana na hali hiyo, *Welfare Principle of a Child* ikatumika, ndio wakasema kwamba wawekwe kwa bibi na hawa bibi mahakama ikawa *very wise* wakasema mmoja yule mtoto wa kike awekwe kwa bibi wa baba na yule mtoto wa kiume awekwe kwa bibi wa mama na hawa sio kwamba ndio wanaolea aa! Isipokuwa wao wana dhamana tu ya kuwatunza.

Mhe. Mwenyekiti, uamuzi wakati mwengine mahakama lazima zitumie akili kama hizo na si lazima tutizame kwenye vitabu tu, kwa maana hiyo, unatakiwa utumie akili kama hizo, ili kusaidia maamuzi ya haki. Kwa hivyo, hivi Mhe. Mwenyekiti, ndivyo ilivyokuwa.

Mhe. Mwenyekiti, nimetumia muda kidogo na nikasema lazima niseme hayo, kwa sababu *at least* Waheshimiwa Wajumbe waweze kufahamu na kuelewa hasa yale ambayo yapo. Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo niseme tena kwamba ninawashukuru sana wajumbe kwa michango yao mingi ambayo wametoa na mingine bila ya shaka sikuweza kuyasema yote, lakini nilisema niseme yale mambo ambayo ni muhimu *at least* Waheshimiwa Wajumbe wajue utaratibu uliopo na vipi ambavyo tunajitahidi katika kufanikisha masuala yetu haya. Kwa kweli nimefurahi sana kupata *comments* zenu kama nilivyosema na *comments* hizi tutaweza kuzishughulikia.

Mhe. Mwenyekiti, la mwisho kabisa ni suala ambalo nilikuwa sipendi nilizungumze, lakini kwa sababu nalo limezungumzwa basi na mimi nitalizungumzia kwa mistari miwili ni kuhusu suala la Rasimu ya Katiba. Mhe. Mwenyekiti, wataalamu wengi wanasema kwamba Katiba ni dira ya mwelekeo wa nchi, pia katiba ina malengo yake na malengo hayo ni kusaidia nchi vile vile katiba inafufua matarajio ya wananchi. Kwa hivyo, hii ndio ile nini hasa katiba na ukesha kuyajua hayo mambo matatu basi wewe mwenyewe utaweza kusema kwamba unataka katiba ipi? Je, katiba au rasimu tuliyonayo inasaidia au haisaidi.

Mhe. Mwenyekiti, jambo moja tu hapa napenda kusema kwamba Mhe. Salmin Awadh Salmin aliposema kwamba nchi moja ina marais watatu hilo naomba nitofautiane naye si nchi moja.

Kwanza ukisema nchi moja ina maana kwamba kama hii Zanzibar si nchi na Tanganyika si nchi. Kwa hivyo, hizi ni nchi mbili Tanganyika na Zanzibar na kwa mujibu wa rasimu ile inasema kwamba Tanganyika kuwe na Rais wake na Zanzibar pia kuwe na Rais wake na halafu yule Rais wa tatu awe wa Muungano wa hizi nchi mbili na hiyo ndio tafsiri hasa ya ile rasimu. Sasa kama tunataka hiyo au tunataka nyengine hiyo bado naendelea kusema ni maamuzi ya wananchi na wananchi wenyewe ndio tutakaosema. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nawaomba sana Waheshimiwa Wajumbe, kwamba tutizame kwamba katiba ni kitu ambacho tukikubali kina muelekeo wa baadaye, maendeleo ya nchi pamoja na kututoa hapa tulipo na kuelekea kwenye misingi mizuri na ya busara.

Baada ya kusema hayo, Mhe. Mwenyekiti naomba radhi kwa wale ambapo pengine sikuwajibu lakini si kwa nia mbovu, isipokuwa mas-uli yalikuwa mengi lakini naheshimu mawazo yenu yote na naomba kutoa hoja

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti, naafiki.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, niwaulize wale wanaokubaliana na hoja ya Mhe. Waziri wanyooshe mikono na wanaokataa, waliokubali wameshinda. *(Makofi)*

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa Baraza limejadili na kuikubali hotuba ya bajeti ya Wizara ya Katiba na Sheria. Sasa

naliomba Baraza lako tukufu likae kama Kamati ya Matumizi, ili kupitisha vifungu vya matumizi vya wizara yangu.

KAMATI YA MATUMIZI

FUNGU 14 – MAHAKAMA KUU ZANZIBAR

Kifungu 0201	Utawala Unguja	71,000,000/=
Kifungu 0301	Ofisi Kuu Pemba	19,000,000/=
Jumla ya Fungu		**90,000,000/=**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

FUNGU 36 – WIZARA YA KATIBA NA SHERIA

Kifungu 011 Wakala wa Usajili wa Biashara na Mali

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Mhe. Mwenyekiti, mimi nilikuwa nikiangalia kwenye hili fungu la Wakala wa Usajili wa Biashara na Mali kuna fungu hapa 142234, 142235 na 142237 haya mafungu nayaona yako mapungufu sana kuliko makusanyo ya mwaka uliopita labda sijui ni sababu zipi kwa maana mara hii anategemea kukusanya kidogo zaidi kuliko kile ambacho mara nyingi tunatarajia kama ulikusanya 50 mwaka jana, basi mwaka huu utakusanya 60, sijui tatizo nini hapa.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Mwenyekiti, ni kweli. Lakini naomba tu Waheshimiwa Wajumbe wakumbuke kwamba zamani tulikuwa na Mrasji Mkuu wa Serikali na hivi sasa tumeikata Mrajis wa Vizazi na Vifo na Mkurugenzi Mtendaji wa Usajili wa Biashara na Mali.

Kwa hivyo kwa sababu hiyo yale mapato yamegawika sehemu mbili, ambapo kuna sehemu ile ya Mrajis wa Vizazi na Vifo ambayo hapa haipo na hii ni ya huyu Mkurugenzi Mtendaji wa Usajili wa Mali Biashara, kwa hiyo ndio maana ikapungua kwa sababu tumeikata sehemu mbili.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Mhe. Mwenyekiti, nimemsikia Mhe. Waziri. Lakini labda angetufafanulia kidogo katika haya mafungu kwa sababu kuna Uandikishaji wa Makampuni, uandikishaji wa majina ya kibiashara halafu kuna ujira wa kutengeneza nyaraka. Labda ubaguzi wake umebagua vipi, lipi likenda wapi na lipi ndio lina sababu zile za kupungua. Yameenda vipi sasa, kidogo nilikuwa nataka ufafanuzi wa hapa. Maana tuone alipohama akaenda kule imesababisha kwamba huku uwepo pungufu.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Mwenyekiti, katika wakala wa usajili wa biashara na mali hii ni mambo yanayohusiana na Makampuni, mambo ya *registration* ya kampuni, majini na kibiashara na mambo kama hayo. Halafu yale mengine ambayo yamo katika urajisi wa vizazi na vifo. Kwa hivyo mapato yale yote hayapo hapa. Kwa hizi ni sehemu kidogo sio kama zile za mwaka jana ambayo yote yalikuwa ni pamoja.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mbarouk Wadi Mussa umeridhika.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Kwenye haya mafungu mawili sina tatizo lakini hili la tatu la ujira wa kutengeneza nyaraka hili, hebu kidogo anisaidie ufafanuzi. Kwa sababu tulianza na milioni 18 tukaja na 38 sasa hivi tumeshuka katika 19 katika kutengeneza nyaraka. Namimi najua hapa kuna makusanyo mazuri kidogo katika kutengeneza nyaraka. Maana unapomtengenezea mtu una chaji Kamishen. Sasa hatu kidogo atusaidie Mhe. Waziri hapa.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Mwenyekiti, ni kweli, kwanza tulianza kwa milioni 18 halafu ikaja 38 na hivi sasa tumerejea katika milioni 19. Lakini kama nilivyosema mwanzo hii Idara ilikuwa ya pamoja, ilikuwa hii ni nusu ya Idara. Zamani Mrajisi Mkuu alikuwa na mambo yote. Mwaka jana kwenye hii 2012/2013 mapato haya yalikuwa kwa pamoja kwa Mkurugenzi wa vizazi na vifo. Sasa safari hii kwa sababu itakuwa haipo yale mapato ambayo yapo kule na kule kuna nyaraka na fedha hizi ambazo tunapata za usajili wa vizazi, halafu kuna fedha zile tunazolipa *registration* na mambo kama hayo. Kwa hivyo zile zote zimepungua. Kwa hivyo bado hapa lazima ipungue kwa sababu yale mapato ambayo tunayapata hayakuchanganyika na yale mapato kama ya mwaka jana ndiyo ikawa hivi.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, mimi nafikiri hoja yangu ni ndogo sana, Mhe. Wazidi anazunguka tu sana huko. Nilikuwa nataka kuona, maana ujira wa kutengeneza nyaraka unatofautiana kabisa na mambo hayo ambayo anayazungumza Mhe. Waziri. Na hili fungu linaonekana limebakia upande huu huu. Sasa hoja yangu ni kwamba huku tulikuwa tumeshakuwa na makusanyo yetu ambayo mapato yatu yalikuwa yameshakuwa makubwa kidogo. Katika fungu hilo hilo moja ambalo halikuenda ule upande wa pili. Sasa ndio nilikuwa nataka kujua ni sababu zipi zilizosababisha kwamba mara hii tukusanye kidogo.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mtando labda nikufahamishe mimi kwa sababu mimi nimefahamu vizuri. Mhe. Waziri, anachokisema zamani ilikuwa ni idara moja sasa imegaiwa, ndio maana ikafikia hali hiyo kwamba kuna

mgawanyo, kwa hivyo lazima kipato chake kitakuwa tofauti na vile zamani. Hayo ndiyo maelezo ambayo ameyaeleza Waziri na ameshakuwa ameyarudia zaidi ya mara tatu. Mimi naona maelezo yanakubalika kabisa.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Mhe. Mwenyekiti, sina tatizo na hayo maelezo anayoyasema, mimi niko na tatizo la kwenye hili fungu lenyewe. Kwa sababu ukizungumzia neno ujira wa kutengeneza nyaraka maana yake kwamba fungu hili au lile fungu ambalo analizungumzia la vizazi na vifo, limekwenda katika Msajili wa vizazi na vifo sina tatizo. Nazungumzia lile fungu moja tu, sababu za kushuka kwake hili utengenezaji wa nyaraka kwa sababu umebakia uko hapa hapa haukuondoka. Maana yake wanatengeneza nyaraka. Nafikiri rabda Mhe. Waziri afafanue zaidi, wanatengeneza nyaraka *document*. Sasa tuone kwa nini kumeshuka, kuna tatizo gani, mapato yetu yameshuka badala ya kupanda wakati yalikuwa yameshafika kwenye milioni 38, sasa yanarudi mpaka kwenye 19, labda kuna sababu.

Maana yake huu utengenezaji wa nyaraka umebakia upo pale pale, haukuondoka huu. Nyaraka zile za vizazi na vifo vile vitu mbali kabisa. Nafikiri nimeeleweka Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyosema mwanzo lakini zaidi idara hii sasa kwanza tutizame ile *pending* ya dunia. Mhe. Mbarouk Wadi Mussa (Mtando) ni miongoni wa Waheshimiwa Wajumbe pamoja na Mhe. Hamza Hassan Juma, waliokwenda Uchina kusoma mambo haya. Sasa kule wenzetu wana mambo mawili.

Kwanza wana *register* zile *documents* zao kwa dakika 10 tu na halafu ule ushuru wake umepungua. Kwa sababu ili kuvutia watu wengi kufanya shughuli. Lakini zaidi mbali na hayo tumeyazingatia hayo. Lakini la pili ni kwamba utaona katika utaratibu wa serikali hivi karibuni zile nyaraka za Ardhi zimeondoka kutoka Afisi yetu kwenda Wizara ya Ardhi, Maji na Nishati. Kwa hivyo hata yale mapato tuliyokuwa tunapata kwa usajili wa nyaraka za ardhi nazo hatunazo sisi sasa, zimekwenda huko katika Wizara ya Ardhi, Maji na Nishati.

Kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti, lazima kwa vyovyote vile kutokana na hayo yote hizi pesa zitapungua na itakuwa haina maana kuweka fedha nyingi ambazo hatutoweza kuzikusanya kutokana na sababu hizo Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Waziri wa Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Mwenyekiti, nataka nitoe ufafanuzi wa ziada baada ya ule ufafanuzi ambao mzuri sana ambao ameutoa Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria. Ukiangalia kitabu chetu hichi huko juu kabisa kwenye *heading* utaona hasa kwa maana ya *actually*,

halafu utaona makisio. Kilichopo hapa ni makisio na hiki kinatokana na pengine haya makisio ambayo yamewekwa hapa hayakufikiwa. Ndio maana Wizara ya Fedha, ambao wanakaa na taasisi ambazo zinakusanya mapato wakaona ni bora warudi huku kwenye *actually* katika kipindi hichi cha mwaka huu.

Kwa hivyo ni lazima tuelewe kwamba hiki kilichopo hapa 38 milioni sio kwamba ndio kimekusanywa bali ilikuwa ni makisio. Sasa kama tunataka kwenda kwenye uhalisia pengine tutakapokwenda kwenye yale makusanyo halisi kwenye vitabu, kwenye zitabu tunaweza tukapata *brake down* hiyo. Lakini tulewe kwamba hichi kilichokuwepo huku ni makisio na sio *actually*. Ila hiki cha mwaka 2011/2012, ndio kilikuwa halisi. Huo ndio ufafanuzi ambao nataka niutoe.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Mhe. Mwenyekiti, tuendelee.

Kifungu 0011	Wakala wa Usajili wa Biashara na Mali	125,700,000
Kifungu 0901		

Mhe. Omar Ali Shehe: Mhe. Mwenyekiti, wakati nachangia nilipeleka ombi kwa Mhe. Waziri ili azingatie juu ya kupunguza gharama zitokanazo na usajili wa vizazi, hasa ile *let registration.* Niliomba hivi kwa sababu ni sera ya serikali kupunguza tozo katika hasa katika huduma. Na hii Mhe. Mwenyekiti, inatokana na sababu kwamba sehemu hizi mbili hatupaswi sana tumchangishe kwa sababu suala la kuzaliwa na suala la kufa, mtu katika kuzaliwa ni haki yake. Kwa hiyo kufanya mtu ukamtoza kitu cha katika suala la haki yake kwa kweli si sahihi. Lakini vile vile mtu ambaye tayari keshakufa badala ya serikali kumchangia, leo tunamtoza tena. Nadhani hiyo si haki.

Naunganisha na hoja ya Mhe. Mbarouk, kama kuna pahala, ikiwa huku kuna punguzo katika kusajili uandikishaji wa Makampuni tunaona kwamba inashuka, lakini huku kwenye vizazi na vifo *trend* inabakia ni ile ile. Kwa hivyo nadhani hapa Mhe. Waziri anikubalie. Kwanza sera ya serikali kwamba suala linalohusiana na huduma halitakiwi liwe linapanda kila siku. Lakini vile vile tuwahurumie sana kuhusiana na mtu keshafiliwa kumtoza fedha sana kwa ajili ya kupaka vyeti hivi pamoja na usajili. Naomba Mhe. Waziri alizingatie hilo na sasa naomba jawabu.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Mwenyekiti, ni kweli Mhe. Omar Ali Shehe alizungumza hayo na naomba radhi sikuyasema kwa sababu ya muda. Lakini hilo tumelitilia maanani sana. Ukitizama kifungu 402295 chini pale "ndoa zisizosajiliwa kabla" yaali *late registration* ni milioni sita na laki tatu. Suala hili tumepata malalamiko kwa watu wengi na hivi sasa

tunalifanyia kazi. Tumeshaandaa waraka, tumeshaupitia katika Kamati ya Uongozi ya Wizara. Hivi sasa iko katika hatua ya mwisho, kwa sababu tulikuwa tuna masuala megine ya kuweka na nafikiri si muda mrefu tutaipeleka kwenye Kamati ya Makatibu Wakuu ili Kamati hiyo ikirudisha tupeleke katika Baraza la Mapinduzi.

Kwa hivyo suala lake hilo tumelizingatia na haahidi kwamba suala hili litapelekwa katika Kikao cha Baraza la Mapinduzi kwa kupata maamuzi ya *registration* hii. Nashukuru Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Omar Ali Shehe: Mhe. Mwenyekiti, nashukuru kwanza nampongeza yeye binafsi kwa kuwa msikivu na kwa kuzingatia utu na thamani ya utu. Naomba Mawaziri wote wafuate mwenendo huo wa Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria.

Kifungu 0901	Vizazi na Vifo	219,300,000
Jumla ya Fungu		**345,000,000**

(Vijifungu vilivyotajwa hapo juu zimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya Mabadiliko yoyote)

FUNGU 14 - MAHKAMA KUU ZANZIBAR

Kifungu 0201 Utawala Unguja

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi hii kwa ajili ya kupata maelezo zaidi kutoka kwa Mhe. Waziri wa Katiba. Mhe. Waziri amejitahidi sana kutoa ufafanuzi juu ya hoja yangu ya ndugu Abrahman Bakari Rashid ambayo nyumba yake imeuzwa na Mahkama.

Lakini ninachotaka kusema Mhe. Mwenyekiti, pamoja na kwamba nyumba imeuzwa, mwenyewe hakuwepo na bila ya taratibu na kwamba nyumba hiyo wameuziana wenyewe wanasheria. Lakini alichodai madai yake kwangu niyafikishe hapa ni fedha zake ambazo zimebakia hajapewa mpaka leo. Nyumba imeuzwa kwa milioni nane na nusu, alichokuwa akidaiwa ni milioni moja na nusu. Kwa hivyo anadai fedha zake zilizokuwa zimebakia na amekuwa akisumbuka anakwenda akirudi hajaweza kupata haki yake. Kwa nataka Mhe. Waziri wa Sheria anieleze kwamba ni lini ndugu Abrahmani atapata haki yake hii iliyobakia. Atakaponijibu nikiridhika nitasema tuendelee.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyoeleza mwanzo narejea hayo hayo niliyoyaeleza kwamba hii ni kesi na kesi anapokuja mdai au mdaiwa kukulalamikia mara nyingi hutia chumvi ili kukufanya wewe uone kwamba kaonewa. Mimi sisemi kwamba nyumba haikuuzwa, lakini kuna misingi ya kisheria mimi nimeita faili hili kutoka Mahkama Kuu wamenileta, kuna makosa ambayo yeye aliyafanya. Mimi nimemwita nikamwambia nilietee taarifa fulani. Kama ninavyosema kaleta jana, jana nafika ofisini ndio taarifa hizo zipo.

Kwa hivyo mimi Mhe. Mwenyekiti, siwezi kusema hapa kwamba atapata fedha zake au hapati itategemea taarifa nitakazozipata na uchunguzi nitakaoufanya. Ninachomuahidi ni kwamba kama kuna haki yake nitampa. Lakini ikiwa hakuna haki yake hatuwezi kumpa na tutamueleza ni kwanini.

Lakini pia naomba hawa watu tunapowaambia wasikae tu huyu nilimwambia all most miaka miwili, lete taarifa mpaka kaja kuleta taarifa baada ya yeye kwenda kwa Mwakilishi wake na Mwakilishi kuna mimi na mimi nikamwambia kuna taarifa nimemwambia alete, miaka miwili angelikuwa keshaleta tungelikuwa tumeshajua.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, mimi ninachosema mimi nitalipitia hilo file tukimalizi hii bajeti, nitatizama, nitatafuta ushauri wa wenzangu Mahakamani halafu hapo ndio tunaweza kuamua kwamba kweli anayo haki au hana.

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, mimi ninachojua na ninavyomfahamu Mhe. Abubakari Khamis Bakary (Waziri wa Katiba na Sheria) hili jambo atalifuatilia ili haki iweze kutendeka. Kwa sababu haki sawa kwa wote. *(Makofi)*

Kwa hivyo naamini atayafatilia madai ya mwananchi wangu huyu na kama anayo haki basi haki yake ampatie. Kwa sababu Mhe. Mwenyekiti, leo tupo hapa duniani kesho na kesho kutwa tunarudi mbele ya haki. Mwenyezi Mungu atakwenda kutuuliza ni namna gani tumesimamia haki za watu. Kwa hivyo baada ya maelezo hayo nasema tuendelee.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, kwanza namshukuru sana Mhe. Waziri kwa ufafanuzi alioutoa katika hoja zangu nilizompelekea kwa maandishi. Na labda nimkumbushie hoja yangu moja ya msingi ilikuwa kuhusu madai ya maasesa ambao walikuwa wakidai kwa muda mrefu. Namshukuru sana Mhe. Waziri bajeti ya mwaka jana nilipoliomba hili na kwa sababu alikuwa na fungu ambalo alilitenga maalum kwa ajili ya kurekebisha mambo aliwalipa lakini kuwalipa kwenyewe alipunguza tu deni.

Kwa sababu kuna madai ambayo wanayodai kuanzia mwaka 2009 wamekuja kulipwa deni la mwaka 2012/2013. Sasa nilikuwa nataka maelezo kwa Mhe. Waziri je, zile zilizobakia za miaka ya nyuma na kama alivyosema Mhe. Salmin Awadh kwamba haki sawa kwa wote kwa hivyo hata hawa maasesa wana haki yao. Kwa hivyo kama wengine wanalipwa na wamelipwa kile cha mbele wakati cha nyuma bado. Basi naomba Mhe. Waziri kama kawaida yake ni mtu msikivu sana, naamini atanipa jawabu ya kuweza kuniridhisha pamoja na wananchi wangu. Mheshimiwa naomba jawabu.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru ni kweli mwaka jana tulipunguza sana hili deni, kwa sababu tulikuwa na deni la kiasi miaka mitatu au minne nyuma. Kwa hiyo mpaka sasa tunadaiwa. Ukitizama katika maposho humu kwa mfano kuna 108 milioni mpaka 203 miolioni hizi ni pamoja na kuwasaidia hao wenzetu ambao bado wanadai.

Sasa mimi namuhakikishia kwamba tu kwamba ingawa hizi hazitoshi deni hili tutapunguza tu lakini ni deni kubwa lakini tuajitahidi kila tunapopata fedha kulipunguza. Namuhakikishia kwamba katika hizi fedha ambazo tumepata basi zimo za kutoa kwa wale ambao wana deni lao. Namuhakikishia kwamba tutafanya hivyo.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, namshukuru sana Mhe. Waziri kwa kutekeleza ile ahadi au kauli ya haki sawa kwa wote. Kwa hivyo naamini kwamba maasesa wetu hawa wataweza kupata haki yao. Ahsante sana.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Nakushukuru sana Mhe. Mwenyekiti, mimi nilichangia kwa maandishi lakini nilimtaka Waziri anipe ufafanuzi kidogo. Nimeona Mahakama kuna watu waliokuwa wameshtakiwa kwenye Mahkama lakini bahati nzuri wanaposhtakiwa wakiwa watu wale hawajatolewa hukumu na siku nyengine wakakaa miaka miwili, miaka mitatu, au zaidi ikawa bado kupata hukumu. Lakini baadaye kesi itakapoendeshwa watu wale wakaonekana kwamba wameshinda kesi hawana hatia na wakati huku wameshasota ndani zaidi ya miaka miwili au miaka mitatu.

Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa nataka ufafanuzi je, watu hawa wanakuwa wanapata haki gani kutoka kwa serikali au kwa Mahakama. Je, watu hawa serikali inawaangaliaje, kwa sababu huku nyuma wameshapoteza muda wao wote kama wanabishara imeshakufa, kama watoto walikuwa wanasoma shule wameshakosa shule. Naomba jibu.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Mwenyekiti, ni kweli Mhe. Subeit Khamis Faki, lakini bahati mbaya namuomba radhi nilisahau kumjibu kutokana na wakati.

Lakini katika suala lake hilo ni kweli kwamba mtu anaweza akawekwa ndani na kesi ikawa inaendelea. Hapa naomba ajue Mhe. Mjumbe kwamba kuna kesi za aina mbili. Kesi ya madai na kuna kesi ya jinai. Sasa unapowekwa ndani kwa madai ina maana kuna mtu mwengine ambaye mnadaiyana halafu akakuweka ndani. Kama itakwenda kesi halafu ukashinda wewe una haki ya kumdai yule mtu mwengine ambaye alikuweka ndani kwamba mlikuwa mnabishana.

Lakini katika kesi ya jinai pia unaweza ukawekwa ndani. Hapa kuna kitu kinachoitwa *malicious prosecution*, kama una hakika, unaushahidi wa huyo aliyekuweka ndani kwamba kakuweka ndani isivyohalali, katumia tu pengine wadhifa wake na ushahidi unao, basi ukimshtaki kwa shtaka linaloitwa *malicious prosecution*, anaweza akahukumiwa na ukapata fidia kwa mambo yote ambayo umeyapoteza.

Kwa hivyo naomba achukue jibu hilo kwamba kuna *malicious prosecution* au kuna madai ya yule mtu na mtu katika kesi za madai.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Mhe. Mwenyekiti, namshukuru Mhe. Waziri kwamba amenipa ufafanuzi ya kutosha lakini nauliza tu. Endapo mtu kashinda na akafungua hiyo kesi na akadai madai lakini ikawa bado hajalipwa au serikali haijamlipa au Mahkama haijamlipa. Hatua gani nyengine anatakiwa mtu achukue.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Mwenyekiti, katika madai wewe unaedai unakuwa na Mwanasheria wako, sasa yule wakili wako anajua utaratibu wote. Unapotoa kesi halafu ukashinda kwa hivyo yule wakili wako anajua utaratibu wa kufatilia lile dai lako. Kwa hivyo siwezi kusema hapo ufanye vipi ufanye vipi. inategemea ile kesi yenyewe, inategemea maamuzi ya mahakama ilivyotaja.

Lakini pia inategemea wakili wako atakuwa *active* namna gani kulifuatilia lile suala ili kukupa haki yako wewe. Na kwa sababu wewe umeshamlipa yule bila shaka atafatilia tu kesi yako.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Mheshimiwa nimemsikia, tuendelee,

Kifungu 0201	Utawala Unguja	1,372,257,000
Kifungu 0301	Ofisi Kuu Pemba	850,444,000

Kifungu 0502	Mahkama za Mikoa	384,107,000
Kifungu 0503	Mahkama za Wilaya	509,629,000
Kifungu 0504	Mahkama za Mwanzo	156,606,000
Kifungu 0601		

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Nashukuru Mhe. Mwenyekiti, na mimi vile vile nimpongeze Mhe. Waziri kwa ufafanuzi wake mzuri na nimuombe azidishe kwa sababu leo kwa ufafanuzi mzuri katupatia wanachama wawili wapya wa CUF Mhe. Hamza Hassan Juma na Mhe. Salmin Awadh Salmin. Naamini akiendelea hivyo atatuongezea wengi zaidi Inshaallah kwa kukubali kauli mbiu yetu.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya salamu hizo ndogo naomba niende katika suala ambalo limelisimamiaa. Mhe. Mwenyekiti, katika mchango wangu nathamini kwamba Mhe. Waziri kutokana na muda hakuweza kuyajibu yote.

Katika suala langu nimezungumzia suala la Mahkamka za Kadhi hasa suala la madai au kadhia za kuwepo suala la rushwa katika Mahkama za Kadhi. Nikataka anisaidie maelezo juu ya kadhia ambayo niliizungumza mwaka jana.

Wakati tukichangia bajeti nilimwambia na akasema anaitambua na akasema kwamba linafuatiliwa suala hilo. Hii Mheshimiwa ni kadhia ya Kadhi ambaye alihusika kusikiliza kesi ile ile aliyesema tuwe na tahadhari nayo, lakini mimi siingii katika hukumu. Mimi nazungumzia kwamba kadhi katika ngazi ya Wilaya ilisikiliza. Na kwa sababu yeye Mhe. Waziri katujia na utaratibu mpya wa kutaja majina mimi siwezi nikamtaja jina. Kwa sababu nilipochangia nilisema namstiri lakini kwa sababu ya uwanzi uliouanzisha mimi naomba nimtaje.

Mhe. Mwenyekiti, Kadhi Mustafa wa Wilaya ya Mjini, huyu alituhumiwa kwa tuhuma kubwa za rushwa na kwamba alilikuwa anaegemea zaidi upande mmoja na kuna mawasiliano makubwa yamefanyika, kumekusanywa mpaka ushahidi mpaka kwamba kulikuwa na suala la gari kwamba alipatiwa na upande mmoja wa kesi hii.

Mhe. Mwenyekiti, mwaka jana nilipolizungumza Mhe. Waziri alinambia alilisikia na amelifatilia. Mwaka huu nimelichangia tena hakunijibu. Nilikuwa naoma anambie kesi ile imefikia wapi. kwa sababu Mhe. Mwenyekiti, aliuliza na kusema kwamba tukiendelea kufunika funika mambo ndipo tunapowaambia waendelee kula ruswa kwa sababu hakuna hatua yoyote iliyochukuliwa dhidi yao. Nilikuwa naomba anipatie maelezo Mhe. Waziri.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Mwenyekiti, namshukuru sana Mhe. Ismail Jussa, lakini nafikiri hilo kama nimelijibu. Suala hili nimelijibu

mwanzo kabla sijazungumzia kuhusu wale matajiri wakubwa wawili wanaogombana. Nilisema ni kweli kesi naijua na ina mambo mengi. Sasa sisi tukafanya uchunguzi wetu tukajua mpaka simu zilizopigwa na yote hayo tunayo. Lakini kiutaratibu nikasema kwa sababu tumeshapata huo hatuwezi kwenda Mahakamani. Lazima utaratibu tupeleke kwa DPP. Nikasema hivi sasa *file* liko kwa DPP, ndivyo nilivyosema.

Mhe. Ismail Jussa hizi sasa nimesema kwamba hili *file* sasa lipo kwa DPP nafikiri kidogo hukusikia. Kwa hivyo hili *file* sasa liko kwa DPP na linapitia halafu DPP atasema kama apelekwe Mahakamani au kuna tatizo fulani. Kwa hivyo tumuachie DPP ili baadae tutapata maelezo. Lakini hapo ndio hatua ambayo tumefika. Ninashukuru.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti nikiri kama hili alilizungumza basi limenipita la kama alighafilika yeye lakini kwa ufupi nakushukuru kwamba sasa nimepata maelezo nimeyasikia na ninashukuru kwamba limefikia katika ngazi ambayo kiutaratibu hatupaswi kuingilia, ngazi ya muendesha mashtaka DPP. Nilikuwa naomba tu kwa sababu ni suala ambalo linahusu maslahi ya umma *public interest* basi baadae kutokana na msimamo wa serikali hii kwamba siku zote inapiga vita rushwa hatua itakayofikiwa aliarifu Baraza hili hata kama ni mwakani tukijaaliwa.

Baada ya hayo Mhe. Mwenyekiti nasema tuendelee.

Kifungu 0601

Mhe. Subeit Khamis Faki: Mhe. Mwenyekiti suala la kesi ambazo kuwa ni kesi za misikiti lakini kesi hizi baadae ukaona kama zinahukunmiwa kwenye mahkama za kawaida, kwa hivyo nilitaka ufafanuzi kwa mfano, mfano kuna kesi kama iliyotokea karibuni jimboni kwangu ambapo wana kijiji cha Maziwa ng'ombe watu waligombana kwa msikiti lakini kesi ile ikenda Mahkama ya Wilaya ya Konde na mpaka sasa hivi kesi iko kwenye Mahkama ya Konde sasa nilitaka ufafanuzi kwa sababu inakuwaje kesi za misikiti zikahukumiwa katika mahkama zakawaida.

(Baraza lilirudia)

KUONGEZWA MUDA WA BARAZA

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti kwa kuwa majadiliano bado yanaendelea na kwa kuwa muda uliobakia ni mdogo wa kawaida hautoshi naliomba Baraza lako tukufu kwa kupitia kwako tuweke kanuni kando tuongeze muda hadi tumalize majadiliano yetu.

Mhe. Mwenyekiti: Wanaokubali hoja wanyooshe mikono, wanaokataa, waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)

KAMATI YA MATUMIZI

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Mwenyekiti nashukuru, Mhe. Mwenyekiti kwa mujibu wa Katiba yetu ya Zanzibar kifungu cha 100 kinasema kwamba Baraza la Wawakilishi linaweza likatunga sheria ya kuanzisha mahkama nyengine yoyote na mojawapo ni mahkama ya kadhi lakini nasema kwamba ni kwa mujibu wa taratibu na sheria ambayo imewekwa na sheria hiyo. Sasa mahkama ya kadhi inasema kwamba intashughulikia kesi ambazo ni za kiislam na katika shughuli za mirathi, ndoa na talaka na shughuli ya mambo ya watoto na vitu kama hivyo. Kesi anazosema Mhe. Mjumbe ni kesi za *criminal*, na kesi za *criminal* zote zinashughulikia na mahkama za kawaida. Sasa kwa mfano suala la msikiti, kweli ni suala la msikiti ikiwa mtu kenda kaiba mule kwenye msikiti hatumpeleki kwenye mahkama ya kadhi tutampeleka katika mahkama za kawaida. Ikiwa kenda kafanya fujo mule tunampeleka katika mahkama za kawaida na kesi ambayo ana-refer Mhe. Subeit nilivyopata habari mimi kwamba hao walioshtakiwa wamekwenda kufanya fujo ndani ya msikiti. Sasa kama ni kwenda kufanya fujo ndio shtaka, sasa kwenda kufanya fujo ndani ya msikiti huwezi ukapelekwa mahkama ya kadhi utapelekwa mahkama hizi za kawaida kwa sababu ile ni *criminal offence* ya kufanya fujo. Kwa hivyo ndio maana hata kama ni kesi ya msikiti lakini iko katika *criminal offence.*

Mhe. Subeit Khamis Faki: Mhe. Mwenyekiti nimemsikia Mhe. Abubakar na nimemfaham vizuri sana lakini hii kesi watu walikuwa wakigombania uimam, na imam anawekwana waumini wa msikiti wenyewe, kwa hivyo watu walikuwa wakigombaniana uimam. Sasa watu kama wanagombaniana uimam hawaijaba kitu, wala msahafu mule walikuwa wanagombana kwa uimam sasa mambo ya maimam ni mambo ya kadhi ninavyoelewa mimi. Sasa watu waligombana kwa uimam si kwa kuiba msahafu wala kitu.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Mwenyekiti mimi kosa hilo silijui, kosa ninalolijua ni lile ambalo nimepelekewa kwa mujibu wa taratibu zetu ni kwamba ambayo imepelekwa kule ni mashambulio kufanya ushambulizi katika msikiti. Sasa kama ni suala la kugombea imam na nini na nini hiyo tunaweza tukaichukua misingi mengine ya kupitia ofisi ya mufti. Lakini sasa

hii ni kesi nyengine na hiyo kama ni ugomvi wa maimam kama mtu anataka kusalisha mwengine hataki, hilo ni suala la mufti ambalo litakuwa baadae.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Mhe. Mwenyekiti, tuendelee.

Kifungu 0601 Ofisi ya Kadhi Mkuu	309,957,000
Jumla ya Fungu	3,583,000,000

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati bila ya mabadiliko yoyote)

FUNGU 15 OFISI YA MWANASHERIA MKUU ZANZIBAR

Kifungu 0201

Mhe. Makame Mbarouk Mshimba: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti nilipokuwa nachangia kwenye kifungu hiki niliwataka wote wawili kati ya Mwanasheria Mkuu na mwenyewe Mhe. Waziri nilinukuu Katiba ili kuangalia jinsi gani Manaibu Waziri wanayo haki gani ya kuweza kutujibu masuala yetu watu wa *back bancher* au wana uwezo tu wa kuchangia tu bila kutujibu hoja nilitaka ufafanuzi huo Mhe. Mwenyekiti ili na mimi niweze kuruhusu kifungu hiki kiendelee.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Mwenyekiti, katika mfumo wa serikali kuna Waziri, na kuna Naibu Waziri au mwengine ataita Waziri Mdogo, na kwa mujibu wa utaratibu ni kwamba Naibu Waziri kwa nchi nyingi za Jumuiya ya Madola huyu ni mtu ambaye anatakiwa ajibu masuala katika Baraza la Wawakilishi lakini hawezi kuingia katika *cabinet* au katika Baraza la Mawaziri. Anaweza akaingia pale ambapo anaalikwa lakini kama hajaalikwa hawezi kuingia. Sasa kwa maana hiyo ni kwamba suala lolote ambalo linamuhusu Waziri kwa sababu Waziri anapotoa kauli anatoa kauli ya serikali. Kwa hivyo suala lolote lilohusu Waziri, Naibu Waziri hawezi akalitoa kauli kwa sababu yeye hausiani na *cabinet.* Lakini kwa mujibu wa utaratibu wa mabunge ya *common wealth* ya Jumuiya ya Madola, Naibu Waziri anaruhusika kujibu maswali katika Baraza na kujibu maswali ya nyongeza na hayo yatakuwa ni majibu wa serikali kwa sababu ameruhusika kwa mujibu wa taratibu hizo.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Mwenyekiti, mimi nilinukuu Katiba na Katiba tunasema ndio dira yetu tunayoifuata kwenye serikali zetu. Nimemfahamu Mhe. Waziri anavyosema kuwa ameonesha mifano katika nchi za wenzetu na wenzetu wanakwenda katika mfumo wa ndani ya Katiba kama tunavyofanya sisi lakini bado Mhe. Mwenyekiti ningemuomba sana

Mheshimiwa wangu waziri ili niweze kumwachia aendelee, hebu anukuu au aangalie kifungu kidogo tu cha Katiba ambacho kinaonesha tamko hilo alilotamka yeye ili mimi nimpe ruhusa apate kuendelea. Mhe. Mwenyekiti naomba hiyo.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Sijafaham Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mshimba hebu rudia unalolitakia maelezo zaidi.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Mwenyekiti, nilimtaka Mheshimiwa wangu Waziri, Mheshimiwa hili suala naona halisikiki naomba tuendelee.

Kifungu 0201 Utawala Unguja	919,000,000
Jumla ya Fungu	919,000,000

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati bila ya mabadiliko yoyote)

FUNGU 35 OFISI YA MKURUGENZI WA MASHTAKA

Kifungu 0201

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, nilipokuwa ninachangia kuhusiana na bajeti ya Wizara ya Katiba na Sheria, sehemu ya Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka nilizungumzia mambo kadhaa mengine nashukuru kama yamepata maelezo, moja katika fungu la maendeleo likifika nitaliuliza, lakini kuna suala la maslahi nashukuru kwamba Waziri kwamba Waziri kalitolea ufafanuzi na naamini kwamba kwa sababu moja katika sifa ya saydina Abubakar ni uadilifu na mimi naamini atalisimamia kwa uadilifu hili.

La pili Mheshimiwa ambalo sikupata maelezo jambo nililonyanyukia hapa na hili nalisimamia kwa sababu ni Ofisi hii lakini majibu nadhani sijui atanijibu Waziri au Kaimu Waziri anayesimamia masuala ya fedha hapa. Niliuliza suala zima la uingizwaji wa fedha za OC katika Ofisi ya DPP kwamba Ofisi hii muhimu ambayo kama haifanyi kazi huo muhimili wa utoaji haki wa mahkama nao utakuwa unakwaza au unakwamishwa, uingizwaji wa fedha za OC umekuwa hauridhishi Mhe. Mwenyekiti na nikasema kwamba kwa mfano ukichukulia mwaka uliomalizika wa fedha bajeti yao ya OC ofisi hii ilikuwa ni 351,000,000 lakini mpaka wamemaliza mwaka mzima Juni wamefunga walichokipata ni 261,564,840 ambayo ni upungufu wa 89,435,160, sasa hili sijui kama ananijibu Waziri maana hizi ilipwaswa wapewe kwa sababu iko chini ya Wizara yake. Au serikali anayekaimu Waziri wa Fedha atusaidie

hapa, kwa nini Ofisi hii haikuingiziwa fedha inavyostahiki ili kuweza kutekeleza kazi zake ipasavyo, naomba maelezo.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Mwenyekiti ninamshukuru Mhe. Jussa lakini naomba Mhe. Jussa ajue tu kwamba fedha ambazo zinaingizwa si katika Ofisi ya DPP tu, katika Wizara ya Katiba na Sheria, katika Mahkama, katika Wizara nyengine na Idara nyengine zote zinategemea fedha ambazo zinapatikana kutoka Wizara ya Fedha na ndio maana Mhe. Mwenyekiti, hata Wizarani kwangu mimi zile fedha ambazo tuloomba hatukuzipata zote. Hata mahkamani ambako tulikuwa tunataka kuwalipa mashahidi na wale *assessor* hazikupatikana zote kutokana na kile kidogo ambacho kinapatikana kinagawiwa kwa kila pahala. Yaani fedha hizi ndio fedha ambazo zimepatikana kipindi hicho najua kwamba kwa mujibu wa utaratibu wetu na matumizi yetu ya DPP kwa sababu ya shughuli nyingi zilizopo hazitoshi, lakini kwa sababu hazitoshi sisi si peke yetu ni sote. Kwa hivyo mimi kama ni mtendaji mkuu wa Wizara nakubali kwamba fedha ni kidogo zile zilizoingizwa na hatukuzipata zote lakini pia ninamuomba Mhe. Jussa ajue tu kwamba fedha hizi *almost* ni kwa serikali nzima hazikupata zile ambazo wameomba, zimegaiwa kwa mujibu wa kile ambacho kimepatikana. Na safari hii tumejaribu kuomba ili tutachopata ili tuendeleza zile shughuli zetu ambazo tumezikusudia kwa mwaka huu na kumalizia zile za mwaka jana.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti ndio maana niliponyanyuka nilisema sijui kama anijibu yeye ama anayekaimu Waziri masuala ya fedha. Kwa sababu Mhe. Mwenyekiti yeye anapaswa kuwa ndio mnufaika, kwa hivyo yeye kunijibu kwamba ni utaratibu wa serikali sawa lakini tunachokipia kelele Mhe. Mwenyekiti hapa ni ule utaratibu wa Wizara ya Fedha kwamba kuna Wizara utakuta uingizwaji wake au Ofisi fulani ni mzuri, Mhe. Mwenyekiti tutakuja kuona huko mbele si kama zinafanya kazi zilizokusudiwa nyengine zinatafunwa tu, lakini Ofisi kama hii muhimu Mhe. Mwenyekiti ninayo *brackdown* hapa, ungetegemea ofisi hii wastani wake ni kama milioni thalathini kwa mwezi lakini kuna miezi hapa Mheshimiwa ina milioni kumi kuna miezi ina milioni nane katika mwaka uliopita wa fedha. Sasa Mheshimiwa kweli ofisi ambayo inashughulikia uendeshaji wa mashtaka kwa nchi nzima kwa Zanzibar unapomuingizia OC milioni nane au milioni kumi katika fungu ambalo wastani wake ulipaswa liwe milioni thalathini, kweli tunaitendea haki ofisi hii.

Kwa hivyo mimi nasema hapa ninapata tabu kidogo kwa sababu najua utaratibu wa serikali inajibu kwa pamoja Mhe. Waziri atanambia ndio utaratibu lakini ndio huo tunaoukataa. Kwa sababu katika bajeti hapa tuliambiwa kuna fedha imebakia inarudi serikalini, lakini kama huku kuna Ofisi kama hizi hazipati haki zake zinavyopaswa. Mheshimiwa, Katibu wa

Baraza la Wawakilishi mara nyingi anatwambia yeye kwamba yeye anajitahidi mara nyingi akenda anapata anachopangiwa. Sasa hawa vile vile nimetoa mfano tu hawa vile vile ni muhimu kwa sababu hawa wanasimamia utoaji wa haki hawa wakikamilishiwa kazi zao Mhe. Mwenyekiti ndipo na kazi za mahkama zitakwenda vizuri. Sasa nilikuwa naomba nisaidiwe, kwamba sijui nani anakaimu hili suala kwa nini katika Ofisi hii wafike kutoka wastani wa milioni thathini waingiziwe milioni nane mpaka milioni kumi tena si kama ingelikuwa mwenzi mmoja miwili ukasema kwamba hii ni axceptional aa kuna miezi haipungui sita Mhe. Mwenyekiti utaratibu ndio huu, milioni kumi, milioni nane naomba maelezo Mheshimiwa niridhike.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti ninafikiri Mhe. Waziri alipokuwa anajibu alizungumza vizuri tu kwamba serikali tungependa yale makisio tuwapatie kama walivyoomba au walivyotaka. Lakini kutokana na tatizo la fedha, inabidi tukose hasa kutiliwa fedha asilimia 100. Sasa kuna utaratibu ambao unafanya na Wizara na Fedha na Wizara zote zimekubaliana pamoja, tunauiita MTEF, *Medium Term Expenditure Frame work* kila Wizara wanatayarisha activities zao na makisio yao wanayotaka kwa kipindi cha miezi mitatu, miwili inayofuata wanapeleka Wizara ya Fedha vile vipaumbele vyao halafu wanaingiziwa pesa lakini kutokana na makusanyo yaliyopo. Kwa hivyo huo ndio utaratibu unaofuatwa. Tatizo kwamba yale makusanyo tu kwa kile kipindi ambacho kinatakiwa kiingizwe fedha kama zipo hakuna tatizo. MTEF ile asilimia 100 watapewa. Kwa hivyo tatizo ni hilo tu, keki yenyewe tunayokusanya ni ndogo.

Kwa hivyo ninaomba kumuhakikishia Mhe. Jussa akiangalia ukurasa 53 utakuta kuwa Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka jumla kuu pale ni asilimia 70 ukurasa 53 kuna jaduweli nzuri tu pale inaonesha kiambatanisho namba moja muhtasari wa upatikanajiwa fedha na matumizi 2012/2013 ukiangalia ukurasa wa 53 Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka na zote nyengine zimeonesha ile *trend* iliyopo. Kwa hivyo si Wizara hii hata Wizara zote hii ndio hali halisi. Ahsante.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti sitaki niurefushe mjadala lakini nikisoma alichonielekeza Mhe. Kaimu Waziri anayeshughulikia masuala ya fedha itakuwa kinanipotosha, kwa sababu hii ni jumla kuu ya fedha zote, ruzuku la maendeleo. Lakini namuomba aangalie matumizi mengineyo ndio ninalolizungumza mimi hapa OC ni asilimia 59. Na kwa mujibu wa takwimu iliyosomwa zinaingia akilini kwa sababu kama bajeti yao ya OC ni 351 milioni wakaingiziwa 261,000,000 kukawana tofaauti ya 89,000,000 inaingia akilini kwamba ni asilimia 59 kwa asiisome kwa pamoja nazungumzia fungu mahsusi la OC.

Mhe. Mwenyekiti mimi nilikuwa nadhani ili nisirefushe mjadala nitaki uhakikisho tu wa Kaimu Waziri wa Fedha kwamba utaratibu huu kwa mwaka huu tunaouanza huu hautojirejea tutaona kwamba Ofisi hii ikipewa kipaumbele kama ofisi nyengine ambazo zinahudumia haki za watu. Naomba uhakikisho huo uniruhusu niendelee Mheshimiwa.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti tunachukua ahadi hiyo tutajitahidi kadiri keki inavyopatikana na Ofisi hii tuione kwa jicho la huruma. Ahsante.

Kifungu 0201	Utawala Unguja	888,520,000
Kifungu 0202	Kituo cha Mafunzo na Utafiti wa Sheria	80,000,000
Kifungu 0301	Ofisi Kuu Pemba	214,480,000
Jumla ya Fungu		1,183,000,000

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati bila ya mabadiliko yoyote)

FUNGU 36 WIZARA YA KATIBA NA SHERIA

Kifungu 0011	Wakala wa Usajili wa Biashara na Mali	273,007,000
Kifungu 0012	Wakala wa Usajili wa Biashara na Mali Pemba	15,996,000
Kifungu 0301	Ofisi Kuu Pemba	196,575,000
Kifungu 0401		

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa muda mrefu nimekuwa nikipiga kelele kusimama kwa suala hili la mwaka wa kiislam karibu mwaka wa tatu tokea kuingia katika Baraza hili la Wawakilishi, imani yangu Mhe. Mwenyekiti umerudi Maka juzi na pembeni yako Katibu wetu atakuongoza vizuri kwa suala hili na nisije nikaambiwa hili suala na nisije nikaambiwa hili suala liko kwa Makamo wa Pili wa Rais kama wapo nilikuwa naomba nipate ufafanuzi wananchi huko wanata suala hili lipate ufafanuzi kwa muda mrefu, kuhusu tarehe ya kiislam lini itaanza.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Mwenyekiti naomba Baraza lako lielewe kwamba katika Baraza hili tunafuata utaratibu na suala hili Mhe. Mjumbe alilileta katika masuala ya kawaida, na mimi nikamjibu kwa mujibu wa sheria namba 7 ya 1984 *interpretation of laws act* inasema kwamba mambo ya *holiday* au siku za mapumziko hilo ni suala kwa wakati ule alikuwa ni Waziri Kiongozi. Lakini kwa sababu ya mabadiliko sasa itakuwa ni Makamo wa Pili wa Rais. Sasa mimi kama Waziri sina *mandate* ya kusema siku fulani iwe ni *holiday*, mimi ninaweza nika-*suggest* na sisi tumeshapita

katika hatua zote hizo tumepita tukakaa na mashekhe wangu na maulamaa wote tukakubaliana baadhi ya mambo sasa hayo lazima tuwapeleke kwa wakubwa wetu, ambao hao wakubwa Makamo wa Pili wa Rais kama yeye ataona kwamba inafaa au kuna matatizo na nini baadae mtu ambaye kwa mujibu wa sheria ile ameruhusiwa kutangaza siku ya mapumziko ni Rais peke yake, sasa si suala letu ni suala la Rais.

Sasa hayo nilimuelekea katika masuala na majibu alipouliza. Sasa mimi sina uwezo tena wa kujibu suala hili kwa sababu halipo katika wanaita *province* yangu, halipo katika mamlaka yangu. Mhe. Mwenyekiti ninakushukuru.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Kwa masikitiko makubwa sana Mhe. Mwenyekiti lakini hata nikakaribia kulia usije ukashangaa ninafikiri asubuhi nilipokuwa nnasema hapa niliwasifu sana mawaziri leo inapokuwa pana hoja, jana waziri akapata kigugumizi mawaziri wanne walinyanyuka jana. Ninafikri serikali inatusikia kwa hivyo mnadhim anaweza kulijibu hili suala serikali inawajibika kwa pamoja. Mimi hapa sisikii lolote Mwenyekiti kwa siku yetu ya leo.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Jaku ilikuwa utupe maelekezo nini cha kufanya kwa sababu sasa hivi umenun'gunika lakini kama tuendelee basi tuambie tuendelee na hilo...

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Kaimu Mnadhimu wa Serikali atoe jawabu.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti, mimi sio Kaimu Mnadhimu wa Serikali, mimi ni Kaimu wa Waziri wa Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais, kwa hivyo sina kauli ya kutoa zaidi ya lile ambalo Mhe. Waziri, amelisema.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, hapa sasa hivi mimi nimeshanganyikiwa, hili suala la muda mrefu mimi Mawaziri wapo na Kaimu yupo mimi nataka jawabu lifahamike ili wananchi watusikie.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Jaku, kwa maelezo aliyoyaeleza Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria, nafikiri tumemfahamu vizuri sana, hilo haliko kwenye mamlaka yake na kwa kuwa hapa hakuna yoyote ambaye ana mamlaka hayo jibu haliwezi kutoka. Kwa hiyo mimi nafikiria kwamba labda tuendelee na Mhe.

UTARATIBU

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, suala hili na mimi nililichangia lakini niliamua kuliacha kwa sababu taratibu akishakuzungumza mmoja inatosha, lakini maelezo yake kidogo yananipa tabu nataka ufafanuzi zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mujibu wa Katiba ya Zanzibar, Ibara ya 43(5) naomba niisome:-

"Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, chini ya mamlaka ya Rais, ndio itakuwa na uwezo wa kufanya maamuzi juu ya sera za Serikali kwa ujumla na Mawaziri chini ya uongozi wa Makamo wa Pili wa Rais, watawajibika kwa pamoja katika Baraza la Wawakilishi kuhusu utekelezaji wa shughuli za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar".

Sasa Mhe. Mwenyekiti, suala hili tumeliuliza hapa mimi na mwenzangu katika Wizara hii, kwa sababu Wizara hii ndio inayosimamia shughuli za dini ya kiislamu, Ofisi ya Mufti iko hapa, Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana iko hapa, Mahakama za Kadhi zipo hapa. Lakini Waziri keshajibu vya kutosha kwamba kwake lishaondoka, yeye kwa hatua zake ashakamilisha. Sasa yule aliyempelekea yeye ndio nasema kwamba chini ya msingi wa *collective responsibility*, dhana ya uwajibikaji wa pamoja, Serikali humu ndani Mhe. Mwenyekiti, haiwezekani ikawa haina msemaji wake na ukituambia kwamba mtu usikaimu Mnadhimu, ukikamata nafasi ya Waziri wa Uratibu, ambayo ni Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais, maana yake vile vile umekaimu shughuli hizo, kwa hivyo sisi hatujui kama ni Mnadhimu au si Mnadhimu, lakini ninachotaka kusema kiutaratibu Msemaji wa Serikali lazima awemo humu na hata kwa maana ya Msemaji Mkuu, hata Makamo wa Pili akiwa hayupo anatakiwa akae mtu ambaye atajibu kwa niaba yake, ndio dhana ya uwajibikaji wa Bunge dunia nzima katika dhana ya Jumuiya ya Madola. Kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti, tusipigwe dana dana tujibiwe, Serikali itujibu.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Mjumbe wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Jaku, kaleta fikra, wazo ndani ya Serikali, nafikiri hizo wazo si baya, sasa tuje tulizungumze, tulizingatie katika Serikali,. lakini kutuambie tutoe jawabu hapa ndio hapana nafikiri si sahihi. Mimi nafikiri Mhe. Mwenyekiti, hilo wacha alilete, tuna taratibu zetu kwenye Serikali, alilete kwenye Wizara, Wizara kuna vikao vyake, vitaanza itazungumzwa mpaka baadae tutasema kwamba kweli inafaa au haifai, kama haifai kwa sababu gani. Kwa hivyo mimi namuomba sana Mhe. Jaku, alilete hilo suala katika Wizara, yeye ni mjumbe wa Kamati, tumia Kamati za Baraza tulizungumze kwenye Kamati, tulipeleke kwenye Wizara itazingatiwa ndani ya Wizara au ndani ya Serikali. Mimi nafikiri huo ndio ushauri wangu,

nimuombe sana Mhe. Jaku, kwa leo anatuambia tutoe jawabu ndio au hapana si sahihi, alilete tulizungumze tulijadili basi hapo tena tutampa jawabu.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, nasimamia bado utaratibu na kwa sababu naingia habari kwa maana mbili. moja kwamba na mimi nilichangia lakini lakini nasimamia ule ule utaratibu ule niliouleza Mhe. Mwenyekiti. Ni kwamba Serikali hapa inawajibika kwa pamoja Mhe. Mwenyekiti,

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Jussa, aliyeuliza suala hili hapa katika kifungu hiki ni Mhe. Jaku, kwa hiyo Mhe. Jaku, kwanza ndio ana haki ya kuuliza zaidi.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, nilinyanyukia hoja

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Jusa, ngojea tumalizane na Mhe. Jaku, halafu utakuja wewe.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, hili suala kama fikra na mawazo ni miaka mitatu, huyo mtoto hata akazaliwa hutambaa, akatweta, akapata mguu, akachanganya na akaenda mbio. Miaka mitatu ni mingi, bora hili suala Serikali iseme hatuliwezi au hatulitaki wananchi wakafahamu.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Mwenyekiti, nafikiri yale aliyoyasema Mhe. Jussa, alisoma kifungu cha katiba ambacho kinafanya Serikali kwa maana ya Mawaziri kuwajibika kwa pamoja, nafikiri iko sahihi. Na Mhe. Jaku, ameleta hoja ya kutaka Zanzibar kuwa na Kalenda ya mwaka wa kuadhimisha mwaka wa kiislamu na Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria alisema vizuri sana na alisema kwa mujibu wa taratibu za kiserikali zinavyokuwa, kwa hiyo mimi siwezi kuwa na uhakika kama hili jambo ni mwaka wa tatu tokea Mhe.Jaku, amelileta.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri wa Katiba alivyosema ni kwamba yeye kama Wizara inayohusika na hizi sekta, amelipokea na amelipeleka Serikalini, tunakubali kwamba Mawaziri hapa tunawajibika kwa pamoja. Mimi niseme tu kwamba, kwa mujibu wa maelezo ya Mhe. Abubakar, maana hilo jambo sasa liko katika *pipe line* ya kuzungumzwa na kushughulikia na Serikali na jambo lolote linalokuwa geni linahitaji kupangwa vizuri na kueleweka vizuri na kukubalika ili liweze kuwekwa katika kalenda za sherehe za kitaifa. Sasa mimi niwaombe Waheshimiwa Wajumbe na Mhe. Jaku, kwamba kwa kuwa limeshafika Serikalini atuachie tuende tukalizungumze na hatimae tutaleta jibu ndani ya Baraza la Wawakilishi, huo ndio utaratibu.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nadhani kama ni suala la uwajibikaji wa pamoja

mimi nikiwa kama Waziri wa Utawala Bora, nasema ni sahihi wanavyosema na Waziri wa Katiba na Sheria kasema sahihi na sisi kama Serikali tunasema tunalishughulikia na taarifa rasmi tutaileta Barazani. Ahsante sana.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Nina matatizo Mhe. Mwenyekiti, mimi nimeshazoea humu ndani, *experience* yangu inavyonipa kwamba kila siku Serikali inasema imo mbioni wakati wote tu. Sasa nambie lini tusije tukapoteza muda hapa, hili jambo litaletwa kesho, kesho kutwa, mwezi tumalize suala hili, mimi nataka niambiwe lini jambo hili litaletwa kwenye Baraza, maana mpaka katika *order paper* kikao kilichopita imetiwa na kwa ghafla ikafutwa, mimi nipewe huo muda tu ni lini hakuna tatizo.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Mwenyekiti, nafikiri Mjumbe ajue kwamba Serikalini kuna utaratibu wake, huwezi hapa ukasema kesho kwa sababu utaratibu ni kwamba lazima uandae waraka upeleke katika cabinet ambapo ni Baraza la Mapinduzi. Mimi sijui wala hapana hata mmoja anaejua hapa kwamba Baraza la Mapinduzi litakaa lini kuzungumzia suala hili. Na kabla hujapeleka katika Baraza la Mapinduzi lazima upeleke katika Kamati ya Makatibu Wakuu, hatujui sote hapa Kamati ya Makatibu Wakuu, itakaa lini kuzungumzia suala hili. Sasa suala ni kwamba hili suala limeshakwenda Serikalini na hata lile suala alilosema Mhe. Jussa, *collective responsibility, collective responsibility* inasema kwamba kama ni Mawaziri akisema mmoja hiyo ndio *responsibility* yeye anasema kwa niaba ya wote, hatuwezi sote hapa tukanyanyuka tukasema suala moja,. akisema Mhe. Mwinyihaji hapa ndio imeshasema Serikali. Kwa hiyo hapa sisi sote *we are responsibility* kwa Serikali.

Mhe. Mwenyekiti, sasa tunachosema ni kwamba, ni kuwa kuna utaratibu wake wa suala hili. Mimi ni kama Waziri wa Katiba na Sheria nimeshapeleka kwa Makamo wa Pili wa Rais, na kumwambia, kule lazima kuandaliwe *paper* iende kwa Makatibu Wakuu, waijadili, halafu pape hiyo iende kwa *cabinet* ijadiliwe halafu ndio itajulikana kwamba linakubaliwa au halikubaliwi. Kwa hivyo kusema hapa kwamba lini hiyo haiwezekani Mhe. Mwenyekiti, lazima tukubaliane ukweli, utaratibu tutakuwa tumekiuka, tutasema keshokutwa Mwenyekiti wa *cabinet* ni Rais, sisi tutamwambia Rais lazima aitishe mkutano kesho haiwezekani.

Mhe. Mwenyekiti: Mimi nafikiria Mhe. Jaku, tukubaliane na Waziri na maelekezo yake ambayo ameyatoa, hili jambo ni muhimu na muhimu kwetu sote, mimi naunga mkono kabisa hoja yako, lakini nafikiria kwamba vile vile una uwezo wa kuleta hoja binafsi ili iwe na mshughulikiaji maalum. Mhe. Jaku, baada ya hapo nafikiri tutaendelee.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: sawa Mhe. Mwenyekiti, lakini nitajiandaa kuleta hoja binafsi panapo uhai.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, kuhusu utaratibu tu nilikuwa sina haja ya kunyanyuka lakini kwa sababu maelekezo uliyoyatoa na mimi nachukulia kwamba ni muongozo wako wa kiti kwamba ije kama hoja binafsi na bila ya shaka ikikubaliwa Baraza hili itakuwa Serikali haina uchaguo tena ni kutekeleza matakwa ya Baraza hili na mimi naamini kwa sababu sisi tuliokuwemo humu ni waislamu itapita kwamba siku iadhimishwe. Lakini nilitaka kunyanyuka kidogo Mhe. Mwenyekiti, kila mmoja anamtizamo wake mimi tafsiri ya Mhe. Abubakar ninaikubali lakini inanipa mashaka, kuhusu suala la dhana, nimezungumza katika utaratibu nafikiri rikodi zitakaa vizuri tu Mhe. Mwenyekiti, hii inaingia katika *Hansard* tutakuja kuhukumiwa kesho na kesho kutwa.

Mhe. Mwenyekiti, dhana ya kuwajibika kwa pamoja mimi naikubali alivyosema yeye Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria, kwamba akisema mmoja ni kama ni sawa sawa na Serikali imesema, ninachokizungumza mimi kuwa suala hili yeye ameshajivua, kwa sababu kuna masuala mawili kuna suala kwamba kuna mgawanyo wa madaraka ndani ya Serikali, kwa hivyo kuna Wizara inayosimamia suala fulani kisekta, halafu inapokuwa Wizara ile Mhe. Mwenyekiti, imekwamba upande wake inalipeleka kwa Mkuu wa Shughuli za Serikali kwamba lipate maamuzi ya Serikali kwa ujumla wake ndio pale tunataka kauli ya Serikali kupitia Msemaji Mkuu ambaye kwa kawaida ni Makamo wa Pili wa Rais, na akiwa hayupo atakuwa na Msemaji wake. Kwa hivyo nataka niweke rikodi hiyo sawa tu Mhe. Mwenyekiti, kwamba sikatai wazo la msingi kwamba Waziri mwenye sekta akishasema ni Serikali imesema, lakini akishasema kwamba katika sekta yake limeondoka kalipeleka katika ofisi za mkubwa maana yake ofisi ya mkubwa huyu kiserikali nayo iwajibike, na ndio maana kifungu cha katiba kikasema Mawaziri chini ya Makamo wa Pili wa Rais, anawajibika kwa pamoja katika chombo hichi. Nataka niweke rikodi hiyo tu sawa, na baada ya hapo tuendelee.

Mhe. Omar Ali Shehe: Mhe. Mwenyekiti, wakati nachangia niligusia suala la rasimu ya katiba. Na katika hapa kwa kweli kwanza naomba niipongeze Serikali kwa msimamo wake wa kwamba Serikali yenyewe haina msimamo lakini Serikali itafuata msimamo au itasimamia msimamo wa wananchi. Wakati nachangia Mhe. Mwenyekiti, nilimuuliza Mhe. Waziri, kwamba msimamo wa wananchi katika suala hili au katika mchakato wa suala hili unapatikana katika *stage* 3, *stage* ya kwanza ni ile iliyopita ya wananchi kutoa maoni yao, *stage* ya pili ni hii ambayo tutaingia karibuni ya kuundwa kwa Mabaraza ya Katiba, na *stage* ya tatu ni ile ya mwisho ya kwenda Bunge la Katiba na baadae tutaingia kwenye kura ya maoni.

Mhe. Mwenyekiti, katika hatua hii kwa sababu Serikali ilisema itasimamia msimamo wa wananchi, na msimamo wa wananchi kwa sehemu hizo tatu. Sasa nilimuuliza Waziri, na bahati mbaya Waziri hakunijibu, ni vipi Serikali sasa inaratibu misimamo hiyo ya wananchi katika sehemu hizo tatu. Lakini la pili ni katika hatua gani au ni pahala gani sasa Serikali itaibuka na kueleza msimamo wake kwa niaba ya wananchi. Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri, hakunijibu na hapa naomba jawabu.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Mwenyekiti, ni kweli kwamba katika utaratibu huu wa rasimu una sehemu tatu, kwanza ni wananchi kutoa maoni yao hiyo tayari, lakini hivi sasa tunakabiliwa na Mabaraza, na baadae kuna Bunge la Katiba na halafu mwisho itakuwa ni kura ya maoni. Katika *state* hii kama walivyosema wenyewe Tume ya Kuratibu Katiba hii ni kwamba sasa katika Mabaraza lengo la kupita katika Mabaraza ni kutaka kujua kama kweli yale maoni ya wananchi waliyoyatoa ndivyo yaliyomo katika rasimu. kwa hiyo bado hiyo itakuwa ni sehemu ya maoni ya wananchi na baada ya hapo Wawakilishi, Wabunge na wengine wana majukumu hasa Wawakilishi na Wabunge kwenda katika Majimbo yao kutaka kujua au kupata yale maoni hasa waliyokubaliana. Kwa sababu wao watakuwa ni Wajumbe wa Bunge la Katiba wao sasa watawakilisha maoni hayo ya wananchi kwa utaratibu uliowekwa kwa sababu wao ni Wawakilishi wao katika Bunge la Katiba. Baada ya hapo litakalokubaliwa pale katika Bunge la Katiba hayo ndio matakwa ya Wawakilishi na matakwa ya wananchi. Kwa hivyo Serikali hapo ikishakujua haya ndio matakwa yao bila ya shaka na Serikali nayo itakaa na kusema kwamba haya ndio matakwa ya wananchi na sisi kama ni Serikali itabidi tuyasimamie matakwa yale.

Mhe. Omar Ali Shehe: Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli pengine ni makosa ya ufahamu kwa sababu hoja ya wananchi, wananchi walitaka kwamba katika hatua hii ya mchakato kwa sababu ukisema Serikali kusimamia ni katika suala hili, si suala la kusubiri mwisho tena Serikali ndio ije ijitokeze, mwisho hata Serikali itakataza na itakuwa ndio basi. Tulidhani kwamba katika hatua hii za mchakato kwamba ifike pahala basi Serikali iweze kujitokeza na kusema kwamba haya ndio maoni ya wananchi, lakini sasa kusema kwamba suala hili hadi wananchi warudi walipigie kura ndio Serikali isimamie nadhani Serikali bora ifike pahala iseme kwamba sisi hatuna dhamana kama hili tujuwe kwamba Serikali haina dhamana katika hili waachiwe wananchi waendelee na utaratibu huu.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Mwenyekiti, Serikali haiwezi katikati kuingilia suala hili, kwa sababu hivi sasa kwa mfano Serikali ikitoa maamuzi yake itawa-*influence* wananchi na hilo ndilo tulokuwa tunakataa,

tunataka maoni ya wananchi wenyewe watakachosema na hio ndio sheria inavyosema, kwa sababu tukiingilia katikati hivi sasa kitakachosemwa na Serikali wananchi itabidi wakichukue na sisi hatutaki tuwa-*influence* wananchi. Kwa hivyo wache wananchi waseme, wakubaliane wakishakukubaliana watatwambia hichi ndicho tunachokitaka baada ya kufika huko kwenye utaratibu wa Mabaraza yote, wakishakutwambia haya ndio maoni ya wananchi ni jukumu letu sisi Serikali kusimama na matakwa ya wananchi. Kwa hiyo ninachotaka kusema Mhe. Mwenyekiti, ni kwamba Serikali hivi sasa haitozungumzia suala lolote kuhusu katiba kwa sababu tukifanya hivyo tutawa-*influence* wananchi, hatutaki tuwa-*influence* wananchi.

Mhe. Omar Ali Shehe: Mimi Mwenyekiti, nadhani katika hili maadam Serikali ishasema kwamba haitowa-*influence* wananchi katika hatua hii basi sina tatizo, basi sasa tunafahamu kwamba Serikali katika hatua ya mwanzo hadi ya mwisho hawatoli- *intervene* suala hili. Nashukuru tuendelee Mhe. Mwenyekiti.

Mhe.Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Mwenyekiti, nafikiri kwa rikodi ya *hansard* hatujasema kwamba Serikali hatuta- *entertain* hilo, nilichosema ni kwamba Serikali hatuto-*interfere* hivi sasa, hatutawa-*influence* wananchi hivi sasa, baadae wananchi wakishatwambia hichi ndicho tunachotaka hapo ndipo Serikali itafuatilia.

Kifungu 0401	Idara ya Mipango, Sera na Utafiti	184,152,000/=
Kifungu 0501	Ofisi ya Mufti	

Mhe.Jaku Hashim Ayoub: Nilimwambia Mhe. Waziri, kuna msikiti kule Mwanakwerekwe umefungwa na mtu kashinda katika Mahakama Kuu ya Zanzibar na Mahakama ya Rufaa Tanzania, nikamwambia ikisha Mahakama haifuatwi nani atafatwa. Mhe. Waziri, hilo hukuwahi kulizungumza naomba ufafanuzi wako na *judgment* ninazo hapa.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Mwenyekiti, suala hili nimelizungumza lakini naomba radhi kwa sababu nili-*confuse* na ile aliyosema na nikamtaja Mhe. Salmini na Mhe. Salmini akanyanyuka akasema si suala hilo, mimi nikamwambia ni kweli. Nikamtaja Mhe.Hija, na kama si yeye basi naomba radhi lakini suala hili nimeshalizungumza na utaratibu ni kama hivyo nilivyozungumza ni kwamba *judgment* mimi ninazo. Huyu mtu alikuja juzi wakati wa Baraza hili kuniona asubuhi, nikamwambia aje mchana, akaja mchana, alipokuja mchana akaniletea makaratasi mengi akasema niyasome nimpe maamuzi hapa hapa, nikawambia hivyo sifanyi,

niletee barua, unipe maelezo yako yote, halafu mimi nitalitizama, basi yule mzee akatoa maneno yake na mengine yaliyokuwa si ya kiungwana kabisa lakini tukabeba sisi ndio jukumu letu, alikuwepo na mtu mwengine, yule ndio akamzungumza akamwambia ah! anavyosema Waziri ni hili na hili yule mwengine akasema basi tutaleta, mpaka hii leo mchana nimekwenda ofisini kwangu hawajaleta. Sasa kama hawajaleta mimi sina la kufanya, walete maelezo yao, walete ushahidi wao wote basi tutatizama, kama kuna haki yake tutampa kama hakuna mimi nitamwambia kwamba huwezi kupata.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, *judgement* tayari imeshatoka Mahakama Kuu ya Zanzibar na Mahakama ya Rufaa Tanzania na vitu wanavyo, sasa anataka kitu gani Mhe. Waziri, uthibitisho wote upo.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Mwenyekiti, ni kweli *judgment* ipo, lakini alipoleta kwangu mimi ni *judgment* ya Mahakama ya Rufaa, hiyo ni kubwa, mimi nikamwambia siwezi kusoma hapa hapa nikatoa maamuzi, niletee na vielelezo vingine, *judgment* ya Mahakama ya Rufaa inasema kwamba ina-*pass* yale maamuzi ya Mahakama Kuu. Sasa kisheria unaposema una-*pass judgment* ina maana yale mambo yaliyokuwepo nyuma yanabakia vile vile, mimi nataka kujua hayo mambo ya nyuma ni mambo gani, ndio nilivyomwambia alete mambo yake mengine yote nijuwe hayo mambo ya nyuma yaliyopelekwa huko Mahakamani ni yepi. Sasa ukiniletea *judgment* ya Mahakama ya Rufaa tupu siwezi kuamua mpaka nijue huko nyuma kuna kitu gani, ndio ninataka nijue, sasa huyu hataki hajaleta mpaka leo, kama hataki au hajaleta mpaka leo mimi siwezi kumshauri na wajibu wangu mimi kushauri baada ya kupata vielelezo, sasa kama hataki kuleta vielelezo hatuwezi kumshauri.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub*:* Kwa vile Waziri, kakiri akipelekewa vielelezo atalifanyia kazi na mimi nitajitahidi kumpelekea vielelezo naomba tuendelee.

Mhe. Fatma Mbarouk Said: Mhe. Mwenyekiti, kwanza niseme kwamba Mhe. Waziri, kajibu hoja nyingi, lakini kwa bahati mbaya mimi nilichangia kwa maandishi wala hakunitaja, lakini nilikuwa na masuala yangu hapa madogo tu wala si makubwa, ilikuwa kuhusu kwanza kwa Mufti wetu alimwagiwa tindi kali na akaumizwa na kwa bahati kapelekwa matibabuni, nikamuuliza kwamba kuna posho lolote ambalo anasaidiwa angalau lile posho la kupata maumivu. Halafu na jengine kwamba kaeleza kwamba kuna Maktaba ya Kiislamu imeanzishwa lakini hakusema iko wapi, kwa hivyo kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Amani nilikuwa nataka kujua hiyo Maktaba iko wapi, sisi tunataka tukasome, tunataka tukajielimishe mambo mengi. Hivyo naomba Mhe. Waziri, ingawaje hakunitaja katika waliochangia kwa maandishi na mimi nilichangia kwa maandishi, naomba majibu.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Mwenyekiti, ni kweli Mhe. Fatma, alileta kwa maandishi na maelezo yake niliyasema yapo hapa lakini nilighafilika, kwa hivyo kwanza namuomba radhi. La pili ni kwamba kweli alisema mambo hayo mawili kwanza Maktaba ya Kiislamu ipo katika Ofisi ya Mufti, kwa hiyo tunamkaribisha yeye na wengine. Pili kuhusu posho la maumivu hii kidogo ni tatizo, kweli mwenzetu, shehe wetu Soraga alipata matatizo kwa bahati Serikali ikachukukwa juhudi kubwa kumpeleka India kwenda kutibiwa, akarudi na aliporudi baadae akenda tena kutizama hali yake, kwa hiyo ameshakwenda mara mbili na hivi sasa Wizara yangu bado inaendelea kumshughulikia kwa mambo ambayo yanahitajiwa, kwa sababu yule ni muislamu mwenzetu, kwa hiyo linapotokea basi tunajitahidi kusaidia. Lakini tukiweka hakika kwamba kila mtu anayeumia katika shughuli hizi za mfanyakazi wa Serikali apewe posho maalum tutakuwa tunajifunga vibaya, lakini mimi nafikiri utaratibu mzuri ni Wizara inayohusika kama Wizara yangu ya Katiba na Sheria hivi sasa tunamhudumia kwa mambo mengi tu. Kwa hivyo tukifanya hivyo nafikiri tunaweza tukafika pahala pazuri.

Lakini tukisema kwamba tuweke posho maalum na wengine itakuwa watu chungu mzima Serikalini wameumia, kwa hiyo tukisema tuwape posho maalum tutakuwa tunafungua mlango mkubwa sana ambapo pengine baadae Serikali itashindwa kuubeba. Lakini mimi naamini kwamba Wizara inayohusika kwa sababu yule ni mwenzao ni vyema kuendelea na mpango ambao tunaoendelea nao pale ambapo ana matatizo sisi wenyewe tunakwenda tunamtizama wakati mwengine tunamsaidia kwa chochote na tunatizama baadhi ya mambo ambayo kwa kweli anastahiki kupewa.

Mhe. Fatma Mbarouk Said: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, nimeridhika na majibu ya Mhe. Waziri, naomba tuendelee.

Kifungu 0501	Ofisi ya Mufti - Unguja	375,124,000/=
Kifungu 0502	Ofisi ya Mufti - Pemba	110,542,000/=
Kifungu 0601	Idara ya Utumishi na Uendeshaji	591,141,000/-
Kifungu 0701		

Mhe. Salma Mohamed Ali: Mhe. Mwenyekiti, wakati nachangia nilimuomba Mhe. Waziri anifahamishe vigezo vinavyotumika au vilivyotumika katika kugawa zaka katika wilaya. Kwa sababu kuna wilaya nyengine zimepata vikundi vingi na wilaya nyengine kidogo, wilaya nyengine zimepata watu wengu na nyengine zimepata watu kidogo. Mhe. Mwenyekiti, naomba nipate ufafanuzi zaidi.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Mwenyekiti, ni kweli Mhe. Salma mbali na mambo mengine aliuliza hayo, lakini katika kujibu pia nilijibu lakini kwa kifupi. Kwa sababu nina *list* hapa a mambo mengi sana. Kwanza nina *list* ya masikini na mafukara ambao wao wamepata shilingi milioni mia tatu na kitu, kuna watu ambao wanafanya kazi za Amir yaani shilingi 800,855,000; kuna kuzitia nguvu nyoyo za walioingia katika Uislamu ambao pia nilielezea hapa, kuna shilingi 3,782,000; kuna kukombolewa utumwani nafikiri nilizungumza, kukombolewa utumwani sio utumwa ule wa zamani tunaoujua, utumwa wa madawa ya kulevya ni moja katika utumwa. Kwa hivyo, hawa tumetoa shilingi 17,700,000; wenye madeni hakuna kuna mambo ya kidini shilingi 144,000,000 na wasafiri walioharibikiwa hamna. Jumla ya fedha tulizotumia hapa ni shilingi 476,471,200.

Halafu kuna vikundi Mhe. Mwenyekiti, Wizara ya Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika tuliwapa shilingi 303,000,000 na hizi waligawa katika vikundi mbali mbali. Mhe. Waziri aliwaambia Wawakilishi wote wapeleke vikundi vyao katika majimbo yao, na vikundi hivyo ndivyo nilivyosaidia. Kila jimbo kuna vikundi ambavyo tuliwapa fedha hizi. Kwa hivyo, majimbo yote yalipata fedha hizo na baadae tulitoa kwa mujibu wa wilaya.

Wilaya ya Mjini kuna vikundi 27, Wilaya ya Magharibi vikundi 28, Wilaya ya Kati vikundi 28, Wilaya ya Kusini vikundi 25, Kaskazini ‘A’ 22, Kaskazini ‘B’ 14, Mkoani 16, Chake Chake 8, Weni 13, Micheweni 10 na wengineo vikundi saba. Jumla ya fedha zote zilizotumiwa ndio hizo nilizosema, shilingi 476,471,200/-.

Mhe. Salma Mohamed Ali: Mhe. Mwenyekiti, katika wilaya inayoongoza kwa kuwa na watu masikini ni Wilaya ya Micheweni. Lakini katika ugawaji wa zaka hapa inaonesha Wilaya ya Micheweni imepata vikundi 10 na hakuna mtu hata mmoja kwenye sehemu ya watu. Bado namuomba Mhe. Waziri anipe ufafanuzi zaidi kwa sababu ikiwa zaka inatolewa kwa masikini Wilaya ya Micheweni inaongoza kwa kuwa na masikini na hapa vikundi ni kidogo Mhe. Mwenyekiti, na katika sehemu ya watu hakuna hasa. Kwa hivyo, Mhe. Waziri anipe ufafanuzi zaidi ili nipate kufahamu.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Mwenyekiti, kweli pengine naweza nikakubaliana naye kwamba Wilaya ya Micheweni ndio inayoongoza kwa umasikinil kaini katika utoaji wa zaka hatutizami hayo yote, kwa sababu kama ukisema hivyo ina maana zaka yote tukaitoe katika Wilaya ya Micheweni.

Lakini la pili sheria za zaka Mashehe watanisaidia, lakini sheria za zaka pale inapotolewa zaka ndio inatakiwa igawiwe pale. Kwa hivyo, *actually* Micheweni kwa sababu hakuna aliyetoa hiyo zaka naweza nikasema isigawiwe, lakini yote hayo hatukutizama, tulitizama utaratibu mwengine wa kusaidia vikundi hivyo, ndio nikasema kwamba Micheweni kuna vikundi 10 ambapo ni shilingi 22,500,000/- tulizozitoa kwa Micheweni. Hizi ni pesa nyingi kwa sababu kuna wengine shilingi 29 milioni, 30 milioni, 26 milioni. Kwa hivyo, hizi Micheweni tumetoa kwa vikundi vya Micheweni, hivyo huu ndio utaratibu tunaofanya si kwa sababu Micheweni ndio wilaya yenye masikini wengi kwa hivyo twende tukawape kila mtu Micheweni itakuwa sivyo na kwengine hivyo hivyo kunahitajika itolewe zaka hii na hivyo ndivyo tulivyofanya. Nakushukuru Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika: Mhe. Mwenyekiti, nataka nimshukuru sana Mhe. Waziri kwa maelezo yake mazuri, lakini nataka kuongeza kidogo suala la magao wa pesa hizi ambazo zilikuja Wizara ya Kazi. Kulikuwa na mambo mengi yameangaliwa, kwa sababu vikundi vile vya ushirika havikupewa kwa sababu ni masikini kwanza nataka ieleweke hivyo, vikundi vile tulivipa kwa sababu ni vikundi ambavyo vimejiweka vizuri katika suala zima la kujiendeleza kiuchumi. Sasa suala lililojitokeza hapa ni kwamba tulishirikiana na Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana na walikwenda wao *physical* wakaangalia na maafisa wetu wa ushirika na vikundi vilivyoangaliwa ni vile ambavyo tayari vilisajiliwa, kwa bahati mbaya vikundi vingi katika maeneo mengi ambayo tumekwenda kuna upungufu wa pesa ilitokezea kupewa kidogo kidogo tofauti na maeneo mengine ni kwamba vikundi vile vilikuwa havijasajiliwa.

Mimi nilisimama hapa mebele ya Baraza hili nikawaambia Waheshimiwa kwamba tujitahidi kuvihamasisha vikundi vyetu na tuvisajili. Na Mheshimiwa Micheweni mbali ya vikundi vile ambavyo amesema Mhe. Waziri lakini Mhe. Subeit Khamis alisimama pale Wete akasema tuviongeze hivi vikundi vya Micheweni kwa sababu ni kidogo, vingi9 vilivyopelekwa vilikuwa vya Ole. Na mimi nikafanya upendeleo mwengine nikatoa pesa katika mafungu ya pesa za Unguja tukaongeza vikundi sita tukavipeleka Micheweni.

Lakini si hivyo tu Mhe. Mwenyekiti, kupitia Wizara ya Kazi tumepeleka boti ya uvuvi huko huko Wilaya ya Micheweni yenye thamani zaidi ya shilingi 14 mioni. Sasa nadhani masuala haya hayatolewi kwa sababu tu ya upendeleo fulani au kupendwa upande fulani, kunakuwa *criteria* ambazo zinatumika na sisi tutajitahidi katika kipindi hiki Mwenyezi Mungu akitujaalia bada ya Mwezi Mtukufu wa Ramadhan kutakuwa na mafungu mengine wale ambao walipata kidogo chini ya wenzao tutajitahidi na wao *Inshaallah* kuwaongezea ili tuweke mambo yote yende sawa sawa. Ahsante sana.

Mhe. Salma Mohamed Ali: Mhe. Mwenyekiti, nimeyasikia majibu ya mawaziri wote wawili, lakini Waziri wa Katiba na Sheria amesema kwamba pahala palipokuwa hapakutolewa zaka haifai kugawa zaka pale, na hapa inaonesha katika Wilaya ya Micheweni viko vikundi vilivyopewa. Sasa sijui hapa kwamba si kosa kufanya hivyo.

Halafu la pili Mhe. Mwenyekiti, ni hii zakka kutoa kwa vikundi. Mimi Mhe. Mwenyekiti, hili linanipa mashaka kwa sababu hivi vikundi kuna watu huchagua vikundi vyao tu wanavyovitaka. Sasa hapa pendekezo langu mimi hii zaka ipelekwe misikitini kwa sabahu misikitini kunapungua ubaguzi, lakini kwenye vikundi mtu akishaona hiki ni kikundi chake anachokipenda atapendekeza kipewe zaka. Mhe. Mwenyekiti, tuendelee.

Mhe. Mohamed Mbwana Hamad: Mhe. Mwenyekiti, na mimi nashukuru kupata nafasi hii ya kutoa maelezo na kutaka maelezo kwa ufafanuzi kwa Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria juu ya suala hili. Nilipokuwa nikichangia nilitaka nipate ufafanuzi juu ya ugawaji wa zaka katika mafungu haya ambayo yapo katika jadweli Nam. 8 ambalo limetufafanulia mambo mbali mbali. Lakini kabla ya kutaka ufafanuzi naomba nimueleze Mhe. Waziri kwambakuna kitu katika Uislamu kinaitwa za na sadaka. Zakka ina taratibu zake na sadaka zina taratibu zake, kwa kuwa mgao huu unaoonekana katika jadweli hili haunipi mimi ufafanuzi halisi kwamba hii ni zakka, naomba Mhe. Waziri arudie katika wale watu makundi manane aliyoyataja katika kutoa majumuisho yake kwamba makundi haya watu wanane ndio wanaostahiki kupewa zakka. Amewataja wakiwa ni mafakiri; masikini; wasafiri walioharibikiwa na wenye madeni ambayo yamewapindukia, wanaotumikia zakka yaani wale wanaofanya kazi ile ya zakka na wanaoingia sasa katika Uisilamu na katika mambo ya dini na wanaojikomboa na utumwa.

Nimepata mashaka kwamba Mhe. Waziri amesema kuwa walaji wa dawa za kulevya wanakombolewa na utumwa. Sasa namuomba Mhe. Waziri asema kwamba hii waliyotoa ni zakka ama nisadaka? Kwa sababu kama ni zakka basi zaka Mhe. Waziri ina makundi haya nane basi, idadi ya watu itategemea mahitaji, lakini wanaopewa zakka ni makundi nane haya tu.

Katika kitabu hiki Wilaya ya Mjini ina vikundi 27 watu nane naomba ufafanuzi wake. Vikundi hivi 27 watu nane wamepewa kima cha shilingi 40 milioni na mtiririko ambao unafuata chini. Mheshimiwa nasubiri maelezo *Inshaallah*.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Mwenyekiti, tuliotoa ni zakka sio sadaka na tumetoa kama alivyosema katika ile misingi nane niliyoitaja. Kwa

sababu wakati wa kutoa zaka kuna misingi yake inayotakiwa, sasa misingi hiyo minane yote tumeikamilisha na tumetoa zakka kwa mujibu wa mkakati huo. Lakini ukitizama katika kifungu hiki alichosema Mhe. Mjumbe kwamba kuna vifungu nane kuna vikundi halafu kuna na watu. Katika hii misingi minane pia inaonesha kwamba unaweza ukatoa zaka kwa mtu. Kwa hivyo, hapa kusema kuwa tumetoa vikundi kwa mfano 27 na hapa mkini kuna watu nane ambao tumewasaidia kwa zakka. Halikadhalika Magharibi, Kati, Kusini, Kaskazini 'A', Kaskazini 'B' na mwenginemo. Kwa hivyo, tusichanganyishe baina ya vikundi na watu, hapa tumeonesha kwamba vikundi tumewapa na watu ambao tulihisi kuwa wanastahiki kupewa zakka kwa mujibu wa haya makundi manane tuliyoyataja tumewapa.

Mhe. Mohamed Mbwana Hamad: Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa hapa hatubishani tunakwenda katika utaratibu ambao unafaa, katika mgao wa zakka Mhe. Waziri wa Kazi na Uwezeshaji alisema kwamba walipita katika vikundi na wao walishirikiana na Wizara ya Katiba na Sheria katika utoaji wa zaka. Lakini mionghoni mwa wanaopewa zakka Mhe. Mwenyekiti,k ni masikini na mafakiri, vikundi vilivyopewa zakka katika mgao wa Mhe. Waziri wa Uwezeshaji miongoni mwa vikundi hivyo kuna watu wana uwezo ni wafanyakazi wa serikali, kuna watu wana mifugo, kuna watu wana mashamba ya mikarafuu mimi nawajua. Kwa sababu miongoni mwa waliopewa vifungu hivyo mimi nawajua. Namuomba Mhe. Waziri aangalie utoaji wa zakka kama ulivyoelezwa ndani ya Qur-ani. Niseme kwamba si vibaya kama wangetoa zaka katika Wilaya ya Mjini mafakiri wangapi hata kama wangefika 400, masikini wangapi, wasafiri wangapi, wanaoingia katika Uisilamu sasa wangapi, mimi ningeona kweli kwamba tumekwenda katika utaratibu wa zakka.

Mhe. Waziri katika hoja zangu nilitaka anipe mfano wa wale walioingia katika Uisilamu ndani ya bajeti ya mwaka 2012 ambao walikuwa si Waisilamu wakaingia sasa katika Uisilamu ni wangapi. Nikamwambia kwamba, misikiti mingi tunayosali hapa Unguja tunaambiwa kwamba leo tutakuwa na watu watano au wawili au mmoja wameingia katika Uisilamu. Hebu anipe mfano katika mgao huu wa zakka kundi hili la wale wanaowezeshwa nyoo zao katika Uisilamu wamewapa wangapi. Ahsante Mheshimiwa.

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika: Mhe. Mwenyekiti, sikusudii kujibu zile hoja nyengine za kitaaluma ambazo Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria atazijibu, lakini amesema kitu kimoja nacho ni kweli. Lakini tujue kwamba kabla maamuzi yale hayajapitishwa Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana ambayo nina hakika wamefanya jambo lile kwa sababu ya elimu ambayo Mwenyezi Mungu amewajaalia wamelitafsiri vizuri,

pale ambapo tumewapa watu ambao wana uwezo, kwa sababu tumewapa pesa zile kwa nini? Kama mtu ana mifugo ni kweli, kama ana kiwanda cha sabuni ni kweli tumetoa, kama ana uwezo kweli tumetoa kwa saabu ya kuwasaidia zile zilikuwa na matumizi maalum.
Kwa sababu lengo letu baada ya mwaka mmoja kitakachopatikana pale ile *capital* itabakia pale pale, lakini ile faida itakayopatikana kutoka pale basi itawapa wananchi wengine kupata fursa kama ile, zile pesa ni kama zinaendelea tu. Kwa hivyo, haina maana kwamba tumewapa watu ni masikini sana hapana, tumewapa wale ambao wamekuwa na vikundi vimeji-*establish* vizuri, vina mwelekeo mzuri, vimejisajili na tayari wana rasilimali ambayo wanaweza kujiendeleza.

Sasa huwezi kwenda kumpa mtu ambaye hana kitu unakwenda kumpa pesa zile yatakuja kutokea yale ya AK na JK watu wakaolea na kufanya mambo mengine. Kwa hivyo, nadhani cha msingi hapa ni kwamba pesa zile zimetolewa katika misingi hiyo kwamba watu hawa tayari wameshajiendeleza. Hebu Waheshimiwa nendeni Gando tukaone maendeleo yaliyopatikana na vikundi vile, na tulikuwa hatuna sababu kwa nini vikundi vile tusiendelee kuvisaidia na tunaahidi tutaendelea kuvisaidia kwa sababu tayari vinajiwezesha wenyewe katika masuala kama hayo.

Kwa hivyo, la msingi hapa ni nini, tutofautishe kwa sababu tafsiri ya zakka kweli tunasema unawapa masikini, lakini mashehe wetu hawa wamesema si lazima hivyo kuna na njia nyengine, tusitafsiri aya kwa kuwa ile "***Kuluu-washrabuu****"* kunyweni tena mnakunywa mnachotaka tu, aa tumalize na huko mbele mambo yanavyokwenda, ahsante sana.

Mhe. Mohamed Mbwana Hamad: Mhe. Mwenyekiti, mimi naona kwamba kauli ya Mwenyezi Mungu haizungumzwi na ubabaishaji wa namna nyengine. Mwenyezi Mungu aliposema zakka wanapewa mafakiri na masikini na wanaofuatia, vikundi vinavyopewa fedha hizi kwa maana ya zakka si zakka, kuna zakka na sadaka Mheshimiwa. Zakka wanapewa watu maalum, zakka ukiwapa watu wasiostahiki si zakka, sadaka Mheshimiwa wanapewa watu wowote, zakka ina muda maalum na ukitoa katika muda usiofaa si zakka.

Kwa hivyo, mimi naomba Mhe. Waziri akubaliane name kwamba atayarishe mfumo unaofaa wa zaka na atayarishe mfumo wa sadaka kuwapa vikundi na watu wengine. Zakka unampa mtu aliyetajwa katika aya hiyo, sadaka hata kama mtu ana mamilioni ya shilingi hakuna tatizo kwenda ukampa na wewe mamilioni mengine. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri pamoja na taarifa zote ambazo zimetoka wafuate utaratibu sahihi *"**innama swadakatu lilfuqarai walmasakiin, illaakhir l-ayya"***. Ama sadaka ya kawaida haizingatii

kiwango, haizingatii mtu, haizingatii mapato ya mtu fulani. *Inshaallah* nashukuru kunipa nafasi hii. Tuendelee Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Mhe. Mwenyekiti, nilipokuwa nikichangia hotuba hii ya Mhe.Waziri nilizungumzia juu ya Mahujaji ambao walichukuliwa fedha zao na wakashindwa kufanya ibada ile ya hijja. Mhe. Waziri alipokuwa akijibu alisema kweli hilo jambo limejitokeza baada ya kufanya utafiti wake, lakini alichokigundua kwamba kuna vikundi visivyo rasmi ambavyo hivi navyo vimekuwa vikijihusisha na masuala haya na akatoa wito kwa wananchi waachane na vikundi hivyo na waende katika vile vikundi ambavyo viko rasmi.

Katika kitabu chake Mhe. Waziri amevitaja vikundi kama 11 humu ambavyo vinaonekana ndivyo vilivyokuwa rasmi, kikiwemo kikundi cha *Al-haramyn Development Fund*. Kwa taarifa Mhe. Mwenyekiti, mahujaji waliokuwa wametoa pesa zao wakashindwa kusafirishwa walitaka kusafiri kupitia kikundi hiki cha *Al-haramyn Development Fund*. Sasa maelezo yake anasema kwamba huenda mahujaji hao walitaka kusafirishwa kwa kikundi kisichokuwa rasmi, sasa hebu atupe maelezo ya kutosha na utafiti alioufanya kama kweli kafanya utafiti wa kutosha juu ya watu hawa. Kwa sababu taarifa nilizokuwanazo kwamba walitaka kusafiri kupitia katika kikundi hiki, ahsante.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Mwenyekiti, katika miaka yote wanapokwenda mahujaji wakirudi tunaandaa ripoti na tunaelezea matatizo yote yaliyojitokeza. Kwa hivyo, na mwaka huu uliopita ripoti hiyo hii hapa ninayo baada ya kutaka kujua kitu gani na kitu gani ambacho kilifanyika na kulikuwa na matatizo gani. Sasa ripoti hiyo inaonesha kwamba mahujaji wote tuliyowaorodhesha hapa walikwenda na kulikuwa hakuna matatizo. Al-haramyn anayosema Mhe. Mwakilishi ni kwamba huyu niliyemtaja yaani Mwenye Zanzibar *Development Organization* Al-haj Ameir Haji, yeye baada ya kupewa fedha hizo aliwaendea baadhi ya vikundi humu kikiwemo cha Al-haramyn kuwaambia kwamba anataka nafasi za watu ili awaweke. Lakini yeye Al-haramyn pamoja na vikundi vingine vilikuwa vimeshajaza wakamwambia sisi hatuna nafasi, kwa sababu huyu hakuji-*organize* ndio maana baada ya kufanya hivyo huyu hakuweza kuwasafirisha na ndio suala lililotokea na katika hiyo ripoti ipo kamili Mwakilishi naweza nikampa ripoti hii si siri. Kwa hivyo, ninachotaka kusema ni kwamba vikundi hivi vya Al-haramyn pamoja na vyengine hivi ni vikundi halali, vimesajiliwa na watu wake walikwenda hijja na wakarudi bila ya matatizo. Huyu mtu mmoja alitaka kutumia hii Al-haramyn ili awasafirishe hao watu wake aliowatapeli, na hawa wakasema wameshajaza kwa maana hiyo hawakwenda.

Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, ninachotaka kusema ni kwamba maelezo haya tuliyoyatoa ni sahihi kutokana na utafiti na ripoti ambayoa ninayo, Mhe. Mwakilishi naweza nikampa ripoti hii.

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana ndio dhamana katika kuwasafirisha Mahujaji na ndio dhama inayovidhamini hivi vikundi, na ndio dhama sisi tunaoelewa ndio wanao-*organize* kila kitu juu ya masuala ya Mahujaji. Mhe. Waziri anatwambia kwamba kuna kikundi hicho kisichorasmi inaonekana kinafahamika, pengine kuna hicho na vyengine. Sasa serikali kwa nini haichukue hatua juu ya vikundi vya aina hii ili athari kama hiyo isiweze tena kutokea katika siku za baadae. Kwa sababu inaonekana kwa maelezo yake hawa watu wanafahamika na wanafanya shughuli hizi hatimae wanaleta madhara kwa wananchi wetu na wao wenyewe Kamisheni ya Wakfu wapo, kwa nini wanaviruhusu vikundi kama hivi na watu kama hawa kufanya shughuli ambazo sio rasmi na wao huku kama serikali ambayo ndio dhamana ya wananchi wake wakielewa juu ya matendo hayo ambayo yanafanyika.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyosema kuna ripoti kwa kila mwaka na ripoti hii baada ya kuja na kuisoma ndio tukajua kwamba kuna watu matapeli. Mwaka huu yaani waliokwenda Hijja mwaka jana kwa hivyo baada ya kuandikwa ripoti ndio nikajua kwamba kuna watu matapeli. Sisi jukumu letu moja ambalo tumeshalifanya tumewatangazia wananchi yeyote anayetaka kwenda Makka kwamba asiende katika vikundi vya watu binafsi, ajiorodheshe katika vikundi ambavyo vimesajiliwa. Hiyo ndo moja ya hatua ambayo tumeshachukua na tunaendelea kuwaelimisha wananchi kuhusu suala hilo. Vile vile tunaendelea kuwaambia kwamba kuna watu ambao ni matapeli, kwa hivyo wajuweni. Sasa tunachukua hizo hatua ndogo ndogo za kusaidia hao watu.

Sasa hawa watu ambao walifanyiwa hivyo ndio nikasema tunawaomba sana waje tupate taarifa kamili na ushahidi na *detail* zote ili tuweze kuchukua hatua. Ingelikuwa kikundi hiki kimeandikishwa basi hatua moja ni kukifuta, lakini yote hayo lazima tupate-*detail* za mambo kama hayo. Kwa hivyo, bado mimi nasema na kwa kutumia nafasi hii nawaomba sana wananchi wasende kujiandikisha kwa watu kama hawa. Kuna vikundi maalum vinavyojulikana waende wakajiandikishe huko na watu wote hao waliotapeliwa tunaomba waje watuone ili tuweze kuchukua hatua zinazofaa.

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Nakushukuru Mhe. Mwenyekiti, na namshukuru Mhe. Waziri kwa maelezo aliyoyatoa naomba tuendelee.

Kifungu 0701 Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana Unguja 410,000,000
Kifungu 0702 Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana Pemba 100,000,000

Kifungu 0801 Afisa Msajili wa Hakimiliki 140,000,000
Kifungu 0901 Afisi ya Mrajis Vizazi na Vifo

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Mwenyekiti, nilipopata nafasi ya kuchangia nilichangia kifungu hiki na nashukuru Mhe. Waziri amejitahidi kutoa majibu pamoja na mapungufu yaliyoko. Lakini kulikuwa na ombi langu ambalo ni muhimu sana sikupata jibu.

Mhe. Mwenyekiti, nilisema tukiachilia mbali wale watu ambao walikuwa na ucheleweshaji wa kupata vyeti vyao vya kuzaliwa, lakini nilisema kuna wengine kwa bahati mbaya hawakupata vyeti hivi hawakushughulikiwa na wazazi wao, kuna wazee, kuna watu wazima, watu wa makamo, kuna vijana, wote hawa hawana vyeti vya kuzaliwa, ni Wazanzibari na wana haki zote za Kitanzania kwa kutumia Tume ya Uchaguzi ya *NEC*, lakini kwa Tume ya *ZEC* wanakoseshwa haki zao zote. Sasa kwa sababu ya umasikini na kwa sababu hawakuwa na kosa na Mwenyezi Mungu kasema usimhukumu mtu kosa ambalo halikumhusu, niliomba Mheshimiwa kwa makusudi kabisa afanye huruma atafute Mfuko popote wakati hawa ni Watanzania na ni lazima watetewe haki zao wasaidiwe kupatiwa vyeti vyao hivyo.Ule mpango ulioko wa kutoa shilingi zisizopungua 32,000 hivi sasa kwa kila mtu ambaye hana cheti wengine hawazimudu, lakini hili naona Mheshimiwa hakulizungumza.

Kwa hivyo naomba sijui katika suala hili la kusaidiwa hawa watu atafute popote fedha lakini wapate haki yao ni wengi tu. Mfano, Jimbo la Nungwi hivi sasa kuna watu mia nane na zaidi hawana vyeti vya kuzaliwa wote washakosa haki zao. Mhe. Waziri hakutoa jibu kuhusu hili, naomba anipe ufafanuzi

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, kama kuna swali hebu uliza swali lako.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Swali ni je, kalikubali lile ombi langu la kuwa atafanya kila inavyowezekana serikali ijitahidi kuhudumia kupatikana kwa vyeti kwa watu hawa wakati ni Wazanzibari.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nasikitika nilitoa jibu la kwa nini hivi sasa tunatoza shilingi 32,000 na utaratibu mzima ambao tumeuchukua hivi sasa ili tupeleke serikali kwa kupunguza hizo shilingi 32,000, kwa sababu hizi ni fedha ambazo zimeshawekwa na serikali. Kwa hivyo, mimi siwezi kusema kwamba badala ya shilingi 32,000 tutoze 20,000, lazima kiutaratibu niandae waraka na waraka huo nimeshauandaa na umeshapitia katika kamati ya uongozi, tunasubiri kupelekwa katika makamati ya makatibu wakuu na ikitoka kwa makatibu wakuu itakwenda serikalini na

serikali wataamua kutoka shilingi 32,000 kama wataongeza au watapunguza, hayo ni maamuzi ya serikali na hiyo ndio hatua tuliyofika ili kuwasaidia hao watu.

Mhe. Mwenyekiti, lakini suala la pili ni kwamba alizungumzia wazee watu wazima wenye umri mrefu. Mhe. Mwenyekiti, katika *late registration* kuna utaratibu wake, unajaza fomu kuna maswali pale na mambo chungu nzima na tunataka watu wote wajaze fomu kwa kumbukumbu zetu, lakini bado sisi kwa watu wazima kama hao basi tunatoa baadhi ya masharti tunamtizama yule mzee, halafu kuna mambo mengine ambayo tunahisi kweli yule mzee anayo kwa mujibu wa uzee wake. Kwa hivyo, yote hayo tunayatizama yanapoletwa katika ofisi yetu. Kwa hivyo, suala la kumpatia mzee *late registration* na baadae cheti cha kuzaliwa halina matatizo, isipokuwa hivi sasa kwa sababu maamuzi ya Baraza la Mapinduzi hayajapatikana ya kupunguza bei, itakuwa bei ni hiyo hiyo mpaka hapo ambapo tutapata *authority* kutoka kwa Baraza la Mapinduzi, kwamba sasa tupunguze bei ya cheti cha *late registration*.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Mwenyekiti, nashukuru kwa majibu mazuri ya kutia tamaa, nampongeza Mhe. Waziri. Lakini Mhe. Mwenyekiti hawa wazee Serikali hii ya Mapinduzi ya Zanzibar, awamu tu sio hii pamoja na kuwa walikuwa hawana vyeti vya kuzaliwa, walikuwa na haki ya kupiga kura na walipata vitambulisho vya kupigia kura, mpaka imeondolewa hivi juzi kwa sababu ya vyeti vya kuzaliwa. Kwa vile Mhe. Waziri wizara yake ina tume maalum ya kurekebisha sheria, haoni kuwa iko haja kwa vile hawa walipewa na serikali na serikali hii hii ikawakosesha haki zao kwa hawa waliokuwa wameshapewa wakati na hii iko katika utaratibu, wakarudishiwa angalau hizi haki zao wakajiona ni watu sawa sawa na wenzao.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Mwenyekiti, utaratibu wa kurekebisha sheria ni mkubwa na mzuri, hainitaki mimi waziri tu, lakini hata mwakilishi mwenyewe akiona kwamba kuna kitu ambacho kinamkwaza basi anaruhusiwa kuleta *private members motion*, anaruhusiwa kuleta *private bill*. Kwa hivyo, hizo ni jukumu la Baraza la Wawakilishi na ninawaomba wawakilishi wafanye, hawajawahi kufanya tokea lianzishwe Baraza hili hebu wachangamke kidogo.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu ya wakati tuendelee.

Kifungu 0901	Ofisi ya Mrajis Vizazi na Vifo Unguja	278,759,000
Kifungu 0902	Ofisi ya Mrajis Vizazi na Vifo Pemba	74,701,000
Jumla ya Fungu		**2,750,000,000**

(Vijifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya Mabadiliko yoyote)

FUNGU 46 - TUME YA KUREKEBISHA SHERIA

Kifungu 0201	Utawala Unguja	483,000,000
Jumla ya Fungu		**483,000,000**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya Mabadiliko yoyote)

FUNGU 14 - MAHAKAMA KUU ZANZIBAR

Kifungu 0201	Utawala Unguja	150,000,000
Jumla ya Fungu		**150,000,000**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya Mabadiliko yoyote)

FUNGU 35 - OFISI YA MKURUGENZI WA MASHTAKA

Kifungu 0201	Utawala Unguja	150,000,000
Jumla ya Fungu		**150,000,000**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya Mabadiliko yoyote)

FUNGU 36 - WIZARA YA KATIBA NA SHERIA

Kifungu 0401	Idara ya Mipango Sera na Utafiti	1,854,313,000
Jumla ya Fungu		**1,854,313,000**

(Vijifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya Mabadiliko yoyote)

(Baraza lilirudia)

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Mwenyekiti, ilivyokuwa Kamati ya Matumizi imejadili na kupitisha makadirio ya fedha ya wizara yangu bila ya mabadiliko. Sasa naomba kutoa hoja kwamba Baraza lako tukufu liyakubali makadirio hayo.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, sasa niwahoji wale wanaoikubali hoja ya Mhe. Waziri wanyooshe mikono. Wanaokataa. Waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Waheshimiwa Wajumbe, niwashukuru sana kwa utulivu pamoja na michango yenu mbali mbali. Kwa hivyo, nachukua fursa hii kuahirisha kikao hiki hadi Jumatatu saa 3:00 za asubuhi.

(Saa 3:10 usiku Baraza liliahirishwa hadi
tarehe 08/07/2013 saa 3:00 za asubuhi)